

3 APRILI, 2018

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 3 Aprili, 2018

(*Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi*)

### WIMBO WA TAIFA

#### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

#### KIAPO CHA UAMINIFU

Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliapa:-

Mhe. Dkt. Godwin O. Mollel

Mhe. Maulid S. A. Mtulia

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

#### TAARIFA YA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitasoma kwenu taarifa ya Mheshimiwa Spika ambayo imetolewa chini ya Kanuni ya 33 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2016.

3 APRILI, 2018

Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa 10 wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada miwili ya Sheria ya Serikali kama ifuatavyo:-

Muswada wa kwanza ulikuwa ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa mwaka 2017 (*The Written Laws Miscellaneous (Amendments) No. 5 Bill, 2017*). Muswada wa pili ni Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa mwaka 2017 (*The Public Service Social Security Fund, Bill, 2017*).

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii Mheshimiwa Spika analiarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Miswada hiyo miwili imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi zinazoitwa:-

Kwanza, Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 ya mwaka 2018 (*The Written Laws Miscellaneous (Amendments) Act No. 1, 2018*).

Pili; Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma Na. 2 ya mwaka 2018 (*The Public Service Social Security Fund Act, No. 2 of 2018*).

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo taarifa ya Mheshimiwa Spika. Tutaendelea, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya

3 APRILI, 2018

Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS  
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (*The Paris Agreement Under the UN Framework Convention on Climate Change*).

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):**

Maoni ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (*The Paris Agreement under the UN Framework Convention on Climate Change*).

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI (K.n.y. MHE. ALLY SALEH ALLY - MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (*The Paris Agreement under the UN Framework Convention on Climate Change*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

3 APRILI, 2018

Na.1

### **Kasi ya kupambana na Dawa za Kulevyaa Nchini**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA (K.n.y) MHE. MWANTUMU  
DAU HAJI aliuliza:-**

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inarejesha kasi ya kupambana na dawa za kulevyaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA  
NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mantumu Dau haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeongeza kasi na harakati za kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevyaa nchini baada ya Bunge lako Tukufu kutunga Sheria mpya ya Kudhibiti na Kupamabana na Dawa za Kulevyaa Na. 5 ya mwaka 2015. Sheria hii imeipa Serikali Mamlaka ya kuanzisha chombo chenye nguvu cha kudhibiti na kupambana na dawa za kulevyaa, ambacho kiliundwa rasmi mwezi Februari mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka hiyo imepewa nguvu Kisheria ya kuweza kukamata, kupekua, kuzuia mali na kuchunguza mashauri yote ya dawa za kulevyaa na makosa mengine yanayohusiana nayo ikiwemo mali zitakazothibitika kupatikana kutokana na dawa za kulevyaa. Hata hivyo, Serikali katika kuongeza kasi ya kupambana na dawa za kulevyaa, mwaka 2017 ilifanya marekebisho makubwa ya sheria hiyo na kuipa nguvu maradufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takribani mwaka mmoja sasa tangu kuundwa kwake hadi kufikia mwezi Februari mwaka 2018, Mamlaka imekwishakamata jumla ya watuhumiwa 11,071; kati ya hao, watuhumiwa 3,486 ni wafanyabiashara wa dawa za kulevyaa na tayari

3 APRILI, 2018

wameshafikishwa Mahakamani. Kutokana na kuongezeka kwa kasi ya kupambana na dawa za kulevyta imesababisha kupungua kwa kiasi kikubwa cha matumizi ya madawa ya kulevyta nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote kushiriki kikamilifu katika juhudzi za Serikali za kupambana na dawa za kulevyta kwani madhara yanayotokana na matumizi ya dawa hizo kwa namna moja ama nyingine yanatuathiri sote kwa njia mbalimbali ikiwemo kuongeza vitendo vya uhalifu, matumizi ya Serikali katika kuwahudumia waathirika pia.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri anayehusika na masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, kutokana na kwamba bado hakujawa na udhibiti wa kutosha wa kuzuia madawa ya kulevyta yasipenye na kutokana na tulivyomsikia Mkuu anayeshughulika na udhibiti wa madawa ya kulevyta kwamba kule Zanzibar bado kunatumika kama kipenyo cha kupitisha madawa haya ya kulevyta. Je, Serikali imejipangaje kuongeza ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ili kudhibiti na kuhakikisha kwamba kule Zanzibar hakuwi mlango wa kupitisha madawa haya ya kulevyta?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli baada ya jitihada na juhudzi kuwa kubwa sana Tanzania Bara, hasa kazi

3 APRILI, 2018

kubwa sana ambayo ilifanywa na Mamlaka ambayo imewafanya wafanyabiashara wengi sana wa dawa za kulevyo nchini na wengine kukimbilia Zanzibar, ni kweli sasa Zanzibar imeanza kutumika kama sehemu ya uchochoro wa wafanyabiashara ambao wanakimbia kutoka Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayofanyika hivi sasa ni kuhakikisha kwamba tunaanza kufanya kazi kwa pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kwanza kutengeneza mfumo mzuri wa kusaidia katika kuhakikisha kwamba tunawabaini wafanyabiashara hata hao wanaokwenda nje Tanzania Bara ambao wanakwenda Zanzibar. Pia vimekuwepo vikao vya mara kwa mara kati ya Mamlaka na wataalam kutoka kule Zanzibar, lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza mfumo mzuri wa udhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwondolee hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hiyo inaendelea na tayari tatizo hilo limebainika, naamini muda siyo mrefu sana maridhiano yakikamilika basi tutafanya kazi pia kuhakikisha kwamba tunazuia na upande wa Zanzibar. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shomari, swalii la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa, Serikali inajizatiti kuzuia suala hili la madawa ya kulevyo, Je, itatuhakikishia viyi kufanya kila Mkoa wa Tanzania kuwa na *sober house* ili kudhibiti matatizo haya? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikakati ambayo tumejiwekea ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevyo, moja ya mkakati ni kitu ambacho kinaitwa *harm reduction*. *Harm reduction* ni kupunguza madhara kwa watumiaji wa

3 APRILI, 2018

madawa ya kulevyta hasa wale ambao wanatumia madawa ya *heroin* ambao wanakwenda kutibiwa kwa kutumia *Methadone*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali pamoja na kuwa na mpango wa kuweka vituo vingi vya *Sober houses* lakini tunatumia hospitali katika Mikoa yetu kuwa na madirisha maalum kwa ajili ya kuwahudumia watu ambao wameathirika na madawa ya kulevyta. Kwa hiyo, naamini huduma itasambaa Nchi nzima na wengi watapata huduma hiyo kuititia katika hospitali za Mikoa katika maeneo husika. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania tumepewa heshima ya kuwa ni katika ya nchi chache ndani ya Bara la Afrika ambayo inafanya vizuri, kuwa na sheria nzuri na inasimamia vizuri udhibiti wa dawa za kulevyta katika nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo, Umoja wa Mataifa umekubaliana kwamba mwaka huu wa 2018, nchi zote za Bara la Afrika, Viongozi wanaosimamia Sheria za Kudhibiti Dawa za Kulevyta katika nchi zao watakuwa na mkutano wao mkubwa sana lakini utafanyika ndani ya Tanzania ili waweze kujifunza zaidi ni kwa kiasi gani Tanzania imefanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongeza kuhusu suala hili la kutengeneza mfumo wa utengemaa kwa waathirika wa dawa za kulevyta, Serikali kuititia Mamlaka kazi kubwa

3 APRILI, 2018

tuliyoifanya katika kipindi hiki kifupi ni kuandaa miongozo na utaratibu wa uendeshaji wa *sober houses* katika nchi yetu ya Tanzania; miongozo hiyo sasa ipo tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali kwa kuanza kujifunza *model* nzuri ya *sober houses* katika nchi yetu ya Tanzania tumetengeneza tayari tumeshajenga na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana amezindua *National Rehabilitation Center* katika Mji wa Dodoma na itaanza kufanya kazi baada ya muda siyo mrefu, hiyo itakuwa ni *model* ya *Sober houses* na *rehabilitation centers* nyingine ambazo tunazihitaji katika nchi ya Tanzania za kuwasaidia hawa waraibu wa dawa za kulevyu kurudi katika hali yao. Hivyo, Serikali inafanya kazi kubwa sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Amir swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Tunaona jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali katika kudhibiti suala hili la madawa ya kulevyu na wakati yanapokamatwa tunaoneshwa. Je, ni kwa nini *cocaine* na *heroin* wakati zinateketezwa hatuoneshwi tunaoneshwa bangi? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwamba amekiria amekuwa akiona uteketezaji wa mashamba ya bangi ambao kwa kipindi cha Januari, 2017 mpaka Disemba, 2017 takribani ekari 542 za bangi zimeteketezwa na hii ikiwa ni kazi nzuri ambayo imefanywa na mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake alitaka kujua kwa nini hatuoni uteketezwaji wa madawa mengine

3 APRILI, 2018

aina ya *cocaine* na *heroin*. Kwa *nature* ya madawa yenyewe namna uteketezaji wake uko tofauti na utaratibu unaotumika ni utaratibu ambao kwanza kabisa utahakikisha tunalinda afya na mazingira vilevile upo utaratibu ambao mamlaka unautumia katika uteketezaji huu ambao kwa kiwango kikubwa sana haijawa rasmi kwamba inaoneshwa kila wakati, lakini ni kweli kazi kubwa imefanyika katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka ninapozungumza hivi sasa takribani kilo 196 za *heroin* zimeteketezwa ikiwa ni kazi nzuri ambayo inafanywa na mamlaka. Kwa hiyo, siyo kwamba kazi hii haifanyiki inafanyika lakini kwa uangalizi mkubwa sana, inahitaji pia kuangalia na athari za mazingira.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naambiwa hapa ulikuwa umesimama.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake sahihi na niunge mkono kwamba ni kweli madawa mengine yanateketezwa kwa uangalifu sana kwa sababu hata bangi tu nilienda kuteketeza nilipotoka pale ilibidi niende kwa Daktari kuangalia kama haijaniingia na Daktari aliniambia sijavuta. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde Mbunge wa Mtera, sasa aulize swalii lake.

Na. 2

**Ufanisi wa TARURA**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE** aliuliza:-

Serikali iliunda chombo kinachosimamia barabara za Vijiji na Mijini kinachoitwa *TARURA*:-

3 APRILI, 2018

Je, chombo hicho kitaanza lini kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa kwani barabara hizi ni mbaya sana hasa wakati wa masika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*) ilianzishwa kwa Sheria za Wakala za Serikali, Sura 445 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 211 la tarehe 12 Mei, 2017. *TARURA* imeanza rasmi tarehe Mosi Julai, 2017, kwa ajili ya utekelezaji wa matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 108,946.2 katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* imeidhinishiwa shilingi bilioni 230.8 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 34,024. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 98.5 zimetolewa na kutumika kujenga barabara zenye urefu wa kilometa 4,188.31, madaraja 35, makaravati makubwa 43 na makaravati madogo 364.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, barabara zilizojengwa katika Jimbo la Mtera zina urefu wa kilometa 93.3 kwa gharama ya Sh.356,737,115.80. Barabara hizo ni:-

Handali – Chanhumba – Igandu - Nghahalezi (kilometra nne); Nghahalezi – Miganda – Idifu - Iringa Mvumi - Mlowa barabarani (kilometra tano); na Nagulomwitikila - Huzi - Ilangali (kilometra 17) kwenda Nhinihi - Wiliko (kilometra 20); Mlowa barabarani - Makangw'a (kilometra 12); Manzase – Sasajila - Ilowelo (kilometra 21.3); Chipogolo - Loje - Igungili (kilometra 14). Wakandarasi wanaendelea kufanyakazi na wanatarajia kukamilisha kazi hiyo Mei, 2018.

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, TARURA imeomba kutengewa kiasi cha shilingi bilioni 243.3 kwa ajili ya ujenzi wa barabara zenyе urefu wa kilometa 23,465.05, ukarabati wa madaraja 117, mifereji ya mvua yenye urefu wa mita 67,844 na makaravati 1,881 kwa nchi nzima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Livingstone Lusinde, swalı la nyongeza.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu, hata hivyo napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la kwanza; urefu wa barabara alizotaja na millioni 350 kweli hapo kuna matengenezo ya barabara kwa kiwango cha changarawe au ni kwa kiwango cha tope?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la pili; kwa kuwa mvua za mwaka huu Mungu ametupa neema zimekuwa nyingi na zimetusaidia sana kwa upande wa kilimo, vilevile zimeleta uharibifu mkubwa sana wa barabara na madaraja, Mheshimiwa Waziri anatuambiaje juu ya matengenezo mazuri na yenye maana kwa ajili ya wananchi kuweza kupitisha mazao yao ambayo wanategemea kuyavuna ili waweze kujilettea maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Kandege, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, anaulizia juu ya idadi ya kilometra ambazo nimezitaja na kiasi cha fedha ambacho kimetumika je, tumetengeneza kwa ubora uliotarajiwा au tumeyatengeneza kwa kutumia tope.

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hatujatumia tope kwa sababu yeye mwenyewe ni shuhuda kwamba tumehama kutoka katika matengenezo yaliyokuwa yanafanywa na Halmashauri pale ambapo kila Mheshimiwa Diwani alikuwa akiomba angalau apate hata kilometa moja au kalivati moja katika aeneo lake, mwisho wake inakuja inafikia kwamba hata ile thamani ya pesa ambayo imetumika haikuweza kuonekana na hivyo tukawa tunarudia kila mwaka katika matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lusinde na bahati nzuri na yeye ni shuhuda amekuwa akifanya kazi nzuri ya kupita kwenye Jimbo lake hebu akalinganishe kazi ambayo imefanywa na chombo hiki cha *TARURA* linganishe na jinsi ambavyo kazi zilikuwa zinafanyika hapo awali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili ameongelea neema ya mvua ambayo tumeypata na sisi sote tukiwa ndani ya Mkoa wa Dodoma ni mashuhuda, tumeypata mvua ya kutosha, mvua ni neema, lakini kila neema nayo inakuja na dhahama yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba nimhakikishie chini ya *TARURA* na ndiyo maana kuna maeneo ambayo kumekuwa na mataengenezo na maombi maalum ili kuhakikisha kwamba barabara hizi zinapitika vipindi vyote na kiasi cha pesa ambacho chombo hiki kimeombewa kama Bunge lako Tukufu itaidhinisha chini ya usimamizi madhubuti hakika barabara zitatengenezwa kwa kiwango kizuri na kitakachowezza kupita katika vipindi vyote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hebu angalia hawa Wabunge wote wana maswali na *TARURA*. Mheshimiwa Mary Chatanda, swali la nyongeza:

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwanza napongeza *TARURA* kwamba wameanza kazi vizuri hususani katika Mji wangu wa Korogwe, lakini napenda kujua je, Wizara ina mpango

3 APRILI, 2018

gani sasa wa kuwawezesha hawa *TARURA* hususani kwenye hizi Halmashauri za Miji pamoja na kwamba wanawapa fedha za kujenga barabara zile kwa kiwango cha changarawe, sasa wapewe fedha za kutengeneza ile mifereji kwa kiwango cha kutumia mawe ili kusudi wasiweze kurudia mara kwa mara kutengeneza zile barabara? Wana mpango gani wa kuwatengea fedha ili Miji hii iweze kuwa na barabara zilizo imara kwa kupitia kuweka mawe misingi yao? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri yote ya msingi ya mwanzo yaliyoweza kutolewa. Naomba nimpongeze mama Mary Chatanda ni mlongoni mwa Wabunge ambaao tulipambana sana katika ujenzi wa barabara na stendi yake ya pale Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa utengenezaji katika Halmashauri za Mji kwanza tunatumia mradi wa *UGLSP* ambaao tunagusa takribani Manispaa na Halmashauri zote za Mji. Kwa hiyo, naomba ni wahakikishie Wabunge wote ambaao wako katika Halmashauri za Miji na Manispaa mpango wetu mkakati ni kuhakikisha maeneo haya tunayabadilisha kwa ajili ya ujenzi katika maeneo haya kwa tabaka la lami. Huu ndiyo mpango wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika ile Miji Mikuu Saba ambayo nimezungumza tutaaendelea kuboresha suala la mifereji, suala la barabara kwa kiwango ambacho tunajua kwamba barabara zetu tunataka *guarantee* ya miaka 20 ndiyo tuweze kuzifanyia *service*, ndiyo maana hatuko katika *supervision* ya hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba nikiri kwamba *TARURA* tuna mtandao wa barabara takribani kilometra 108,000 ambaao ni matandao mkubwa sana, lakini ukiangalia kutokana na suala la kisera la mgawanyo wa

3 APRILI, 2018

Mfuko wa Barabara ambao asilimia 30 inakuja *TARURA* na asilimia 70 inaeda *TANROAD*, eneo hili ndilo lina changamoto kubwa. Baadaye tutaangalia nini cha kufanya, lengo letu kubwa ni kwamba Halmashauri zote ziweze kuitika kwa sababu wananchi huko ndiko uchumi unapojengeka. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutulie kidogo. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza. (*Kicheko*)

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninachotaka kujua *TARURA* ni chombo ambaco kimeundwa hivi karibuni, nataka kujua *TARURA* sasa kwa sababu barabara wanazoshughulikia ni zile zilikuwa zinashughulikiwa na Halmashauri chini ya Madiwani. Je, hiki chombo sasa kinasimamiwa na mamlaka gani kwa niaba ya wananchi, kwa sababu hawaingii kwenye Baraza la Madiwani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba *TARURA* ni chombo ambacho kimeanzishwa hivi karibuni. Kimsingi taarifa ya kazi zinazofanyika taarifa yake inapelekwa kwenye chombo kinaitwa *DCC* na katika *DCC* Waheshimiwa Wabunge wote wanakuwemo kwenye kile chombo, lakini pia kila Mwenyekiti wa Halmashauri husika anahudhuria kwenye hicho kikao na ndio fursa ambayo kwa sasa hivi *TARURA* inatoa taarifa juu ya utekelezaji wa kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, hata katika vipaumbele vya barabara ambazo zinaenda kutengenezwa ni wajibu wa Halmashauri kwa kushirikiana na Madiwani wote tunaidhinisha barabara ambazo ni vipaumbele, lakini *TARURA* inapelekewa kulingana na bajeti

3 APRILI, 2018

sasa wao ndio wanasema katika hizi barabara tunaenda kutengeneza barabara zipyi, lakini fursa kama *forum* ya Waheshimiwa Madiwani bado ipo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Saidi Mtulia, swali la nyongeza. (*Makofii*)

**MHE. ABDALLAH S. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *Alhamdulilah.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana, lakini pia nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima, nina afya njema, akili timamu na utayari wa hali ya juu ya kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Kinondoni na tunasema dua la mwewe halimpati kuku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo letu la Kinondoni na Manispaa ya Kinondoni kwa ujumla *TARURA* inafanya kazi vizuri, tunawapongeza sana. Hata hivyo, Manispaa yetu ya Kinondoni ina barabara za kiwango cha lami siyo zaidi ya asilimia 10 za barabara zote katika Manispaa ya Kinondoni na tumewaambiwa wananchi tunataka kuleta Kinondoni mpya; je, *TARURA* ina mpango gani wa kutuongeza barabara zetu katika kiwango cha lami ili angalau kufikia asilimia 50 kama siyo asilimia mia moja? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) - MHE. JOSEPH S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa, *welcome again* uko katika nafasi iliyo sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo chombo chetu *TARURA* kinafanya kazi vizuri ni pamoja na Manispaa ya Kinondoni, nimepata fursa ya kwenda

3 APRILI, 2018

kutembelea, Halmashauri zingine zinatakiwa kwenda kuiga na kutazama kazi nzuri ambayo inafanywa na *TARURA* Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la kuungeza ili angalau tufike asilimia 50 ya barabara zote kuwa za lami, kati ya Miji ambayo ina fursa ya kupata maendeleo kwa maana ya miundombinu ya barabara ni pamoja ni Jiji letu la Dar es Salaam. Naamini katika mpango mzima wa kuboresha Jiji la Dar es Salaam na *program* zinazoendelea hakika, barabara za Kinondoni zitahama kutoka hiyo asilimia kufika asilimia 50 katika kipindi ambacho siyo kirefu sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu niongezee katika majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba katika eneo la Kinondoni ambako Mbunge aliyeapishwa leo Mheshimiwa Mtulia anatoka ni kwamba hiyo *coverage* tutaifika haraka sana kwa sababu tuna *combination* mbili; tuna mradi wa *DMDP* ambaao Mheshimiwa Mbunge anaufahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu una kazi kubwa sana ya kuboresha miundombinu ya barabara za lami katika Jiji la Dar es Salaam na eneo la Kinondoni ni eneo moja wapo, lakini kuna upande mwingine upande wa *TARURA*, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge aondoe hofu zile ahadi alizozisema kwa wananchi wake, naamini ikifika mwaka 2020 zote zitakuwa zimeteklezwa tena kwa zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Naamini huo utekelezaji wa ahadi zote unahusu Majimbo yote. Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel. (*Makofii*)

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Hata hivyo, nitumie fursa hii kuwashukuru

3 APRILI, 2018

wananchi wa Siha kwa kuniamini tena na kuhakikisha hawa wanaosema muda nawapiga kipigo ambacho hawajawahi kukisikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara yetu ya kutokea Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwenda kwenye Kata ya Biriri kukutana na barabara inayotokea Sanya Juu kuelekea mpaka *KIA* (Kilimanjaro *International Airport*), kwa mwaka jana ni katika barabara mbili ambazo zilikuwa zipandishwe hadhi kuingizwa *TANROAD* ikashindikana ikawa imepanda barabara moja ya Mwanga. Nataka kumuuliza Waziri mwaka huu basi isidunde kama zawadi ya watu wa Siha kwa uamuzi wa busara walioufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) - MHE. JOSEPH S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze na kumkaribisha sana Dkt. Mollel na kumhakikishia kwamba yuko katika nafasi ambayo ni salama sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kupandisha hadhi barabara ambayo anaiongelea ili iwe chini ya *TANROAD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shuhuda kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi tulikuwa tunapenda barabara za Majimboni kwetu zipandishwe zichukuliwe na *TANROADS*, lakini ni kwa nini tulikuwa tunataka zichukuliwe na *TANROADS*? Ni kutokana na namna ambavyo barabara ambazo ziko chini ya *TANROADS* zimekuwa zikhudumiwa kwa namna nzuri. Ndiyo maana kama Bunge tukaona kwamba ni vizuri tukaanzisha chombo ambacho kitakuwa kinafanya kazi madhubuti kama ambavyo zimekuwa zikifanywa na *TANROADS*.

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie, kwa kasi ambayo tumeanza nayo na jinsi ambavyo *TARURA* imeanza kufanya kazi, nimtoe mashaka, barabara ambayo anaisemea chini ya *TARURA* itakuwa na hadhi na ubora sawa na barabara ambazo zinatengenezwa chini ya *TANROADS*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 3

### **Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Nduli**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Kiwanja cha Ndege cha Nduli kipo katika mpango wa Serikali wa Ujenzi wa viwanja 11:-

(a) Je, ni lini kiwanja hicho kitajengwa?

(b) Mpaka sasa hakuna kituo cha kujaza mafuta katika kiwanja hicho; je, ni utaratibu gani unaotumika ili kiwepo kituo cha mafuta katika kiwanja hicho?

### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS JOHN KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:

(a) Kiwanja cha Ndege cha Nduli kililichopo Mkoani Iringa ni mionganini mwa viwanja 11 vya ndege vilivyo fanyiwa upembu zi yakinifu na usanifu wa kina uliomalizika mwezi Mei mwaka 2017. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Serikali ilitenga fedha za ndani kwa ajili

ya maandalizi ya ujenzi wa kiwanja hicho ikiwa ni pamoja na kutangaza zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutokana na Benki ya Dunia kuonesha nia ya kufadhili ujenzi wa uwanja huu, Serikali ilisitisha taratibu za ndani za manunuzi ili kusubiri manunuzi kufanyika kwa kuzingatia taratibu za Benki ya Dunia. Hivyo, uwanja huo utaanza kujengwa mara moja baada ya taratibu hizo kukamilika.

(b) Kwa sasa kiwanja hiki hakina ndege za kutosha zinazoweza kuvutia uwekezaji wa kituo cha mafuta. Ni vema ielevweke wazi kwamba sera ya uwekezaji katika viwanja vyta ndege inatoa fursa ya kuuza mafuta ya ndege kwa makampuni binafsi yenye leseni ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga *TCAA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makampuni yenye leseni hizo na yaliyoingia mikataba ya biashara ya mafuta ya ndege na Mamlaka ya Viwanja vyta Ndege Tanzania *TAA* ni Puma, *Oilcom*, *Total* na *Prime fuels*. Kwa hiyo, ni utashi wa makampuni ya mafuta na nguvu ya soko inayosukuma uwekezaji wa biashara ya mafuta katika viwanja vyta ndege. Ni matumaini yangu kwamba kiwanja hiki kitakapokamiliika kujengwa kitawavutia wawekezaji na hatimaye kumaliza tatizo hili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza kabisa nianze kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mapokezi makubwa kabisa ya ndege ya *Bombadier* ambayo jana ilitua na Mheshimiwa Rais akiwa anaongoza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili pia niipongeze Serikali kwa kuanza sasa kujenga kiwanja chetu cha Nduli

3 APRILI, 2018

kwa sababu nina imani kabisa sasa hata utalii utafunguka katika Mkoa wetu wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ndege ya *Bombadier*ina uwezo wa kutua katika kiwanja chenye urefu wa kilometra 1.2 na kiwanja chetu cha Nduli kina urefu wa kilometra 1.6, tatizo ni kipande tu kidogo cha mita kama 100 ambacho ni kibovu sana ambacho hakiwezi ndege kubwa kutua na hata zile ndege ndogo ambazo zinatua, zinatua kwa matatizo makubwa sana na mpaka sasa hivi kiwanja chetu kina abiria karibu 20,886,000. Je, Serikali sasa haioni umuhimu sasa wa kujenga hicho kipande kidogo cha mita 100 ili tuweze kupata ndege kubwa na hizo ndogo zipate kutua vizuri wakati tunasubiri huo ujenzi wa kiwanja hicho, kwa ufadhili wa Benki ya Dunia? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; nimesikia tayari zoezi la uthamini wa mali limeshaanza katika kiwanja chetu cha Nduli. Hofu yangu kubwa ni kwamba zoezi hili huwa linafanyika mapema kabisa lakini huwa linachukua muda mrefu sana kwa wananchi kulipwa mali zao, nina mfano halisi kabisa wa kiwanja cha ndege cha Songea ambacho toka mwaka 2010 karibu miaka nane bado hawajalipwa na vilevile hata barabara yetu ile ya mchepuo ilichukua karibu miaka sita mpaka wananchi kuanza kulipwa. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kuwa wananchi hawa amba wanapisha hiki kiwanja wanalipwa mapema zaidi?

Mheshimiwa Naibu Sika, ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nizipokee pongezi nyingi ambazo amezitoa kwa kupokea ndege ambayo jana Mheshimiwa Rais ameipokea. (*Makof*)

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia uboreshaji wa kiwanja hiki, amekuwa akifuatilia na mimi binafsi nilifika kuona hali ya uwanja. Suala la kwanza ambalo amelizungumzia juu ya kuongeza urefu wa kiwanja. Ilikuwa imetengwa shilingi bilioni 47 kwa ajili ya upanuzi wa kiwanja hiki lakini kwa bahati nzuri tumepata fedha kwa udhamini wa Benki ya Dunia tutakwenda kujenga kwa thamani ya shilingi bilioni 94.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha kwamba huduma nyingi katika uwanja huu zitakuwa zimeongezeka. Hii ni pamoja na kuweka taa za kuongozea ndege, kuongeza urefu wa uwanja na sasa huu uwanja pamoja na taa zitakapowekwa utakuwa na urefu wa mita 2,500 kwa maana utaweza kumudu kiwango hiki ambacho Mheshimiwa Mbunge anaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge, wananchi wa Iringa na Watanzania kwa ujumla tuvute subira, tunaenda kuboresha huu uwanja utakwenda kuwa wa kisasa pamoja na kuweka majengo, jengo la abiria pamoja na jengo la wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni ushahidi tosha kwamba sasa hivi *compensation* hazichelewi kulipwa. Viko viwanja ambavyo vinaendelea kujengwa kule Shinyanga, *compensation* imelipwa lakini uthamini umeshakamilika, tunaendelea kuhakiki wenzetu wa Wizara ya Fedha wanahakiki umethaminishwa kama Sh.3,043,626,000 kwa ajili ya kulipa *compensation*. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge uvute subira, uhakiki unafanyika na mara uhakiki ukikamilika fedha hizi zitalipwa kwa wananchi. Kwa hiyo, wananchi wasubiri kulipwa *compensation* yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, swali la nyongeza.

3 APRILI, 2018

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kutambua na kupongeza kazi nzuri ambayo inafanywa katika kuboresha viwanja mbalimbali vya ndege hapa nchini, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa nilizonazo ni kwamba uwanja wa ndege wa Lindi umeshafanyiwa upembuzi na usanifu. Sasa, Serikali iko tayari kuanza kutenga fedha za ndani badala ya kutegemea fedha za nje kwa ajili ya kuanza ukarabati wa uwanja huu wa ndege ikizingatiwa uwanja ulivyokaa kimkakati, lakini historia ya uwanja huu na mahitaji ya uwanja huu kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimjulishet tu Mheshimiwa Mbunge kwamba avute subira wakati wa bajeti ataona kwamba tumeweka fedha za kutosha kupitia mapato ya ndani. Ile asilimia ya fedha ambazo tumetenga kupitia mapato ya ndani ni kubwa. Kwa hiyo, ilikuwa sio vema nizungumze hapa lakini labda kama baadaye tunaweza tukaonana nimwoneshe, lakini wakati wa bajeti tutaonesha namna ambavyo Serikali imedhamiria kuboresha viwanja vyake kupitia mapato ya ndani. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha, swali la nyongeza.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Kanda ya Kusini ni uwanja ambao upo Mtwara Mjini na ule uwanja wa Mtwara Mjini nimekuwa nazungumza sana kwenye Bunge hili kwamba ni uwanja ambao hauruhusu ndege kuweza kutua wakati wa usiku, miaka ya nyuma huko

3 APRILI, 2018

taa zilikuwepo zikaondolewa. Je, mpango wa Serikali wa ahadi inazotoa kila mwaka wa kukarabati na kuweka taa za kuongozea ndege Mtwara Mjini kiwanja hiki cha Kanda ya Kusini utaanza lini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Maftaha kwa kuendelea kufuatilia ujenzi huu wa uwanja wa ndege wa Mtwara. Kikubwa tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni kwamba katika Bajeti ya fedha ya mwaka uliopita kulikuwa kumetengwa fedha, pia katika mwaka huu unaokuja kwa ajili ya kuongeza zile huduma ambazo zilikuwa zimepungua katika uwanja huu tumeweka fedha za kutosha. Kwa hiyo, avute tu subira, nimefika uwanja wa ndege wa Mtwara nimeuona kwanza sasa hivi huduma zinaendelea vizuri, hili zoezi la taa litakamilika tu Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, swalii la nyongeza.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba niilize Serikali, je, ni lini uwanja wa ndege wa Njombe utawekwa lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Njombe ni kati ya viwanja 11 ambavyo viko kwenye utaratibu wa kuboreshwa. Kulikuwa kuna changamoto kidogo pale ya wale majirani kwenye uwanja Mheshimiwa Mbunge anatambua, kuna watu wameendelea kuweka majengo marefu kandokando ya uwanja huo.

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mawazo ya kuuhamisha ule uwanja ili uwe nje ya sehemu hiyo uliopo. Kwa hiyo, zoezi hilo tuliwaachia wataalam waendelee kuliangalia itakapokuwa imekamilika au itakapokuwa imeonesha tofauti basi tutaendelea na hatua ya kuujenga huu uwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu changamoto zilizokuwepo na Mheshimiwa Mbunge tumekuwa tukizungumza nae, lakini nasi tumelichukulia hatua tumewaaagiza wataalam wa upande wa TAA na Mkoa waweze kukaa na kuona kama tutauhamisha huu uwanja basi tusichelewe kuchukua hizo hatua ili tuweze kufanya ujenzi wa uwanja huu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nashawishika kukutajia viwanja vya Wabunge waliosimama hapa kwa sababu muda wetu umekwenda. Naona Mbunge wa Songea uwanja wa Songea, Mbunge wa Ileje kasimama na Singida naona ameshasimama. Mheshimiwa Naibu Waziri naomba uwatazame hawa watu ili bajeti yako itakapofika uwe na majibu ya kuwapa. Waheshimiwa Wabunge naomba tukae, muda wa swali hili umekwenda sana.

Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido sasa aulize swalii lake.

Mheshimiwa Kiruswa naomba utumie *microphone* ya kiti kinachofuata kwa sababu hiyo haisikiki.

Na. 4

#### **Mradi wa Maji kutoka Mto Simba hadi Longido**

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA** aliuliza:-

Upungufu wa maji safi na salama kwa matumizi ya binadamu na mifugo ni moja ya kero kubwa kwa wananchi

3 APRILI, 2018

wa Wilaya ya Longido. Vyanzo vya maji vilivyoko ni vichache na ni vya muda (*seasonal*) na mahali pengine hakuna kabisa:-

(a) Je, utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuleta maji ya bomba kutoka Mto Simba ulioko Siha, Mkoani Kilimanjaro hadi Mji wa Longido kilometra 64 unaogharimu shilingi bilioni 16 umefikia hatua gani?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza usambazaji wa maji hayo ili yawafikie wananchi wapatao 23,000 waishio katika Kata Kimokouwa na Namanga pia Kiserain ambazo zipo umbali wa kuanzia kilometra 15 - 25 tu toka Longido Mjini?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Longido. Mradi huo umegawanyika katika vipande vinne. Utekelezaji wa kipande cha kwanza unagharimu shilingi bilioni 10.89. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa kipande hicho umefikia asilimia 15. Utekelezaji wa kipande cha pili unagharimu shilingi bilioni 2.54.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwezi Machi 2018 utekelezaji wa kipande hicho umefikia asilimia 40. Kipande cha tatu kinagharimu shilingi milioni 276.36. Hadi mwezi Machi 2018 utekelezaji wa kipande hicho umefikia asilimia 90. Kipande cha nne kinahusu ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji katika Mji wa Longido kwa gharama ya shilingi bilioni 2.09 ambapo utekelezaji wa kipande hicho umefikia asilimia 85.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu umesanifiwa kutoa huduma kwa Kata za Longido, Engikaret na Orbomba

3 APRILI, 2018

zenye jumla ya wakazi 16,712 kwa takwimu ya sensa ya watu wa makazi ya mwaka 2012, ambapo Kata ya Longido ina wakazi 2,285; Kata ya Orbomba 7,900; na Engikaret ya wakazi 6,527; na inatazamiwa idadi ya watu ikafika 26,145 kwa Kata zote tatu ifikapo mwaka 2024 kwa ongezeko la asilimia 3.8 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Kata za Kimokouwa, Namanga na Kiserian zitaingizwa katika mpango wa awamu ya pili ya uzambazaji maji baada ya mradi huu kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kabla ya yote nipende kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutupatia mradi huu mkubwa wa kutuletea maji safi na salama kwa ajili ya binadamu na mifugo toka Mlima Kilimanjaro Mto Simba.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa wananchi wa hizi Kata tatu zilizolengwa na mradi huu wana shauku kubwa ya kupata maji haya ikizingatiwa kwamba Wilaya hii ni kame, Je, mradi huu unategemewa kukamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kufahamu uhaba wa maji katika Wilaya ya Longido Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji alipotembelea Longido mwaka jana aliwaahidi wananchi wa Kijiji cha Wosiwosi wanaoishi pembezoni mwa Ziwa Natron lenye maji yasiyofaa kwa matumizi ya binadamu pamoja na wananchi wa Kata ya Tingatinga katika Kijiji cha Tingatinga kwamba atawapatia mabwawa ya maji; je, ahadi hii ataitimiza lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ya kipekee anavyowatetea wananchi wake wa Longido. Kubwa tu itambulike kutokana na changamoto kubwa sana kwa Mji ule wa Longido katika suala zima la maji, Wizara yetu ikaona haja ya kuwapatia wananchi wale maji safi na salama na ya kuwatosheleza, lakini anataka kujua ni lini mradi ule unakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi ule unakamilika mwishoni mwa mwezi Mei. Mimi kama Naibu Waziri nilipata nafasi ya kufika pale katika kuhakikisha tunausukuma mradi ule ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. Nimgakikishie Mheshimiwa Mbunge, nilipofika katika ule utekelezaji wa mradi nimemkuta Mkandarasi amelala, nillimtikisa kwa mujibu wa mkataba ili mwisho wa siku wananchi wake wapate maji. Nataka nimhakikishie tutashirikiana ili wananchi wake waweze kupata maji safi na salama kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ahadi ya Mheshimiwa Waziri ya mabwawa, nataka nimhakikishie ahadi ni deni. Sisi kama Wizara ya Maji kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameahidi tutatekeleza kwa wakati katika kuhakikisha wananchi wake wanapata maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Ngonyani, kwa sababu lazima upande wa Upinzani wapewe nafasi jamani. (*Kicheko*)

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Kambi Mbadala, kwanza niwapongeze Wizara hii ya Maji kwa kufanya kazi vizuri hasa mdogo wangu kwa kubeba ndoo kichwani. Kule Mnyuzi katika Kijiji cha Lusanga kuna mradi mkubwa wa maji ambao upembizi yakinifu umeshafanyika na maji hayo yangeweza kufika mpaka Shamba Kapor; je, mradi huu mpaka sasa hivi umefikia wapi?

3 APRILI, 2018

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. Hata hivyo, nimpongeze Kaka yangu Mheshimiwa Maji Marefu kwa namna anavyowapigania wananchi wake wa Jimbo la Korogwe Vijijini. Nataka nimhakikishie yeye ni jembe wembe!

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa kama alivyokuwa amesema, upembuzi yakinifu umeshakamilika, kubwa nimwombe tu Mhandisi wa Maji wa Korogwe Vijijini asilale. Ahakikishe kwamba anatangaza ile kazi ili mwisho wa siku Mkandarasi apatikane na utekelezaji wa mradi uanze mara moja na Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo katika kuhakikisha tunawapa fedha ili mradi ule ukamiliike kwa wakati. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza niipongeze Serikali kwa mkakati mkubwa inayoweka kuhakikisha wananchi wote kwenye vijiji wanapata maji. Hata hivyo, tukirudi nyuma historia ni kwamba Serikali ilipochimba visima iliachia Kamati za Maji kuendesha visima hivyo. Je, Serikali kwa sababu imejizatiti kupeleka maji kila kata na vijiji, ina mpango gani ya kuchukua wale wanafunzi wenyeweji waliomaliza Kidato cha Nne wakajifunze Chuo cha Maji kwa ajili ya kuja kusimamia visima hivyo ili viweze kutumika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hilo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

3 APRILI, 2018

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, mama yangu, kwa swali zuri, lakini kikubwa na sisi tumepokea ushauri. Tulivyoanzisha miradi ya maji na kuhakikisha wananchi wanapata maji, lakini lazima kuwe na usimamizi, tukaona haja ya kuwashirikisha wananchi katika kuhakikisha kwamba, kunakuwa na jumuiya za watumiaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na nia njema ya kuweka jumuiya ya watumiaji maji, lakini kumekuwa na changamoto za aina yake. Sisi kama Wizara ya Maji tumekuwa na Chuo cha Maji kipo pale Ubungo; ni fursa pia niwahamasishe vijana wenzangu wapate nafasi ya kufika pale na sisi kama Wizara tutaangalia namna ya kuweza kuwasaidia katika kuhakikisha na wao wawe sehemu ya kumilliki miradi ile ya maji. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musa Ntimizi, swali la nyongeza.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini shida ya ya maji Longido ni sawasawa na shida ya maji iliyopo Jimbo la Igala. Maeneo mengi ya Jimbo la Igala maji chini hayapatikani kwa urahisi, visima vingi vimechimbwa lakini havitoi maji na kusababisha kupotea fedha nydingi za Serikali; lakini yako maeneo mengi ambayo yanaweza yakachimbwa mabwawa na yakasaidia upatikanaji wa maji katika Jimbo la Igala.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti umeshafanyika, upembuzi yakinifu na usanifu katika Kata ya Goweko na Igala umeshafanyika, lakini mpaka sasa miradi hii hajafanyika na miradi hii ilikuwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017, lakini mpaka sasa hakuna kinachofanyika. Sasa naomba kujua miradi hii ni lini itatekelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

3 APRILI, 2018

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Moja tu, ukimwona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Sasa mpaka Mheshimiwa Ntimizi analia maana yake Igala kuna hali mbaya sana katika suala zima la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Maji na kwa kuwa, sisi si Wizara ya ukame, tupo tayari kushirikiana nae katika kuhakikisha tunawachimbia mabwawa ili wananchi wake waweze kupata maji kwa wakati. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti.

Na. 5

**Mradi wa Maji wa Kata ya *Old Moshi***

**MHE. MARWA R. CHACHA (K.n.y. MHE. LUCY F. OWENYA)** aliuliza:-

Mradi wa Maji Vijijini katika Kata ya Old Moshi Magharibi katika Kijiji cha Mande haujatekelezwa kuanzia mwaka 2008;

Je, ni sababu zipi zilizosababisha mradi huo kutokamiliika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP I*) Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ilipanga kutekeleza miradi ya maji katika vijiji 12. Kati ya vijiji hivyo ujenzi wa miradi umekamilika katika vijiji sita vya Korini Juu, Korini Kati, Korini Kusini, Kilima Juu, Kilima Kati na Golo na utekelezaji wa miradi iliyobaki unaendelea kufanya katika awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP II*).

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu wa mradi wa maji wa Tela Mande ulikamilika mwaka 2013. Mkandarasi aliyeeteuliwa hakuweza kuanza kazi na ulichelewa kutekelezwa kutokana na ufinyu wa bajeti. Halmashauri ya Wilaya ya Moshi iliutangaza mradi huu katika mwaka wa fedha 2017/2018 na kwa sasa mradi huo upo kwenye hatua ya tathmini (*evaluation*) ili kumpata mkandarasi wa ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uUtekelezaji wa mradi huu unategemea kuanza mwezi Mei, 2018. Mradi huu utakapokamilika utahudumia wakazi 5,141 kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 kwa Viji ya Tela na Mande.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha swali la nyongeza.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa NJaibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, mradi huu umechukua muda mrefu sana. Ukiangalia kwenye swali la msingi ni tangu 2008, lakini ukija kwenye majibu anasema usanifu umekamilika tangu 2013. Pamoja na kwamba Serikali inasema wako kwenye *evaluation* wananchi wa Wilaya ya Moshi na hususan wa Kata ya Tela wanataka kujua, huu mradi umetengewa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika Wilaya ya Serengeti kuna miradi ya maji kwenye Vijiji vya Nyagasense, Rung'abure na Kibanchebanche. Mradi wa Nyagasense hautoi maji na walishalipa *retention* yote. Pia Mradi wa Rung'abure hautoi maji. Mradi wa Kibanchebanche

3 APRILI, 2018

mkandarasi ametokomea na nimemwambia Mheshimiwa Waziri twende Serengeti, hatukwenda mpaka leo, wameshalipa mpaka *retention* lakini miradi haitoi maji. Ni nini tamko la Wizara dhidi ya matatizo haya ambayo yametokea, wamelipwa fedha zote miradi haitoi maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, swalii la nyongeza la kwanza linahitaji takwimu. Kama unazo unaweza kujibu kama huna kikanuni utampa Mheshimiwa Mbunge majibu baadaye, lakini karibu kwa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimjibu swalii kaka yangu Mheshimiwa Marwa Chacha, moja alitaka kujua gharama ya mradi; gharama ya mradi itagharimu kiasi cha milioni mia nane ishirini na mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii lake la pili; kuna baadhi ya miradi ambayo imeshalipwa fedha za Serikali lakini haitoi maji. Nataka nimhakikishie sisi kama Wizara ya Maji na kama viongozi; maana unapokuwa Naibu Waziri, ni jukumu lako kuhakikisha wananchi wanapata maji. Sisi hatutamwonea haya ye yeyote ambaye amefanya ubadhifru wa fedha za Serikali. Kama kweli kuna fedha ambazo kuna mtu amezila, basi ajiandae kuzitapika ili wananchi waweweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swalii la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa hali ya kusuasua kwa huu mradi wa Mande, Tela kunafanana kabisa na miradi mingine iliyo katika maeneo ya tambarare ya Mkoa wa Kilimanjaro, ukiweko ule mradi wa Mwanga mpaka kule Hedaru mpaka Mombo. Ni lini sasa Serikali itatupa muda muafaka wa kukamilika kwa miradi hiyo?

3 APRILI, 2018

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Tunapozungumzia suala la maji, maji hayana mbadala, si kama wali, ukikosa wali eti utakula ugali. Kwa hiyo kuna haja kubwa sana ya kuhakikisha wananchi wanapata maji kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi kama Wizara ya Maji katika kuhakikisha wananchi wanapata maji kwa wakati lazima kuwe na ufuutiliaji na usimamizi wa karibu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara ya Maji tumejjipanga katika kufuatilia na kusimamia miradi hii kwa wakati ili wananchi waweze kupata maji kwa muda muafaka uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Nagu

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Naomba niipongeze Wizara na Serikali kwa kutengea fedha Mradi wa Endasak, Endagao na Endeshwal na Mradi wa Malama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo miradi hii miwili imepangiwa shilingi bilioni 1.31 na bilioni 1.2 mradi wa pili na naishukuru Serikali kwa kuanza kutekeleza mradi, lakini imechukua muda mrefu sana. Naomba kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini kasi itaongezeka ili miradi hii miwili iweze kukamilika kwa sababu Wilaya ya Hanang ilivyo chini ya *Rift Valley* ina ukame na watu wanapata shida kubwa sana ya kutafuta maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi

3 APRILI, 2018

hii lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Mary Nagu, mama yangu kwa namna anavyowapigania wananchi wake. Kubwa ni kwamba sisi kama Wizara ya Maji jukumu letu ni kuwapatia wananchi maji. Zipo changamoto ambazo tumekumbana nazo, moja ni wakandarasi ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa kususasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara tumejipanga kwa mkandarasi ambaye atatushelewesha katika kuhakikisha wananchi wanapata maji, hatuna sababu ya kujadiliana naye, tutamwondo, tutamweka mtu ambaye atawezeku fanya kazi kwa wakati ili wananchi waweze kupata maji kwa muda uliopangwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jaffar Sanya Jussa, Mbunge wa Paje, sasa aulize swali lake. Swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Ussi Pondeza.

Na. 6

**Hitaji la Samani na Gari kwa Vituo vyta Polisi  
Paje na Jambiani**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA (K.n.y. MHE. JAFFAR SANYA JUSSA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itavipatia Vituo vyta Polisi vyta Paje na Jambiani samani za ofisi pamoja na magari kwa ajili ya *patrol?*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaffar Jussa, Mbunge wa Paje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna uhaba wa magari pamoja na samani katika Vituo vyta Polisi vyta Paje

na Jambiani, kama ilivyo kwenye maeneo mengine hapa nchini. Kwa sasa Vituo vya Polisi cha Paje na Jambiani vinapata huduma za doria kutoka kwa *OCDwa* Makunduchi, hali inayosababisha kuwa na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi lipo katika mchakato wa kupokea magari mapya yaliyonunuliwa na Serikali ambayo yatagawawiwa kwa kuzingatia kiwango cha uhalifu, idadi ya watu na ukubwa wa eneo katika kamandi husika. Aidha, Jeshi la Polisi litaendelea kutumia bajeti inayotengwa kutimiza azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa linakuwa na vitendea kazi vya kutosha, ikiwa ni pamoja na magari na samani katika vituo vya Polisi kote nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Tatizo la samani katika vituo vya Zanzibar, zaidi katika Majimbo ya Chwaka, lakini yako katika Wilaya nyingi za Zanzibar yote. Jimboni kwangu kuna Kituo cha Chumbuni ambacho kinahudumia wilaya mbili, Wilaya ya Magharibi na Wilaya ya Mjini, lakini kituo hiki hakina samani, hakina gari, kinahudumia watu zaidi ya 70,000 na kinavuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshalisemea sana suala hili na nimeshaliuliza zaidi ya mara tatu, mara nne na nikaahidiwa kitatengenezwa na huduma zitapatikana, lakini mpaka leo hali iko vile vile. Je, Mheshimiwa Waziri anatuambia nini wananchi wa Chumbuni kuhusu suala letu hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge

kwa kuwa mfuatiliaji sana wa masuala ya jimbo lake na masuala yanayohusu Vituo vy'a Polisi vilivyoko katika Jimbo lake. Amekuja Mara kadhaa akisemea jambo hilo na tulishatuma wataalam wetu wafanye tathmini ili tuweze kujua namna tunavyoweza kulishughulikia. Kwa kuwa tunaelekeea kwenye bajeti niendelee tu kumhakikishia kwamba, punde bajeti inavyoruhusu tutaweka kipaumbele kwenye jambo hilo ambalo amekuja akilisemea mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. Kwa kuwa mwaka 2015 nilipokuwa Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki nilitoa ufadhilli wa gari la golisi kwenye Kituo cha Kata ya Maore kwa ajili ya Jimbo la Same Mashariki; nina uhakika Serikali inalifahamu hilo. Kwa kuwa, lile gari sasa halina matairi, linahitaji kufanyiwa *maintainance* kubwa. Je, Serikali mnatoa ahadi gani leo hapa ili wananchi wa Same Mashariki wasikie?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhesimiwa Mbunge Anne Kilango Malecela kwa kusaidia kazi za Ofisi ya Polisi katika Jimbo la Same Mashariki kuweza kufanya kazi na wanakukumbuka sana. Nimefika mwenyewe Same nimeona wakikukumbuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Serikali inatambua jitihada alizofanya Mheshimiwa Mbunge na tutaongea na Kamanda wa Polisi wa Mkoa ili tuweze kuona namna ambavyo tunaweza tukaunga mkono jitihada hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge ulizifanya. Hata hivyo niendelee kukuomba uendelee kuwakumbuka wananchi wa

3 APRILI, 2018

Same kwani wanakukumbuka sana ili vitu kama vile matairi wasiendelee kuvikosa, waendelee kupata kama ulivyokuwa unafanya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masoud, swali la nyongeza.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kituo cha Polisi cha Kingeja, Jimbo la Mtambire ni kibovu, chakavu na kimekaliwa tangu enzi ya ukoloni. Kumekuwa na ahadi ya Serikali karibu miaka 13 kwamba watakijenga kituo kile, lakini dalili hazioneshi kwamba kuna nia njema ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ituambie ina mkakati gani wa ziada kuhakikisha kwamba, Kituo cha Polisi cha Kingeja kinajengwa sambamba na Kituo cha Polisi cha Mkoani hasa ukizingatia kuna vifaa vy ya Polisi ambavyo tayari vimewekwa katika eneo la Wilaya ya Mkoani ambavyo vinatakiwa viweze kusambazwa. Je, Kituo cha Polisi cha Kingeja...

**NAIBU SPIKA:** Hilo ni swali la pili, Mheshimiwa Masoud. Hii ni nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali ni njema na utaona kwamba, wiki moja iliypita Mheshimiwa Makamu wa Rais alikuwa ziarani kule pamoja na Naibu Waziri. Pia utaona kwamba, wamefanya shughuli kubwa ambayo inahusu ujenzi wa vituo na kazi inaendelea. Kwa hiyo kazi ile inayoendelea itafika pia mpaka Jimboni kwako pamoja na kituo kile ulichokitaja na vituo vingine ambavyo vinahitaji huduma kama hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

3 APRILI, 2018

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, Kituo cha Polisi Makambako ni kituo cha kiwilaya na kwa sababu Makambako ndipo katikati ya kwenda Songea, Mbeya na Iringa; na kwa sababu, Waziri alituahidi kutupatia kitendea kazi cha gari. Je, ahadi yake ya kutupatia gari iko pale pale ili shughuli za kipolisi pale ziweze kufanyika kwa ufanisi mzuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pana uhitaji mkubwa wa gari katika Kituo cha Makambako. Niendelee kusema tu kwamba, Serikali inaendelea kuweka umuhimu mkubwa wa kukipatia gari kituo kilichopo hapo na punde magari yatakapopatikana tutaweka kipaumbele kile kama ambavyo tuliahidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 7

#### **Ongezeko la Ajali za Barabarani Nchini**

**MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza:-

Kumekuwa na idadi kubwa ya ajali nchini zinazosababisha vifo, majeruhi na upotevu wa mali:-

(a) Je, kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia 2016 – 2018 ni ajali ngapi zimetokea na kusababisha vifo au majeruhi?

(b) Je, ni waathirika wangapi waliomba fidia na wangapi mpaka sasa wamelipwa fidia zao kutoka kampuni za bima?

3 APRILI, 2018

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Rose Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2018 Jeshi la Polisi kuitia Kikosi cha Usalama Barabarani lilichukua hatua za makusudi kupunguza ajali ambapo mpaka kufikia Disemba, 2017 limefanikiwa kupunguza ajali za barabarani kwa asilimia 43.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 kulitokea jumla ya ajali 9,856 ambazo zilisababisha vifo 3,256 na majeruhi 2,128. Mwaka 2017 kulitokea ajali 5,310 ambazo zilisababisha vifo 2,533 na majeruhi 5,355 wakati kwa kipindi cha Januari hadi Februari, 2018 zimetokea ajali 769 ambazo zimesababisha vifo 334 na majeruhi 698.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2018 jumla ya waathirika wa ajali 1,583 walilipwa fidia yenye jumla ya thamani ya fedha za kitanzania billioni 7.3 kutoka kampuni mbalimbali za bima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, swalii la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri mimi nilikuwa *very specific* kwenye swalii langu la msingi, nililiza ni watu wangapi walilomba fidia na wangapi wamelipwa mpaka sasa hivi. Kwa maelezo yako Mheshimiwa Waziri inaonesha jumla ya vifo na majeruhi ni zaidi ya elfu 14, hiyo ni kwa mwaka 2016 mpaka 2018 na ambao wamelipwa fidia mpaka sasa hivi ni watu 1,583, ni kama asilimia zaidi ya 10 kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa mwaka 2009 Bunge lilipitisha Sheria namba 10 ili kuwalinda waathirika wa ajali hizo. Sasa Mheshimiwa Waziri hawa wenzetu ambao

3 APRILI, 2018

wanaoshughulikia hili suala la bima hawa wenzetu wa *TIRA* (*Tanzania Insurance Regulatory Authority*) inaonesha kabisa kuna upungufu. Ambao wamekuwa *beneficiary* wakubwa wa hii *issue* ya bima ni hizi kampuni ambazo yanakatisha bima, lakini ajali inapotokea inaonesha kabisa Watanzania wamekuwa ni waathirika wakubwa ambao wameachiwa mzigo mkubwa. Sasa Mheshimiwa Waziri huoni ni wakati muafaka sasa tuanzishe idara maalum ambayo itakuwa inatoa elimu kwa Watanzania pale ajali inapotokea ili wajue hatua stahiki ambazo wanatakiwa kuchukua ili walipwe fidia zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rose Tweve kwa *ku-take serious concern* ya Watanzania wanaopata matatizo hayo na kutokupata fidia ama kuchelewa kupata fidia. Niseme tu kama Serikali tunapokea wazo lake na kwa sababu tuna wataalam wazo hilo litachambuliwa kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa Watanzania kuchukua hatua haraka za kufuata taratibu zinazotakiwa badala ya utaratibu ambao maeneo mengi wamekuwa wakifanya panapotokea matatizo ya aina hiyo; kuamua kuchukua sheria mikononi ama kuamua kufanya taratibu za njia za mkato ambazo zinasababisha wao kukosa kile ambacho walitakiwa wapate.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa hizi ajali za barabarani zinatokana na uzembe wa baadhi ya madereva na baadhi ya madereva

kutumia simu wakati wakiwa wanatumia vyombo ya moto. Je, Serikali ina mkakati gani wa kurekebisha Sheria ya Usalama Barabarani ili kuwachukulia hatua kali zaidi hawa madereva ambao wamekuwa wakitumia simu wakati wakitumia vyombo nya moto? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli kuna kiwango kikubwa cha ajali zinatoka kutokana na uzembe. Ukiangalia hata kwenye kumbukumbu zaidi takribani ya matukio zaidi ya 1,500 yanatokana na uzembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kile alichokisema cha kurekebisha sheria na kuchukua hatua tunaendelea na utaratibu huo na tunasema tunakokwenda tutaanza hata kutumia taratibu ambazo nchi zingine wanatumia kwa *count down* dereva ambaye anapatikana sana na makosa aweze kukosa sifa za kuendelea kumiliki leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunalifanyia kazi wazo lake na nimpongeze sana kwa kuguswa na jambo hili kwa sababu limekuwa likisababisha hasara sana kwa familia na kwa Taifa. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga, swali la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Swali langu ni hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali zinaendelea kutokea kwa wingi, hata hivi sasa hivi ninavyoongea ukipita barabara ya Morogoro – Dodoma kuna ajali nyingi sana, lakini *traffic* wamegeuka *agent* wa TRA kazi yao ni kusimamisha magari na kutoza faini. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba atoe tamko kuanzia leo hii matrafiki waache kutoza faini wakazane na

3 APRILI, 2018

kutoa elimu kwa kutoa elimu kwa watumia vyombo nya moto na wasafiri ili wajue ni haki gani watapata pindi ajali zinapotokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja, sisi kama Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Polisi, kutoza faini ama kukusanya faini si kipaumbele chetu; sisi kipaumbele chetu ni maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa imepita miaka mingi sana ya kutoa elimu na tunaendelea kuona kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alisema uzembe bado uko mwingi sana ndipo tunapokwenda kwenye hatua hiyo ya kutoza faini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama Watanzania watazingatia kwamba wamebeba dhamana kubwa ya maisha ya Watanzania na maisha yao wao wenyewe, wakawa waangalifu hili suala la faini litakuwa limeisha, lakini kwa kuwa tunawapenda zaidi na tunapenda zaidi maisha yao ndio maana tunakuwa hatuna njia nyingi zaidi ya kuchukua sheria kali ili kuweza kuokoa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitoe rai kwa Jeshi la Polisi kuendelea kuwa *strictly*, kuendelea kuwa wakali punde watu wanapofanya mzaha na huku wakiwa wamebeba abiria ili kuweza kuokoa maisha yanayopotea kutokana na ajali nyingi zinazotokea barabarani. Jambo hili ninalolisemea ni kwa vyombo nya moto vyote, ukianzia magari ambayo si ya abiria pamoja na bodaboda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisitiza sana hili kwa sababu tumeshuhudia vifo vikiwa vimetokea na pale tunapokwenda kwenye kuokoa miili tunakuta watu walikuwa tayari walishaandikiwa faini ikiwa ni kwamba wameambiwa

3 APRILI, 2018

kwamba wanakwenda mwendo kasi. Hata hivyo, pamoja na faini wanaendelea na mwendo kasi ama na uzembe na baadaye inagharimu maisha ya Watanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venance Mwamoto, swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuuliza swali. Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa askari katika baadhi ya sehemu na askari wengi sana kwa maana ya *traffic* wako barabaran, je, Serikali sasa haioni imefikia wakati wa kuweza kupata kamera au teknolojia nyingine badala ya kutumia askari ambao kwa kweli utendaji wao hauna tija. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mwamoto kwa jambo hilo alilolitoa. Ni kweli kuna uhitaji mkubwa sana wa kuhamia kwenye teknolojia, nchi nyingi zilizoendelea ndio utaratibu unaotumika. Sisi kama Serikali wataalam wanaendelea kufanya kazi jambo hilo ikiwepo na kufanya upembuzi yakinifu ili kuweza kujua mahitaji pamoja na maeneo ambayo tunaweza tukaanza nayo ili kuweza kupunguza adha inayojitokeza; kwa sababu kwanza tu kukaa kwenye jua kukaa kwenye mvua pamoja na uchache wa askari inasababisha ufanisi kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo lake hilo tunalifanya kazi na nimpongeze sana kwa kuleta hoja hiyo makini, lakini nimpe pole tu kwa yeye ni ndugu yangu kwa yale yaliyotokea Jumamosi, yaliyotokea tarehe moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mbunge wa Mgogoni, sasa aulize swali lake.

3 APRILI, 2018

Na. 8

**Jeshi la Polisi Kukamata Watu Pasipo Ushahidi Zanzibar**

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF aliuliza:-**

Kuna ushahidi wa kutosha kwamba kuna watu kadhaa ambao wamekuwa wakikamatwa na Jeshi la Polisi Unguja na Pemba huku baadhi yao wakifunguliwa mashtaka na wengine kuachiwa:-

(a) Je, ni kwa nini Jeshi la Polisi linashindwa kufanya kazi kwa weledi na kukamata watu pasipo ushahidi kwa lengo la kukomoa tu?

(b) Ili kulisafisha Jeshi la Polisi, je, Serikali haioni haja ya kuwawajibisha watendaji ambao wenyewe tabia ya kuwakomoa wananchi kwa kuwakamata pasipo ushahidi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mbunge wa Mgogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi ni chombo kilichoundwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria na linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba na Sheria na kanuni na taratibu zilizopo, jukumu lake kuu likiwa ni kulinda usalama wa raia na mali zao. Jeshi la Polisi limepewa mamlaka ya kisheria ya kukamata, kuhoji na kuweka watuhumiwa mahabusu kwa muda ulioruhusiwa kisheria endapo itabainika kuwa kuna viashiria au taarifa ya kuhusika katika kutenda kosa la jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria na kanuni na taratibu za utendaji zinazoongoza Jeshi la Polisi linapobainika askari amebambika kesi kwa sababu zozote zile huchukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu ikiwamo kufukuzwa kazi.

3 APRILI, 2018

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Naibu wa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Katika jawabu la msingi la Mheshimiwa Waziri amesema Jeshi la Polisi limepeewa mamlaka kisheria kutuhumu, kukamata, kuhoji na kuweka watuhumiwa mahabusu kwa muda ulioruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako watu wengi ambao wanawekwa mahabusu ya polisi kwa zaidi ya siku 15, akiwemo mwanafunzi Abdul Nondo, ambao wanawekwa mahabusu ya polisi kwa zaidi ya siku 15 bila ya kupelekwa mahakamani. Nataka njue ni sheria gani ambayo inatumika au inatumiwa na polisi kuwaweka watu mahabusu ya polisi kwa muda huo mrefu bila ya kuapeleka mahakamani? Nataka kujua sheria ni sheria gani. Swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni hatua gani ambayo Mheshimiwa Waziri ataichukua iwapo tutamletea orodha ya watu ambao wamebambikiziwa kesi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema jeshi la polisi linafanya kazi kwa mujibu wa sheria na katika ufanyaji kazi wake kuna hatua mbalimbali za kuchukua ikiwemo kufanya upelelezi, kufanya mahojiano na baadaye mambo yote yale yakikamilika hatua nyingine ndipo huwa zinafuatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jambo la usalama ni kipaumbele, usalama wa mtuhumiwa lakini na usalama wa raia wengine wanaosalia, Jeshi la Polisi hutumia wajibu wake lililopewa wa kulinda usalama wa raia kuweza kuhakikisha kwamba linatimiza majukumu yake na huku watu wakiwa salama pamoja na mali zao.

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu jambo la pili, kwa kuwa ni suala la takwimu nitamwomba Mheshimiwa Mbunge niweze kuwasiliana naye kuweza kumpa masuala yale ya takwimu na yeye kama ana orodha kuweza kubadilishana orodha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haji.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni muda gani kisheria jeshi la polisi linaposhindwa kupeleka ushahidi wa kesi unaopeleka mahakamani naweza kupeleka maombi ya kuondoa mashitaka hayo mahakamani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu ndugu yangu Khatib wa kutoka kwetu kule kwa mama, kwamba makosa ya jinai hayana ukomo kwa hiyo, inategemea kosa analolisemea ambalo anaweza akasubiria na akaenda kuomba liondolewe ni aina gani ya makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo kama makosa ni yale ambayo shitaka lake halina ukomo, basi ni vyema kuacha vyombo vingine ambavyo vinatoa hukumu vikatoa hukumu ndipo yeye akatambua kwamba jambo hilo limeshafika ukomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutamalizia na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha kwa niaba yake.

3 APRILI, 2018

Na. 9

**Kuwapa Kipaumbele Wananchi Wanaosambuliwa  
Mashamba yao na Tembo**

**MHE. MARWA R. CHACHA (K.n.y. MHE. JOYCE B.  
SOKOMBI)** aliuliza:-

Katika Msimu wa mwaka 2017/2018, wananchi wa Wilaya ya Serengeti na Bunda wanaoishi kandokando ya Mbuga ya Serengeti wameathirika sana kwa mashamba yao kushambuliwa na tembo na hivyo kukumbwa na baa la njaa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuyafanya maeneo hayo kuwa kipaumbele cha kuwapa msaada wa chakula?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) mnamo mwezi Mei, 2017 ilichukua hatua madhubuti ya kupeleka mahindi kiasi cha tani 400 kwa Wilaya ya Serengeti na tani 253.6 kwa Wilaya ya Bunda na kuyauza kwa bei nafuu kwa wananchi walioathiriwa na ukame pamoja na uharibifu wa mazao uliosababishwa na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua stahiki na za haraka za kukabiliana na upungufu wa chakula katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo Wilaya ya Serengeti na Bunda. Aidha, Wizara ya Kilimo itashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuweka mkakati wa pamoja wa kudhibiti tembo wanaoharibu mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali mnamo mwezi Mei, 2018 kuititia Wizara ya Kilimo ikishirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Taifa ya Takwimu itafanya tathimini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2017/2018 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2018/2019 (*Preliminary Food Crop Production Forecast*) katika Wilaya zote nchini ikiwemo Wilaya ya Serengeti na Bunda ili kujua hali ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine Wilaya ya Serengeti na Bunda zimekuwa zikifanya tathmini za athari za uharibifu wa mazao unaosababishwa na tembo mara unapojitokeza ili kubaini ukubwa wa tatizo na idadi ya wakulima walioathirika. Taarifa za tathmini hizo huwasilishwa Wizara ya Maliasili na Utalii ambapo wakulima waliobainika kuathiriwa hulipwa kifuta jasho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine matokeo ya tathmini hii yataainisha Wilaya zenye viashiria vinavyopelekea uwepo wa upungufu wa chakula kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya uharibifu wa mazao unaosababishwa na wanyampori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa upatikanaji wa chakula katika maeneo yatakayobainishwa kuwa na viashiria vya upungufu wa chakula na kuchukua hatua stahiki ikiwamo ya kufanya tathmini ya kina ya chakula na lishe (*Comprehensive Food and Nutrition Security Vulnerability Assessment*).

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya kina itaainisha hali halisi ya upatikanaji wa chakula, idadi ya watu walioathirika, viwango vya athari, kipindi cha athari, sababu zilizosababisha na hatua stahiki za kuchukuliwa na Serikali na wadau wengine katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Lengo ni kuhakikisha uwepo wa hali endelevu na ya utengemano wa hali ya usalama wa chakula na lishe nchini.

3 APRILI, 2018

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chacha, swali la nyongeza.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, baada ya kupata janga la tembo kuharibu mazao ya wananchi wa Serengeti na Bunda nilimwombwa chakula, kwa kweli tulipata mahindi nimshukuru sana. Nina maswali mawili ya nyongeza lakini kimsingi swali hili lilikuwa lijibiwe na Wizara ya Maliasili na Utalii. Sasa kwa kuwa Serikali ni moja naomba niulize maswali yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016, baada ya tembo kuharibu mazao sana na kupiga kelele hapa Bungeni ikaonekana hatua haichukuliwi nilimwandikia Spika wa Bunge barua dhidi ya madhara na hatua ambayo wananchi walikuwa wameamua kuichukua. Mheshimiwa Spika akamwandikia Waziri wa Maliasili na Utalii aliyeuwepo, Mheshimiwa Maghembe ambaye tuliondoka naye kwenda naye Serengeti akaona madhara makubwa na akakabidhiwa tathmini ya uharibifu wa mazao na mauaji ambayo yameyosababishwa na tembo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa, hizo barua kama zilielekea kwa Spika, nyingine kwa Mheshimiwa Waziri unayesema wa Maliasili, maswali unataka kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, naomba ujikite kwenye swali la msingi uliza maswali yako nyongeza ili na yeye aweze kupata kujibu kwa kikamilifu.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazao na mauaji hauwezi ukaisha mwezi mtu hajauawa na tembo. Mashamba yanaharibowi kwa kiasi kikubwa na Serikali ilishaahidi kuweka uzio au *fence* kuzunguka makazi ya wananchi, sasa miaka mitano inaelekea kwisha hakuna hatua yoyote, hakuna chochote kilichofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaweka mpaka fedha kwenye bajeti yake kuweka *game posts* kwenye

3 APRILI, 2018

maeneo ya makazi ya wananchi ili kuzuia tembo, lakini mpaka leo hakuna chochote kilichofanyika. Nini tamko la Serikali dhidi ya uharibifu unaosababishwa na tembo kwenye mazao ya chakula na mauaji ya wananchi wa Serengeti, Bunda na Tarime na maeneo mengine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo naomba usubiri ajibu mwenye tembo wake. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili ya Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri ambalo ameliuliza. Ni kweli kabisa kumekuwa na matatizo katika maeneo mengi na hilo eneo alilolisema ni mojawapo ya maeneo ambayo kumekuwa na tatizo sana la tembo kuvamia katika mashamba ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi uliopita tarehe 29 na tarehe 30 tulipeleka Maafisa wetu kwenda kufanya tathmini katika yale maeneo ili kuangalia uharibifu mkubwa ambao umefanyika na ili tuone ni hatua gani ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili suala ambalo amesema kwamba tuna mpango wa kuweka uzio, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali bado inafanya jitihada kuhakikisha kwamba tunachukua hatua za tahadhari na kuona ni nini kifanyike katika kuweza kuhakikisha kwamba tunawalinda wananchi wale ambao wanazunguka hifadhi zetu. Kwa hiyo, tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake dogo la nyongeza, lakini kwa niaba pia ya

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa pongezi alizozitoa naomba nizipokee. Vile vile naomba pia niongezee katika majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili amejibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la nyongeza kwa sababu linahusu wakulima, mazao na chakula naomba niseme kabisa kwamba sisi kama Wizara ya Kilimo kwa vile inahusu wakulima na mazao, basi tutashirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, vile vile na Ofisi ya Maliasili na Utalii kuhakikisha kwamba tunahakikisha wakulima wetu wanapewa stahiki zao zinazostahili ili tatizo hili lisiweze kujitokeza tena. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Swali langu la nyongeza lilikuwa ni hilo aliloliongelea Mheshimiwa Ryoba, labda swali (b), kutokana na hizo posho kusuasua na wananchi wanakuwa hawazipati kwa muda, ni lini sasa Serikali itakaa na wale wananchi ili kuongea nao au kuwapa uhakika wa kuwapa hizo fidia kwa muda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naona Mheshimiwa wa fidia amesimama, ama wewe jibu kwanza halafu ataendelea Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali moja dogo la nyongeza la Mheshimiwa mdogo wangu Agnes Marwa na wifi yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sisi Wizara ya Kilimo kama nilivyosema kwenye jibu langu lile la nyongeza, ni kwamba hatuwezi tukafanya Wizara ya Kilimo peke yetu sisi kama Wizara ya Kilimo kwa sababu inawahusu wakulima kwa sababu hii inahusisha Wizara tatu; Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii.

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ningependa kuwaasa Maafisa Kilimo wetu, Maafisa Ugani wetu kule kwenye halmashauri wajaribu ku-review zile posho na viwango vya posho ambavyo huwa wanavifanyia tathmini kwa wakulima wetu kabla hawajapeleka Wizara ya Maliasili na Utalii ili wakulima hawa waweze kupata haki zao stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongezea majibu kwa yale Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo ameyajibu vizuri sana. Basi katika hili suala ambalo nimelisema Wizara ya Maliasili na Utalii sasa hivi inafanya mapitio ya zile kanuni zetu za kifuta jasho za mwaka 2011 ambazo ndizo zinaongoza namna ya kutoa kifuta jasho, si fidia kama inavyosomeka, ni kifuta jasho kwa wale wananchi ambao wameathirika. Kwa hiyo, baada ya hizi taratibu kukamilika basi mambo yatakuwa yamekwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu hili suala lake kwamba ni lini watalipwa, kama nilivyosema katika jibu langu la kwanza kwamba tarehe 29 na tarehe 30 mwezi uliopita maafisa wetu wameshakwenda kufanya tathmini. Baada ya tathmini hiyo kukamilika basi taratibu za kuwalipa hao wote walioathirika zitafanyika mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dokta Raphael Chegeni, swali la mwisho.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Suala la tembo pamoja na uharibifu wake ni suala zito sana. Linaongelewa hapa kwa juu juu lakini madhara yake ni makubwa sana kwa wananchi na hasa wanaozunguka maeneo hayo. Je, unaposema mapitio ya kanuni, ni lini sasa yatakuwa tayari? Swali hilo tu kwa sababu wananchi wana shida kubwa sana.

3 APRILI, 2018

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba sasa hivi tuko kwenye hatua ya mwisho ya kupitia hizi kanuni upya ili angalau kuweza kuvipitia hivi viwango vyote ambavyo vimekamilika. Kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka huu hautakwisha hizi kanuni zitakuwa zimeshakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Kabla sijaleta matangazo tuliyonayo mezani leo na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza Wabunge wapya walioapishwa leo na niwatakile kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yenu. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni waliotufikia leo na tutaanza na wageni walioko jukwaa la Spika. Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa January Makamba ambaye ni Waziri Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, hawa wanaongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Mhandisi Joseph Malongo. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Dokta Harrison Mwakyembe ambao ni viongozi wa kundi la *STARTIMES* la nchini wakiongozwa na Rais wa kundi hilo Ndugu Pang Xin Xing. Aidha ujumbe huu umeambatana na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji – *TBC* Dkt. Ayoub Ryoba. Karibuni sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge *STARTIMES* ndiyo Kampuni iliyosaidia *TBC* kuanza kutangaza ama kurusha matangazo yake kidigitali kutoka kwenye analogia, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni ambao wamekaa kwenye majukwaa ambayo wanakaa wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

3 APRILI, 2018

Tunao wageni 44 wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel ambao ni viongozi na wanachama wa CCM na familia yake kutoka Wilayani Siha. Karibuni sana wageni wetu. Hawa wameongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Siha Ndgugu Wilfred Mossi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni 33 wa Mheshimiwa Maulid Said Mtulia ambao ni viongozi na wanachama wa CCM na familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana na hawa pia wameongozwa na Naibu Meya wa Kinondoni, Mheshimiwa Gere Mangalu Manyama. Karibuni sana (*Makofi na vigelegele*)

Tunao pia wageni 39 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wana maombi kutoka Mkoa wa Dodoma; karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine linatoka Utawala. Waheshimiwa Wabunge mnataarifiwa kwamba leo kutakuwa na kikao cha *briefing* saa 10 kamili Ukumbi wa Msekwa; siku ya leo tarehe tatu mwezi wa Nne tutakutana Wabunge wote kwenye mkutano wetu wa *briefing*.

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo lingine linatoka kwa Katibu Msaidizi wa Wabunge wa CCM, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kuwa kutakuwa na kikao cha Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi hivyo Waheshimiwa Wabunge wote wanaotokana na chama hiki wanaombwa kukutana Ukumbi wa *White House* mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge. Kwa hiyo, tukahirisha shughuli za Bunge Waheshimiwa Wabunge wanaohusika waelekee *White House*.

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni Mwenyekiti wa ibada *Chapel* ya Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria ibada katika Ukumbi wa Pius Msekwa *Chapel/Ghorofa* ya pili, leo siku ya Jumanne tarehe 3 Aprili, 2018 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana.

3 APRILI, 2018

Sasa haya matangazo mawili nadhani Mheshimiwa Anna Lupembe awasiliane na Uongozi wa CCM kuona namna gani watagawana huo muda wa hivyo vikao.

Waheshimiwa Wabunge hilo ndio lilikuwa tangazo letu la mwisho tutaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo!

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naib Spika, mwongozo wa Spika.

## **MWONGOZO**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuomba mwongozo. Nimesimama hapa kwa kanuni ya 68 ila kutokana na muda naomba nisii some.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipoingia hapa asubuhi ya leo shughuli yetu ilianza na Wimbo wa Taifa amba si mara moja huwa tunaanza na tukifunga Bunge tunamaliza na Wimbo wa Taifa. Hata hivyo, Wimbo wa Taifa amba mara zote tumekuwa tukiimba ndani ya Bunge lako Tukufu sio ule wimbo amba ulikuwa wimbo rasmi uliokubalika na *BAMUTA* miaka ile ya zamani kabla ya kuwa *BASATA* kwa sababu una makosa makubwa matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, una kosa la kimelodia kwenye neno na watoto, kuna kosa la *rhythm* kwenye neno la kwanza la Mungu halafu kuna kosa la *wording*. Sasa shaka yangu ni kwamba huu wimbo tunaoimba sasa ni *remix* sijui umekuja katika mazingira gani. Sasa naomba mwongozo wako hivi ni sawa sawa sisi kuimba wimbo amba si rasmi ndani ya Bunge lako Tukufu?

3 APRILI, 2018

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kikao chako cha Bunge kiwe halali inatakiwa itimie nusu ya idadi ya Wabunge wa Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hesabu yangu ya haraka haraka nimehesabu nimekuta Wabunge hawajafikia nusu ya idadi ya Bunge. Mwongozo wangu ni huu; je, kikao chako hiki tuliyoyafanya haya kama hesabu yangu ni ya kweli, tuliyoyafanya haya ni halali ikiwemo viapo vya Wabunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni hatua gani itachukuliwa dhidi ya wale wabunge ambao hawapo kwa wakati huu Bungeni wakati walitakiwa wawepo kwa sababu wamechaguliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kama kikao hiki si halali viperi kuhusu posho tutalipwa au la?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo miwili. Kwanza mwongozo nimeombwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda kuhusu Wimbo wa Taifa unaoimbwa hapa Bungeni na kama wimbo huo ni rasmi ama si rasmi japokuwa kwa maelezo yake yeye ametoa maelezo kwa kirefu kuonesha namna ambavyo wimbo huu si wimbo ule ambao ni rasmi kama ambavyo tunaufahamu na ambao ulikuwa umeshakubaliwa na vyombo vinavyohusika.

Waheshimiwa Wabunge, ili niweze kutoa mwongozo ulio kamili ni lazima nijiridhishe na haya maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Sixtus Mapunda kama ni kweli yamekosewa ama hayajakosewa. Wakati huo huo nitakapoyasikiliza maneno hayo, yale nitakayoyakuta pengine hayako sawasawa nitatoa mwongozo huo hapa Bungeni maana wimbo sisi kama Bunge tunapaswa kuimba

wimbo ulio rasmi. Kwa hiyo, kama kutakuwa na makosa nitatoa mwongozo hapo baadaye.

Waheshimiwa Wabunge pia nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Goodluck Mlinga akizungumzia akidi ya kikao hiki cha Bunge, japokuwa hakutaja ni kanuni gani, yeye amesema tu kikanuni wanatakiwa kuwa nusu, lakini kanuni inayotuongoza kwa ujumla wake kuhusu akidi ni kanuni ya 77. Fasili ya kwanza ukisoma mpaka ya tano inakupa mwelekeo wa namna gani utasema kwamba shughuli hii ni halali ama si halali kwa kutumia akidi.

Hata hivyo, kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge kwanza Mheshimiwa Mbunge anapaswa kusimama na kusema akidi haijatimia. Akisema akidi haijatimia mimi naagiza kwamba hesabu zifanywe, Wabunge Wahesabiwe, si Mbunge anayefanya kazi ya kuhesabu Wabunge wako wangapi.

Kwa hivyo alipaswa anieleze mimi kwamba akidi haijatimia kwa ajili ya jambo lililo mbele yetu. Kwa sababu ukizisoma hizi kanuni kwa ujumla wake akidi si moja kwa kila jambo linalofanyika hapa ndani. Kwa hivyo unasema neno akidi kulingana na jambo lililo mbele yetu ili sisi tujiridhishe kwamba kwenye hili jambo tunalotaka kulifanya je akidi imetimia ama haijatimia ndiyo kanuni zetu kwa ujumla.

Hata hivyo, kwenye suala la hesabu alizofanya yeye na kuonesha kwamba Wabunge hawajafikia nusu suala la akidi kuulizwa kwa yeye, kwa sababu ameulizia kwa ujumla wake suala la akidi ni wakati wa kuanza kikao. Kwa hiyo Mheshimiwa Goodluck kama amezipata taarifa kutoka Ofisi ya Katibu kwamba wakati tukianza asubuhi kulikuwa hakuna akidi, hiyo ndiyo taarifa ninayoweza kuisikiliza, lakini taarifa anayoitoa sasa ama mwongozo anaohitaji sasa hauko kikanuni.

Kwa hivyo swali lake, kwa sababu amezungumzia mambo matatu; la kwanza amesema ikiwa nusu ya Wabunge hawakuwepo wakati tukianza, kwa hivyo sasa

3 APRILI, 2018

hata yale mambo ambayo tumefanya ikiwa ni pamoja na kuapisha, kuapisha kumeapishwa kihalali kabisa. Mheshimiwa Mbunge alipaswa afuate kanuni inayozungumzia akidi wakati huo, wakati tunafanya hayo maamuzi, wakati tunafanya tukio hilo.

Pia amesema hatua gani zitachukuliwa kwa Wabunge ambao hawapo. Nadhani ufanuzi wa mambo haya tulishawahai kuutoa kwa kirefu sana huko nyuma sina sababu ya kurudia kwa sababu Wabunge wakiwa hawapo hapa Bungeni kuna mambo mengi. Wengine wanaweza kuwa wako kwenye Kamati, ama wana kazi maalum waliyopewa. Sasa Mheshimiwa Mbunge hajaeleza vizuri kwa sababu sisi tunapochukua taarifa za Wabunge waliohudhuria tunataka kwanza kujiridhisha kwenye hilo suala la akidi lakini pia kujua kwamba wabunge wetu wako wapi. Kwa hiyo, Wabunge kama wamepewa majukumu mengine wanaweza kuwa nje ya ukumbi huu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge amesema pia kuhusu je, posho italipwa? Posho inalipwa kwa Wabunge waliohudhuria na kukaa hapa kufanya kazi. Kama mtu amehudhuria akaondoka zake huyo kanuni na maamuzi ambayo tulishatoa huko nyuma yatafanya kazi yake. Kwa hiyo, kama ameingia hapa ndani akajiandikisha na kuondoka utaratibu ni uleule kwamba hatolipwa hiyo posho inayoulizwa na Mheshimiwa Mlinga.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge tutaendelea. Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

#### **UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kazi ama majukumu tulionayo leo pamoja na mambo mengine tunalazimika kufanya uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge na nitatoa maelezo ya Mheshimiwa Spika kuhusu uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kama inavyoonekana kwenye *Order Paper*, moja ya shughuli za leo ni uchaguzi wa Wenyeviti watatu wa Bunge kufuatia kuanza kwa kipindi cha pili cha maisha ya Bunge kwani hili ni Bunge la Kumi na Moja. Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Bunge imeweka uwepo wa Wenyeviti watatu wa Bunge ambao wanapatikana kwa kuchaguliwa na Wabunge.

Aidha, Kanuni ya 7(2) ikisomwa pamoja na Kanuni 11(1)(a) ya Kanuni za Bunge imeweka utaratibu utakaofuatwa katika kufikia upatikanaji wa Wenyeviti wa Bunge kwamba Kamati ya Uongozi itapendekeza majina ya Wabunge sita ambayo yatawasilishwa Bungeni ili kupigiwa kura kutoka miongoni mwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumatano tarehe 28 Machi, 2018 Kamati ya Uongozi ilikutana pamoja na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge ili kuyapata majina sita ya kuwasilisha Bungeni ili yapigiwe kura. Hata hivyo, kwa kuzingatia utendaji kazi wa wenyeviti watatu waliokuwepo wakati wa kipindi cha kwanza cha maisha ya Bunge hili na kwa mujibu wa Kanuni ya 11(2) inayotoa fursa kwa Wenyeviti wa awali kuchaguliwa tena katika kipindi cha pili. Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwa kauli moja walifikia uamuzi wa kupendekeza majina matatu badala ya sita ili yaweze kuwasilishwa Bungeni na Bunge liombwe kuyathibitisha kama yalivyokubaliwa na Kamati ya Uongozi.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka pia kuwa Bunge letu lilikwishaweka utaratibu kwamba katika chaguzi zinazofanyika hapa Bungeni iwapo idadi ya wagombea inalingana na nafasi zilizopo na vigezo vinavyohitajika vimetimizwa basi wagombea hao wanapita bila kupingwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu kama huu ulitumika kwenye uchaguzi wa Wenyeviti katika kipindi cha pili cha maisha ya Bunge la Kumi mwaka 2013 ambapo Kamati ya Uongozi ilipendekeza majina matatu ya

3 APRILI, 2018

waliokuwa Wenyeviti kuwa waendelee na nafasi hizo na Bunge likaridhia. (*Makofi*)

Hivyo kwa kuzingatia utaratibu huo, nawasilisha majina ya Wabunge waliopendekezwa na Kamati ya Uongozi ambaao ni Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga ili yathibitishwe na Bunge kwa njia ya kuhoji badala ya utaratibu wa kupiga kura. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo sasa naomba kulihoji Bunge kuridhia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga wathibitishwe kuwa Wenyeviti wa Bunge.

*(Hoja Iilitolewa lamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliridhia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu,  
Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Najma  
Murtaza Giga kuwa Wenyeviti wa Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kuwatangaza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga kuwa ndio Wenyeviti wa Bunge kuanzia sasa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wenyeviti wetu wa Bunge kwa kupata uthibitisho huo wa Bunge na niwatakie kila kheri katika utendaji wenu wa kazi wa kumsaidia Mheshimiwa Spika katika majukumu yake. Naamini mtaendelea kutoa ushirikiano kama ambavyo mmekuwa mkifanya hivyo siku zote mpaka Bunge limeonesha kuwa na imani na ninyi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada kusema hayo, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

3 APRILI, 2018

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (*The Paris Agreement under the UN Framework Convention on Climate Change*)**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kutupatia fursa ya kuwasilisha hili Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi. Pia napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kupitia Rasimu ya Azimio hili na kuipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wadau wote wa mazingira kwa kushirikiana na Ofisi yetu katika jithada mbalimbali za kuboresha Azimio hili, lakini na ushiriki wetu kwenye mkataba. Pia niwashukuru wataalam katika Ofisi ya Makamu wa Rais wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, *Engineer Joseph Kizito Malongo* kwa kazi nzuri waliyofanya ya maandalizi ya Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha Azimio hili, napenda niwasilishe maelezo mafupi ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu Mkutano wa Kimataifa kuhusu Binadamu na Mazingira ulifanyika huko Stockholm, Sweden mwaka 1972. Katika mkutano huo kwa mara ya kwanza kabisa Jumuiya ya Kimataifa ilikubaliana kwamba masuala ya mazingira na maendeleo yanafungamana na kwamba lazima yaende sambamba. Aidha, mwanzoni mwa miaka ya 1980 wanasyansi na wafuatilaji wa hali ya hewa duniani walianza kuona na kutoa taarifa kuhusu kuongezeka kwa joto duniani kuanzia kipindi cha mapinduzi ya viwanda.

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia angalizo hilo la kuongezeka kwa joto duniani, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira Duniani (*UNEP*) kwa kushirikiana na Shirika la Hali ya Hewa Duniani walipitisha uamuzi wa kuunda jopo la kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Lengo la jopo hilo ilikuwa ni kujadili matokeo ya uchunguzi wa kisayansi kuhusu sababu halisi za ongezeko la joto duniani ambalo lilonekana kubadilisha mifumo ya hali ya hewa na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya kwanza ya jopo hilo ilitolewa mwaka 1990 na kuwasilishwa mbele ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa (*United Nations General Assembly*) na kujadiliwa. Majadiliano hayo ndio yalizaa majadiliano ya kuunda Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi. Kwa hiyo, mwaka 1992 Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi ulipitishwa huko Rio De Janeiro, Brazil wakati wa Mkutano huo.

Naomba nirudia hapo, tarehe 5 Mei, 1992 Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi ulipitishwa huko Brazil wakati wa Mkutano wa Dunia kuhusu Mazingira na Maendeleo (*Earth Summit*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania iliridhia mkataba huo wa mwaka 1992 mwaka 1996 na Itifaki yake ya Kyoto mwaka 2002. Lengo la mkataba huo ilikuwa ni kuzuia ongezeko la gesijoto na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mifumo ya ikolojia ya dunia ili kuharakisha maendeleo endelevu duniani. Mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko katika mifumo ya hali ya hewa yanayosababisha na ongezeko la joto duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kuongezeka kwa gesijoto ni kutokana na matumizi makubwa ya nishati chafuzi kwa shughuli za maendeleo zilizofanyika katika nchi zilizoendelea takribani miaka 150 iliyopita. Athari zitokanazo na mabadiliko hayo ni pamoja na ukame, mafuriko, kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza, kumezwa kwa visiwa vidogo kwenye bahari kutokana na kuongezeka kwa ujazo

3 APRILI, 2018

wa maji ya bahari, kuyeyuka kwa barafu katika vilele vya milima mirefu kama vile Mlima wa Kilimanjaro, kuharibika kwa madaraja, reli, barabara na makazi kutokana na mafuriko na kuongezeka kwa vimbunga. Majanga haya huathiri zaidi nchi maskini kama ya kwetu kutokana na uwezo wake mdogo wa kuhimili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na umuhimu kwa kila Mtanzania kuishi katika mazingira bora na salama, Tanzania ni mionganoni mwa nchi zilizokuwa mstari wa mbele katika uhifadhi wa mazingira na katika nchi yetu tumetenga takribani asilimia 30 ya ardhi kwa ajili ya uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, kuridhia makubaliano haya kutasaidia nchi yetu kufanya mikakati yake ya maendeleo kwa namna endelevu. Tanzania imekuwa ikishirikiana na nchi nyingine katika utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi tangu ulipopitishwa. Katika ushirikiano huo, Tanzania imenufaika na miradi yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 700 ambayo imesaidia kutekelezwa kwa miradi mbalimbali katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwemo Mradi wa Usambazaji Maji Simiyu, tumesomesha wanafunzi takribani 200 kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika shahada mbalimbali na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa mengine yatokanayo na uanachama wa Tanzania kwenye Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi ni pamoja na utekelezaji wa mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Pwani ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Vilevile tumeweza kufanikiwa kupata mradi wa kuongeza uhimili ambaao uliwezesha upatikanaji wa maji katika Wilaya za Igunga (Tabora), Nyasa (Ruvuma), Misenyi (Kagera) na Wilaya ya Kaskazini A. Pia upo mradi wa vijiji vya mfano (*Eco Village Project*) ambaao umewezesha upatikanaji wa nishati na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya Dodoma, Morogoro na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna mradi wa kurejeleza ardhii iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo ya nyanda kame (*Reversing Land Degradation Trends in Increasing Food Security in Degraded Ecosystems in Semi-arid Areas of Central Tanzania*). Mradi huu unalenga kurejesha mifumo ya ikolojia ya kilimo iliyoharibika ili kuongeza uzalishaji wa chakula katika maeneo kame na pwani ya nchi. Mradi huo unatekelezwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na utekelezaji wa mradi huu ni manufaa ya uanachama na ushiriki wa Tanzania katika mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya vijiji kupitia mfumo wa ikolojia (*Ecosystem-Based Adaptation for Rural Resilience in Tanzania*). Lengo la mradi huu ni kuziongezea jamii za vijijiini uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kuimarisha uhimilivu wa mifumo ya ikolojia na kupata njia mbadala za kujenga ustawi wa jamii. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri tano nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, tumeanzisha Kituo cha Kitaifa cha Ufuatiliaji na Upimaji wa Hewa Ukaa (*National Carbon Monitoring Center*) kilichopo Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Kwa ujumla, miradi yote hii imetekelizwa katika pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na faida hizo, utekelezaji wa Mkataba huu na Itifaki yake umekubwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kutoshirikisha nchi zote katika upunguzaji wa gesijoto hivyo kusababisha upunguzaji wake kuwa mdogo na kuongezeka kwa gharama za kukabiliana na majanga ya athari za mabadiliko ya tabianchi hasa kwa nchi maskini kama ya kwetu. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Mkutano wa 21 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Paris, Desemba, 2015 ulipitisha kwa kauli moja makubaliano ya Paris. Makubaliano hayo ya Paris yana malengo makuu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuongeza ushirikishwaji wa nchi zote duniani katika juhudzi za kuhakikisha kwamba joto la dunia haliongezeki zaidi ya *centigrade* mbili kabla ya mwisho wa karne hii na kuhakikisha kwamba ongezeko la gesijoto duniani linabaki chini ya *centigrade* 1.5 ikilinganishwa na kabla ya maendeleo ya viwanda. Pia kuongeza uwezo wa nchi kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuchochaea upunguzaji wa gesijoto usioathiri maendeleo na uhakika wa chakula kwa nchi husika. Vilevile lengo lake ni kuongeza upatikanaji wa fedha na teknolojia kwa ajili ya kusaidia maendeleo himilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni mionganini mwa nchi zilizoathirika kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabianchi katika sekta zote. Hivyo kuridhia kwa makubaliano ya Paris kutasaidia nchi yetu kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, kupata teknolojia safi ambazo zitasaidia katika mikakati ya Serikali ya kujenga uchumi endelevu wa viwanda na wenye kustahimili mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tutanufaika na kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa chakula, kutunza misitu ambayo ipo hatarini kutoweka, kuandaa na kutekeleza mikakati na mipango ambayo itasaidia kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta za afya, kilimo, maji na sekta nyinginezo hasa zile zinazoathirika na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, nchi yetu itapata fedha za kutekeleza programu za miradi kupitia mifuko mbalimbali kama vile Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi na taasisi za kimataifa kama vile Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (ACP).

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa makubalino ya Paris utazingatia misingi ya usawa, uwezo na historia ya nchi na hali yake ya uchumi. Kwa maana hiyo, nchi yetu haitabanwa wala kulazimishwa kupunguza uzalishaji wa gesijoto duniani bali itashiriki katika juhudzi hizo kwa hiyari na bila kushurutishwa, ukizingatia kwamba mchango wa nchi yetu katika kuongezeka kwa gesijoto duniani ni mdogo mno.

3 APRILI, 2018

Hata hivyo, kama Tanzania ingekuwa inabanwa kisheria kupunguza uzalishaji wa gesijoto bado ina ziada ya uwezo wa kunyonya gesijoto kuitia misitu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Tanzania inazalisha kiasi cha tani za hewa ya *carbon 0.2* pekee kwa mwaka wakati ina misitu takribani hekari milioni 48 ambayo ina uwezo wa kunyonya kiasi cha takribani tani tisa za hewa ya *carbon*. Aidha, ardhi ya Tanzania ina eneo la takribani asilimia 30 ambalo limehifadhiwa kisheria na linaendelea kunyonya gesijoto zinazozalishwa duniani bila mipaka. Hata hivyo, utekelezaji wa makubaliano ya Paris ni wa hiyari, hakuna sheria za kuzibana nchi wanachama na makubaliano haya yanairuhusu nchi kujitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na dhana kwamba nchi yetu tukiridhia makubaliano haya basi tutalazimishwa kufanya maendeleo kwa namna ambayo itapunguza kasi yetu ya maendeleo. Ukweli ni kwamba kwa mujibu wa mkataba huu nchi zinapaswa kuweka mipango yake ya upunguzaji wa mchango wake kwenye gesijoto duniani kulingana na mazingira halisi ya nchi hiyo, kwa hiyo, hakuna wasiwasi huo. Sisi tunadhani kwamba manufaa makubwa zaidi yapo kwenye mchango ambao Tanzania itaupata kutoka kwenye Jumuia ya Kimataifa kwenye jitihada zake za kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi (*adaptation*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nchi kuwa mwanachama wa Makubaliano ya Paris, Ibara ya 20 inaelekeza nchi husika kuridhia makubaliano haya kama iliyio kwenye mikataba mingine ya kimataifa. Hadi kufikia tarehe 21 Aprili, 2016, ambacho ni kipindi maalum kilichowekwa kwa nchi kusaini, jumla ya nchi 182 zilikuwa zimesaini ikiwemo Tanzania. Aidha, kufikia tarehe 28 Machi, jumla ya nchi 175 zilikuwa zimeridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufikia akidi ya nchi zinazohitajika kuridhia yaani nchi 55, makubaliano ya Paris yameingia katika hatua ya utekelezaji kabla ya muda

uliopangwa ambao ni mwaka 2020. Kimsingi utekelezaji wake umeanza tangu tarehe 4 Novemba, 2016. Hivyo kuna umuhimu wa nchi yetu kuridhia ili iungane na nchi nyingine katika utekelezaji na kuendelea kunufaika na fursa zilizopo. Kwa upande wa Bara la Afrika, hadi kufikia tarehe 26 Machi, 2018 nchi 45 kati ya nchi 54 za Afrika zilikuwa zimeridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kupitia kwa haraka vipengele muhimu vyta makubaliano haya ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufahamu kwa kina.

Kwanza Ibara ya Pili ya makubaliano inazungumzia lengo na lengo kuu kwa kweli ni kushirikisha nchi zote wanachama katika jitihada za kushughulikia mabadiliko ya tabianchi hasa upunguzaji wa gesijoto duniani na kusaidia nchi zinazoendelea kama Tanzania kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo lingine ni kuongeza upatikanaji wa chakula na kuchochea maendeleo endelevu. Utekelezaji wa makubalino haya utazingatia misingi ya usawa, uwezo na hali ya uchumi wa nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 3 inazungumzia wajibu wa nchi mbalimbali katika kutekeleza makubaliano haya. Nchi zitatakiwa kuandaa na kuwasilisha taarifa kuhusu juhudzi zake za kufikia malengo ya makubaliano ya Paris kama yalivyoainishwa katika Ibara za 4, 7, 9, 10, 11 na 13. Nchi zilizoendelea zitawajibika kuchangia fedha za kusaidia nchi zinazoendelea katika kutekeleza programu na miradi ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na miradi ya upunguzaji wa gesijoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 inazungumzia muda wa kufikia kiwango cha juu cha upunguzaji wa gesijoto. Nchi zinatakiwa kupunguza gesijoto kwa lengo la kufikia kiwango cha juu cha upunguzaji kwa kuzingatia misingi ya usawa na maendeleo endelevu na kuondoa umaskini. Makubaliano haya yanabainisha kuwa nchi zinazoendelea zitahitaji muda mrefu zaidi kufikia kiwango

3 APRILI, 2018

cha juu cha kupunguza gesijoto. Hatutawekewa *deadline* ambayo hatutaweza kuimudu ya kupunguza kiwango cha gesijoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tano inazungumzia sekta ya misitu, inasema kwamba kila nchi mwanachama inahimizwa kutunza misitu inayonyonya gesijoto. Juhudi hizi zikizingatiwa zitachangia kuongezeka kwa motisha na kasi ya kutunza misitu ambayo huchangia upatikanaji wa mvua na kuhifadhi vyanzo vya maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Sita inazungumzia ushirikiano wa hiari katika utekelezaji. Nchi zitashirikiana kwa hiari katika utekelezaji wa mikakati ya kupunguza gesijoto na kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kuchochea maendeleo endelevu na hifadhi ya mazingira. Mfumo wa kusimamia upunguzaji wa gesijoto duniani umeanzishwa ili kutoa motisha na kuchochea ushiriki wa taasisi za umma na sekta binafsi katika jitihada hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Saba inazungumzia kuhimili mabadiliko ya tabianchi, kwamba kila nchi mwanachama inawajibika kuandaa na kutekeleza mipango ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi (*National Action Plan*). Kuimarisha uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kutasaidia kupunguza athari za ukame, mafuriko na kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tisa inazungumzia upatikanaji wa fedha za utekelezaji. Makubaliano ya Paris yanatoa haki kwa nchi zinazoendelea ambazo ni mwanachama kupata fedha za kushughulikia changamoto za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kuititia ufadhili wa mifuko ya mabadiliko ya tabianchi na wadau wengine. Nchi zilizoendelea zitatakiwa kutoa taarifa kila baada ya miaka miwili kuhusu kiwango cha fedha walizotoa au wanazotarajia kutoa kama msaada kwa nchi ambazo ziko hatarini kuathirika na mabadiliko ya tabianchi. Kama nilivyoyeleza hapo awali kwamba ushiriki wetu katika Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi hadi sasa umewezesha

3 APRILI, 2018

nchi kupata msaada wa takribani shilingi bilioni 700. Tunaamini kwamba tukiridhia Makubaliano ya Paris fursa hizi zitapanuka na kuongezeka zaidi na hasa mchango wa nchi zinazoendelea kupitia mifuko mbalimbali ya mabadiliko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 inazungumzia teknolojia na imeweka mfumo wa nchi zinazoendelea kupata teknolojia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 inazungumzia kuhusu kujengewa uwezo. Inasema kwamba nchi zinazoendelea, kama nchi yetu, zina haki ya kujengewa uwezo na uelewa katika kushughulikia mabadiliko ya tabianchi, hali ambayo itaongeza uelewa wa jamii kuhusu hatua za kuchukua ili kupunguza athari za mabadiliko haya katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 inazungumzia uwazi katika utekelezaji. Ibara hii inazitaka nchi wanachama kuwa na mfumo wa uwazi wa kupeana taarifa kuhusu utekelezaji wa makubaliano ili kuhakikisha kwamba malengo yanafikiwa. Mfumo huu umewekwa makusudi ili kuwezesha nchi kutambua uwezo mdogo wa nchi maskini na utatekelezwa kwa hiari bila kuingilia uhuru wa nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 20 inazungumza kuhusu utaratibu wa uridhiaji na inasema kwamba kila nchi itaridhia kulingana na taratibu zake kama sisi tunavyofanya hivi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 28 inazungumzia uhuru wa kujitoa na inasema kwamba nchi ina haki ya kujitoa katika makubaliano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania inaingia kwenye uchumi wa viwanda, Makubaliano ya Paris yatasaidia kuchochea matumizi ya gesi asilia, upatikanaji wa teknolojia safi, kufunza wataalam wetu na kuendelea kuwa na vyanzo vya nishati endelevu ili kukabiliana na uchafuzi

3 APRIL, 2018

wa mazingira. Aidha, Makubaliano ya Paris yataongeza ushirikiano, upatikanaji wa fedha na kuchochera biashara ya hewa ukaa na upashanaji wa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa nchi yetu kuridhia utazingatia Katiba ya nchi yetu ambayo inalipa Bunge madaraka ya kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri yetu na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Hati ya kuridhia itawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambaye ana jukumu la kupokea na kuhifadhi hati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba niwasilishe Azimio la Bunge la Kuridhia kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mionganoni mwa nchi wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 1992 na Itifaki yake ya Kyoto ya mwaka 1997;

Na kwa kuwa nchi yetu iliridhia mkataba huo mwaka 1996 na itifaki hiyo mwaka 2002; Na kwa kuwa lengo kuu la mkataba huu na itifaki yake ni kuzuia ongezeko la gesijoto na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mifumo ya ikolojia ya dunia ili kuhakikisha maendeleo endelevu duniani;

Na kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yanababishiwa athari nyingi ikiwa ni pamoja na ukame, mafuriko, kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza, kumezwa kwa visiwa vidogo kwenye bahari kutokana na kuongezeka kwa ujazo wa maji ya bahari, kuyeyuka kwa barafu kwenye vilele vya milima mirefu kama vile Kilimanjaro na uharibifu wa miundombinu ya barabara, reli, makazi kutokana na mafuriko na kuongezeka kwa vimbunga;

Na kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mionganoni mwa nchi zinazoathirika kwa kiasi kikubwa na matokeo hasi ya mabadiliko ya tabianchi;

3 APRILI, 2018

Na kwa kuwa tangu mkataba huu na itifaki yake iridhiwe na nchi wanachama na kuanza kutekelezwa kumejitokeza changamoto katika utekelezaji wake ikiwemo nchi zilizoendelea kuogopa kupoteza nguvu za kiuchumi kwa sababu ya utekelezaji wa mkataba huu utaathiri uzalishaji viwandani na kupunguza matumizi ya nishati chafu, ushindani wa kiuchumi baina ya nchi zinazoendelea na zile zenyel uchumi unaokua haraka, unasababisha kuongezeka kwa viwanda vinavyochafua mazingira na kutoshirikisha nchi zote katika upunguzaji wa gesijoto kunasababisha upunguzaji wake kuwa mdogo na kuongezeka kwa ghamara za kukabiliana na majanga ya mabadiliko ya tabianchi, hasa kwa nchi zinazoendelea;

Na kwa kuwa nchi yetu inatambua changamoto hizo na umuhimu wa kila Mtanzania kuishi katika mazingira bora na safi;

Na kwa kuwa katika Mkutano wa 21 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Paris (Ufaransa), Desemba, 2015 nchi wanachama wa mkataba walipitisha Makubaliano ya Paris kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi; Na kwa kuwa Makubaliano ya Paris yanalenga kuboresha utekelezaji wa mkataba ule wa mwaka 1992 kwa kufanya yafuatayo:-

Kwanza kutunza misitu inayonyonya joto; kuandaa na kutekeleza mipango ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi; kuwa na mifumo ya upatikanaji wa fedha na teknolojia safi kwa nchi zinazoendelea kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi na kuweka utaratibu wa kuzijengea uwezo nchi zinazoendelea katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi;

Na kwa kuwa makubaliano haya yalitiwa saini na nchi wanachama ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2016 huko New York, Marekani;

Na kwa kuwa makubaliano haya yatawezesha nchi wanachama kuchukua hatua madhubuti katika kuuboresha utekelezaji wa mkataba huu ikiwa ni pamoja na kuongeza ushirikishwaji wa nchi zote duniani katika juhudzi za kuhakikisha kwamba joto duniani haliongezeki zaidi ya *centigrade degree* mbili kabla ya mwisho wa karne hii na kuongezeka kwa uwezo wa nchi kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuchochaea upunguzaji wa gesijoto usioathiri maendeleo na uhakika wa chakula kwa nchi husika, kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha na teknolojia kwa ajili ya kusaidia maendeleo himilivu;

Na kwa kuwa ni muhimu kwa nchi yetu iridhie makubaliano haya ili kuwezesha utekelezaji wake, wenyewe lengo la kupambana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 1992 na kuendelea kunufaika na ushirikiano wa kikanda na wa kimataifa katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi;

Na kwa kuwa hatua hii itasaidia kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kupata teknolojia safi ambazo zitasaidia katika mikakati ya Serikali ya kujenga uchumi endelevu wa viwanda na wenyewe kustahimili mabadiliko ya tabianchi; Na kwa kuwa nchi yetu kwa kuweka saini makubaliano haya na hatimaye kuyatekeleza itanufaika na mambo yafuatayo:-

Kwanza, kuwa mionganini mwa nchi zilizo mstari wa mbele katika kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kunusuru uchumi wa nchi yetu; kuimarika kwa ushirikiano baina ya nchi yetu na jumuiya ya kimataifa katika kusimamia na kutekeleza masuala yanayohusu mabadiliko ya tabianchi; kuongeza upatikanaji wa fursa zilizopo na za miradi na teknolojia safi itakayowezesha matumizi ya gesi asilia majumbani na viwandani ili kuchochaea maendeleo ya viwanda kwa kutumia nishati yenye bei nafuu na kuimarisha hali ya uchumi wa nchi na kujenga uchumi endelevu wa viwanda na wenyewe kustahimili mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha mipango ya Taifa ya kuhimili athari ya mabadiliko

3 APRILI, 2018

ya tabianchi ili kupunguza majanga yatokanayo na athari hizo; Na kwa kuwa utekelezaji wa makubaliano hayo ni wa hiari na nchi ina uhuru wa kujitoa; Na kwa kuwa katika Kikao cha Baraza la Mawaziri cha Nne cha mwaka 2017/2018 kilikubali Makubaliano ya Paris kuhusu kuboresha utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi yaridhiwe na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Hivyo basi kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na mkataba huu na itifaki yake kwa Tanzania na pia umuhimu wa manufaa ya makubaliano hayo, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 linaazimia kuridhia Makubaliano ya Paris kuhusu Kuboresha Utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Toa hoja Mheshimiwa January Makamba.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liridhie Makubaliano ya Paris kuhusu Kuboresha Utekelezaji wa Mkataba wa Makubaliano ya Tabianchi (*The Paris Agreement under the United Nations Framework Convention on Climate Change*).

**MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA), MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MAKUBALIANO YA PARIS CHINI YA MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU MKATABA WA MABADILIKO YA TABIANCHI (THE PARIS AGREEMENT UNDER THE UN FRAMEWORK CONVENTION ON CLIMATE CHANGE) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa Kimataifa kuhusu Binadamu na Mazingira ulifanyika huko Stockholm, Sweden tarehe 5-16 Juni 1972. Mkutano huo ulisisitiza kuwa

maendeleo ya kiuchumi ni lazima yaende sambamba na suala la hifadhi ya Mazingira. Aidha, mwanzoni mwa miaka ya themanini wanasayansi walianza kutoa taarifa kwamba joto la dunia lilianza kuongezeka kuanzia kipindi cha mapinduzi ya viwanda. Kufuatia angalizo hilo, mwaka 1988, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) kwa kushirikiana na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) walipitisha uamuzi wa kuunda Jopo la Kimataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (*Intergovernmental Panel on Climate Change - IPCC*). Lengo la Jopo hilo lilikuwa kujadili matokeo ya uchunguzi wa kisayansi kuhusu sababu za ongezeko la joto duniani ambalo lilionekana kusababisha mabadiliko ya tabianchi. Taarifa ya kwanza ya Jopo ilitolewa mwaka 1990 na kuwasilishwa mbele ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN General Assembly). Baada ya kujadili taarifa hiyo Mkutano wa Umoja wa Mataifa uliunda Kamati ya Majadiliano ya Kimataifa (*Intergovernmental Negotiating Committee - INC*) ambayo ilianzisha majadiliano ya kuunda Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi. Tarehe 5 Mei 1992 Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi ulipitishwa huko Rio de Janeiro, Brazil wakati wa Mkutano wa Dunia kuhusu mazingira na maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania iliridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi mwaka 1996 na Itifaki yake ya Kyoto mwaka 2002. Lengo la Mkataba huu ni kuzuia ongezeko la gesijoto na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mifumo ya ikolojia ya dunia ili kuhakikisha maendeleo endelevu duniani. Mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko katika mifumo ya hali ya hewa yanayosababishwa na ongezeko la joto la dunia. Sababu za kuongezeka kwa gesijoto ni kutokana na matumizi makubwa ya nishati chafuzi kwa shughuli za maendeleo zilizofanyika katika nchi zilizoendelea kwa zaidi ya miaka 150 iliyopita. Athari zitokanazo na mabadiliko hayo ni pamoja na ukame, mafuriko, kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza, kumezwa kwa visiwa vidogo kwenye bahari kutokana na kuongezeka kwa ujazo wa maji ya bahari, kuyeyuka kwa barafu katika vilele vya milima mirefu kama vile Mlima Kilimanjaro, uharibifu wa madaraja, reli, barabara na makazi

3 APRILI, 2018

kutokana na mafuriko na kuongezeka kwa vimbunga. Majanga haya huathiri zaidi nchi maskini kutokana na uwezo wake mdogo wa kuhimili.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kutambua changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na umuhimu wa kila mtanzania kuishi katika mazingira bora na salama, Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoko mstari wa mbele katika uhifadhi wa mazingira na imetenga zaidi ya asilimia 30 ya ardhi kwa ajili ya uhifadhi. Hivyo, kuridhia Makubaliano haya kutasaidia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Tanzania imekuwa ikishirikiana na nchi nyingine katika utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi tangu ulipopitishwa. Katika ushirikiano huo Tanzania imenufaika na miradi yenye thamani ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 300 ambayo imesaidia yafuatayo: - ununuzi wa vifaa vya utabiri wa hali ya hewa vyenye thamani ya zaidi ya sh. 150 milioni. na vitendea kazi vya Ofisi; kujenga uwezo wa wataalam ambapo watanzania zaidi ya 200 wamefadhliliwa kusomea masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika ngazi ya shahada ya uzamili na zaidi ya 50 shahada ya uzamifu; kuongeza ushiriki na ushawishi katika agenda na mikakati ya jumuiya ya kimataifa kuhusu suala la mabadiliko ya tabianchi; Kuanzisha Kituo cha Mafunzo ya Mabadiliko ya Tabianchi (*Centre for Climate Change Studies*) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; mradi wa kusambaza maji kutoka Ziwa Victoria hadi Mkoa wa Simiyu.

**Mheshimiwa Spika**, manufaa mengine yaliyotokana na uanachama wa Tanzania kwenye Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi ni utekelezaji wa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Katika Maeneo ya Pwani ya Tanzania Bara na Zanzibar ambao umejenga ukuta wa fukwe katika maeneo ya Barabara ya Obama - *Ocean Road* (920m) na Kigamboni (Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere – 480m); ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua ili kupunguza mafuriko maeneo ya Bungoni (475m), kata ya Buguruni (Wilaya ya Ilala) na Miburani – Mtoni (550m) (Wilaya ya Temeke); Mradi wa kuongeza uhimili ambao uliwezesha upatikanaji wa maji katika Wilaya za Igunga mkoani Tabora katika Vijiji vya

Nanga, Igumbi, Majengo na Itunduru, Nyasa mkoani Ruvuma kijiji cha Ng'ombo, Misenyi mkoani Kagera katika vijiji vya Byeju, Mbale, Kanyigo, Kashasha, Bukwali na Kitobo na Wilaya ya Kaskazini A kijiji cha Nungwi; Mradi wa Vijiji vya Mfano (*Eco-villages Project*) ambao umewezesha upatikanaji wa nishati na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji vya Chololo - Dodoma; Luguru - Morogoro; na Zanzibar. Mradi wa kurejeleza ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame ya nyanda za kati (*Reversing land degradation trends and increasing food security in degraded ecosystems of semi-arid areas of central Tanzania*). Mradi unalenga kurejesha mifumo ya ikolojia ya kilimo iliyoharibika ili kuongeza uzalishaji wa chakula katika maeneo kame na pwani ya nchi. Mradi unatekelezwa katika Kata ya Haubi (Halmashauri ya Kondoa); Kata ya Sigili (Halmashauri ya Nzega); Kata ya Mpambala (Halmashauri ya Mkalama); Kata ya Sukuma (Halmashauri ya Magu); na Kata ya Micheweni na Kiuyu Maziwa Ngombe, katika wilaya ya Micheweni, Kaskazini Pemba.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Vijiji kuititia Mfumo Ikolojia (*Ecosystem-Based Adaptation for Rural Resilience in Tanzania*). Lengo la mradi ni kuziongezea jamii za vijiji uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kuimarisha uhimilivu wa mfumo-ikolojia na kupata njia mbadala za kujenga ustawi wa jamii. Mradi huu utatekelezwa katika Halmashauri tano (5) ambazo ni: - Kishapu (Shinyanga), Mpwapwa (Dodoma), Mvomero (Morogoro), Simanjoro (Manyara) na Kaskazini Unguja, Shehia A (Unguja).

Vilevile chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi kimeanzishwa Kituo cha Kitaifa cha Ufutiliaji na Upimaji wa Hewa Ucaa (*National Carbon Monitoring Centre- NCMC*) kilichopo Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA). Kwa ujumla miradi chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi imetekelizwa katika pande zote za Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na faida hizo, utekelezaji wa Mkataba huu na Itifaki yake umekumbwa na

changamoto kadhaa zikiwemo: kutoshirikisha nchi zote katika upunguzaji wa gesijoto hivyo kusababisha upunguzaji wake kuwa mdogo na kuongezeka kwa gharama za kukabiliana na majanga ya athari za mabadiliko ya tabianchi hasa kwa nchi maskini. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Mkutano wa 21 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Paris, Ufaransa, Desemba, 2015 ulipitisha Makubaliano ya Paris. Makubaliano ya Paris yana malengo makuu yafuatayo: - kuongeza ushirikishwaji wa nchi zote duniani katika juhudzi za kuhakikisha joto la Dunia haliongezeki zaidi ya 2oC kabla ya mwisho wa karne hii na kuhakikisha kuwa ongezeko ya gesijoto linabaki chini ya 1.5oC ikilinganishwa na kabla ya maendeleo ya viwanda; kuongeza uwezo wa nchi kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuchochea upunguzaji wa gesijoto usioathiri maendeleo na uhakika wa chakula kwa nchi husika; kuongeza upatikanaji wa fedha na teknolojia kwa ajili ya kusaidia maendeleo himilivu.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni mionganini mwa nchi zinazoathirika na mabadiliko ya tabianchi katika sekta zote. Hivyo, kuridhia Makubaliano ya Paris kutasaidia kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, kupata teknolojia safi (*clean technology*) ambazo zitasaidia katika mikakati ya serikali ya kujenga uchumi endelevu wa viwanda na wenye kustahimili mabadiliko ya tabianchi; kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa chakula; kutunza misitu ambayo iko hatarini kutoweka; kuandaa na kutekeleza mikakati na mipango ambayo itasaidia kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta za afya, kilimo, maji na sekta nyingine zinazoathirika na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Tanzania itapata fedha za kutekeleza programu na miradi kuititia Mifuko kama vile Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi na Taasisi za Kimataifa kama vile umoja wa nchi za African Caribbean and Pacific (ACP).

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Makubaliano ya Paris utazingatia misingi ya usawa, uwezo na historia ya nchi na hali ya uchumi wake. Aidha, chini ya Makubaliano hayo, Tanzania haitabanwa au kulazimishwa kupunguza uzalishaji

wa gesijoto bali itashiriki katika juhudhi hizo kwa hiari bila kushurutishwa. Hata kama Tanzania ingekuwa inabanwa kisheria kupunguza uzalishaji wa gesijoto bado ina ziada ya uwezo wa kunyonya gesijoto kuititia misitu yake. Kwa sasa Tanzania inazalisha kiasi cha tani za hewa ya kaboni 0.2 pekee kwa mwaka wakati ina misitu takribani hekari 48 millioni ambayo ina uwezo wa kunyonya kiasi cha tani 9 za hewa ya kaboni. Aidha, ardhi ya Tanzania ina eneo la takriban asimilia 30 ambalo limehifadhiwa kisheria na linaendelea kunyonya gesijoto zinazozalishwa duniani bila mipaka. Hata hivyo, utekelezaji wa Makubaliano ya Paris ni wa hiari, hakuna sheria za kuzibana nchi wanachama na Makubaliano haya yanaruhusu nchi kujitoa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa nchi kuwa Mwanachama wa Makubaliano ya Paris, Ibara ya 20 inaelekeza nchi husika kuridhia Makubaliano haya kama ilivyo kwa mlikataba mingine ya kimataifa. Hadi kufikia tarehe 21 Aprili, 2016 (Kipindi maalum kichowekwa kwa nchi kusaini), jumla ya nchi 182 zilikuwa zimesaini ikiwemo Tanzania. Aidha, kufikia tarehe 28 Machi, 2018 jumla ya nchi 175 zilikuwa zimeridhia. Baada ya kufikia akidi inayohitajika (55), Makubaliano ya Paris yameingia katika hatua ya utekelezaji kabla ya muda uliopangwa ambao ni mwaka 2020. Kimsingi, utekelezaji wake umeanza tangu tarehe 4 Novemba, 2016. Hivyo, kuna umuhimu wa Tanzania kuridhia ili iungane na nchi nyingine katika utekelezaji na kuendelea kunufalka na fursa zilizopo. Kwa upande wa Bara la Afrika, hadi kufikia tarehe 26 Machi 2018, nchi 45 zilikuwa zimeridhia.

**Mheshimiwa Spika**, vipengele muhimu vya Makubaliano ya Paris ni kama ifuatavyo: -

**Moja, Ibara ya 2: Lengo la Makubaliano.** Lengo ni kushirikisha nchi zote wanachama katika juhudhi za kushughulikia mabadiliko ya tabianchi hasa upunguzaji wa gesijoto na kusaidia nchi zinazoendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, kuongeza upatikanaji wa chakula na kuchochea maendeleo endelevu. Utekelezaji utazingatia misingi ya usawa, uwezo na hali ya uchumi wa nchi husika.

**Mibili, Ibara ya 3: Wajibu wa nchi katika kutekeleza Makubaliano ya Paris.** Nchi itatakiwa kuandaa na kuwasilisha taarifa kuhusu juhudzi zake katika kufikia malengo ya Makubaliano ya Paris kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 4, 7, 9, 10, 11 na 13. Nchi zilizoendelea zitawajibika kuchangia fedha za kusaidia Nchi zinazoendelea kutekeleza programu na miradi ya kuhimili athari za mabadiliko haya na miradi ya upunguzaji gesijoto.

**Tatu, Ibara ya 4: Muda wa kufikia kiwango cha juu cha upunguzaji gesijoto.** Nchi zinatakiwa kupunguza gesijoto kwa lengo la kufikia kiwango cha juu cha upunguzaji kwa kuzingatia misingi ya usawa na maendeleo endelevu na kuondoa umasikini. Makubaliano yanabainisha kuwa nchi zinazoendelea zitahitaji muda mrefu zaidi kufikia kiwango cha juu cha kupunguza gesijoto.

**Nne, Ibara ya 5: Sekta ya misitu.** Kila nchi mwanachama inahimizwa kutunza misitu inayonyonya gesijoto. Juhudi hizi zikizingatiwa zitachangia kuongezeka kwa motisha na kasi ya kutunza misitu ambayo huchangia upatikanaji wa mvua na kuhifadhi vyanzo vya maji nchini.

**Tano, Ibara ya 6: Ushirikiano wa Hiari katika utekelezaji.** Nchi zitashirikiana kwa hiari katika utekelezaji wa mikakati ya kupunguza gesijoto na kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kuchochaea maendeleo endelevu na hifadhi ya mazingira. Mfumo wa kusimamia upunguzaji wa gesijoto umeanzishwa ili kutoa motisha na kuchochaea ushiriki wa taasisi za umma na sekta binafsi katika upunguzaji wa gesijoto na kuchochaea maendeleo endelevu.

**Sita, Ibara ya 7: Kuhimili mabadiliko ya tabianchi.** Kila nchi mwanachama inawajibika kuandaa na kutekeleza mipango ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Kuimarisha uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi utasaidia kupunguza athari za ukame, mafuriko, na kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza.

**Saba, Ibara ya 9: Upatikanaji wa fedha za utekelezaji.** Makubaliano ya Paris yanatoa haki kwa Nchi zinazoendelea ambazo ni Mwanachama kupata fedha za kushughulikia changamoto za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kuititia ufadhili wa Mifuko ya Mabadiliko ya Tabianchi na wadau wengine. Nchi zilizoendelea zitatakiwa kutoa taarifa kila baada ya miaka miwili kuhusu kiwango cha fedha walizotoa au wanatarajia kutoa kama msaada kwa nchi ambazo ziko hatarini kuathirika na mabadiliko ya tabianchi.

**Nane, Ibara ya 10: Teknolojia.** Ibara imeweka mfumo wa Nchi Zinazoendelea kupata teknolojia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**Tisa, Ibara ya 11: Kujengewa uwezo.** Nchi Zinazoendelea zina haki ya kujengewa uwezo na uelewa katika kushughulikia mabadiliko ya tabianchi. Hali ambayo itaongeza uelewa kwa jamii kuhusu hatua za kuchukua ili kupunguza athari za mabadiliko haya katika maeneo yao.

**Kumi, Ibara ya 13: Uwazi katika utekelezaji.** Ibara inazitaka nchi wanachama kuwa na mfumo wa uwazi wa kupeana taarifa kuhusu utekelezaji wa Makubaliano ili kuhakikisha malengo yake yanafikiwa. Mfumo huu utatambua uwezo mdogo wa nchi maskini na utatekelezwa kwa hiari bila kuingilia uhuru wa nchi husika.

**Kumi na Moja, Ibara ya 20: Utaratibu wa uridhiaji.** Kila nchi itaridhia kulingana na utaratibu wake. Pale ambapo jumuiya yoyote ambayo Tanzania ni mwanachama itaamua kujunga na Makubaliano haya, utaratibu wa mgawanyo wa majukumu ya utekelezaji utaridhiwa baina ya Tanzania na jumuiya husika.

**Kumi na Mbili, Ibara ya 28: Uhuru wa kujitoa.** Nchi ina uhuru wa kujitoa baada ya kupita miaka mitatu ya kuwa mwanachama. Aidha, Nchi ikijitoa kwenye Mkataba mama (Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi) itahesabika imejitoa pia kwenye Makubaliano haya.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Tanzania inaingia kwenye uchumi wa viwanda, Makubaliano ya Paris yatasaidia kuchochea matumizi ya gesi asilia; upatikanaji wa teknolojia safi; kufunza watalaan wetu, na kuendelea kuwa na vyanzo vya nishati endelevu ili kukabiliana na uchafuzi wa mazingira. Aidha, Makubaliano ya Paris yataongeza ushirikiano, upatikanaji wa fedha, kuchochea biashara ya hewa ukaa na upashanaji taarifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Tanzania utaratibu wa kuridhia utazingatia Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo inalipa madaraka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kujadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Hati ya kuridhia itawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambaye ana jukumu la kupokea na kuhifadhi Hati hizo.

**Mheshimiwa Spika**; baada ya maelezo haya, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la kuridhia kama ifuatavyo: -

**KWA KUWA**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mionganini mwa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 1992 na Itifaki yake ya Kyoto ya mwaka 1997;

**NA KWA KUWA**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Mkataba mwaka 1996 na Itifaki yake mwaka 2002;

**NA KWA KUWA**, Lengo kuu la Mkataba huu na Itifaki yake ni kuzuia ongezeko la gesijoto, na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mifumo ya ikolojia ya Dunia ili kuhakikisha maendeleo endelevu diniani;

**NA KWA KUWA**, mabadiliko ya tabianchi yanasaababisha athari nydingi ikiwa ni pamoja na ukame, mafuriko, kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza, kumezwa kwa visiwa vidogo kwenye bahari kutokana na kuongezeka

3 APRILI, 2018

ujazo wa maji ya bahari, kuyeyuka kwa barafu katika vilele vya milima mirefu kama vile Milima Kilimanjaro na uharibifu wa miundombinu ya barabara, reli na makazi kutokana na mafuriko na kuongezeka kwa vimbunga;

**NA KWA KUWA,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mionganoni mwa Nchi zinazoathirika na matokeo hasi ya mabadiliko ya tabianchi;

**NA KWA KUWA,** tangu Mkataba huu na Itifaki yake uridhiwe na Nchi Wanachama kuanza kutekelezwa mwaka 1996 na 2002, kumejitokeza changamoto katika utekelezaji ikiwa ni pamoja na: Nchi Zilizoendelea kuogopa kupoteza nguvu za kiuchumi kwa sababu utekelezaji wa Mkataba huu utaathiri uzalishaji viwandani kwa kupunguza matumizi ya nishati chafu; ushindani wa kiuchumi baina ya Nchi Zinazoendelea na zile zenye uchumi unaokua haraka unasababisha kuongezeka kwa viwanda vinavyochafua mazingira; na kutoshirikisha nchi zote katika upunguzaji wa gesijoto kunasababisha upunguzaji wake kuwa mdogo na kuongezeka kwa gharama za kukabiliana na majanga ya mabadiliko ya tabianchi hasa kwa Nchi Zinazoendelea;

**NA KWA KUWA,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua changamoto hizo na umuhimu wa kila Mtanzania kuishi katika mazingira bora na salama;

**NA KWA KUWA,** katika Mkutano wa 21 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Paris – Ufaransa Desemba, 2015, Nchi Wanachama wa Mkataba walipitisha Makubaliano ya Paris kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi;

**NA KWA KUWA,** Makubaliano ya Paris yanalenga kuboresha utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 1992 kwa kufanya yafuatayo: - kutunza misitu inayonyonya joto; kuandaa na kutekeleza Mipango ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi; kuwa na mifumo ya

upatikanaji wa fedha na teknolojia safi kwa Nchi Zinazoendelea kwa ajili ya kukabiliana na changamoto ya Tabianchi; na kuweka utaratibu wa kuzijengea uwezo Nchi zinazoendelea katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya Tabianchi;

**NA KWA KUWA,** Makubaliano haya yalitiwa saini na Nchi Wanachama ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2016 huko New York - Marekani;

**NA KWA KUWA,** Makubaliano haya yatawezesha Nchi Wanachama kuchukua hatua madhubuti katika kuboresha utekelezaji wa Mkataba ikiwa ni pamoja na kuongeza ushirikishwaji wa nchi zote duniani katika juhudzi za kuhakikisha joto Dunia haliongezeki zaidi ya 20C kabla ya mwisho ya karne hii, kuongeza uwezo wa nchi kuhimili mabadiliko, athari za mabadiliko ya tabianchi na kuchochlea upunguzaji wa gesijoto usioathiri maendeleo na uhakika wa chakula kwa nchi husika, kuongeza upatikanaji wa fedha na teknolojia kwa ajili ya kusaidia maendeleo himilivu;

**NA KWA KUWA,** ni muhimu nchi yetu iridhie Makubaliano hayo, ili kuwezesha utekelezaji wake wenye lengo la kupambana na chamgamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 1992, na kuendelea kunufaika na ushirikiano wa Kikanda na Kimatalifa katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi;

**NA KWA KUWA,** hatua hii itasaidia kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, kupata teknolojia safi (*clean technology*) ambazo zitasaidia katika mikakati ya Serikali ya kujenga uchumi endelevu wa viwanda na wenye kustahimili mabadiliko ya tabianchi;

**NA KWA KUWA,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka saini Makubaliano hayo na hatimaye kuyatekeleza itanufaika na mambo yafuatayo: -

3 APRILI, 2018

- a) kuwa mionganoni mwa nchi zilizoko mstari wa mbele katika kupambana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi ili kunusuru uchumi wa nchi yetu;
- b) kuimarika kwa ushirikiano baina ya Nchi yetu na Jumuia ya Kimataifa katika kusimamia na kutekeleza masuala yanayohusu mabadiliko ya tabianchi;
- c) kuongeza upatikanaji wa fursa zilizopo za miradi na teknolojia safi itakayowezesha matumizi ya gesi asilia majumbani na viwandani ili kuchochaea maendeleo ya viwanda kwa kutumia nishati yenye bei nafuu;
- d) kuimarisha hali ya uchumi wa nchi na kujenga uchumi endelevu wa viwanda wenye kustahimili mabadiliko ya tabianchi;
- e) kuimarika kwa mipango ya Taifa ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi ili kupunguza majanga yatokanayo na athari hizo;

**NA KWA KUWA**, utekelezaji wa Makubaliano hayo ni wa hiari na nchi ina uhuru wa kujitoa;

**NA KWA KUWA**, Baraza la Mawaziri katika Kikao chake Na. 4/2017 -18 lilikubali Makubaliano ya Paris kuhusu Kuboresha Utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi yaridhiwe na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

**HIVYO BASI**, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu na Itifaki yake kwa Tanzania na pia umuhimu na manufaa ya Makubaliano hayo, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia Makubaliano ya Paris kuhusu kuboresha utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi yaani **THE PARIS AGREEMENT UNDER THE UN FRAMEWORK CONVENTION ON CLIMATE CHANGE**.

3 APRILI, 2018

**Mheshimiwa Spika;** naomba kuwasilisha na kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na utaratibu wetu. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Makubaliano ya Paris yatokanayo na utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (*The Paris Agreement under the UN Framework Convention on Climate Change*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) na (4), ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Makubaliano ya Paris yatokanayo na utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi ililetwa mbele ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ajili ya kulipitia, kulichambua na hatimaye kulishauri Bunge kuliridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Makubaliano ya Paris.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Paris wa

3 APRILI, 2018

Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 1992 na Itifaki yake ya Kyoto ya mwaka 1997 (*Kyoto Protocol*). Tanzania iliridhia mkataba huu tarehe 17 Aprili, 1996 na itifaki yake mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la mkataba wa mabadiliko; katika kutekeleza mkataba huu na itifaki zake kumejitokeza changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Baadhi ya nchi wanachama kuhofia kupoteza nguvu za kiuchumi kwa sababu utekelezaji wa mkataba huu utaathiri uzalishaji viwandani kwa kupunguza matumizi ya nishati chafu;

(ii) Ushindani wa kiuchumi baina ya nchi zinazoendelea na zile zenyet uchumi unaokua haraka unasababisha kuongezeka kwa viwanda vinavyochafua mazingira; na

(iii) Kutoshirikisha nchi zote katika upunguzaji wa gesijoto na kuongezeka kwa gharama za kukabiliana na majanga ya mabadiliko ya tabianchi, hasa kwa nchi zilizoendelea kukwepa gharama zinazosababishwa na athari za kuongezeka kwa gesijoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto tajwa, nchi wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi walipitisha Makubaliano ya Paris kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 1992. Makubaliano haya yalifiwiwa katika Mkuutano wa 21 uliyofanyika Paris, Ufaransa tarehe 30 Novemba hadi tarehe 22 Desemba, 2015 na kutiwa saini na nchi wanachama ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2016 huko New York, Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhununi la mabadiliko haya ni kuboresha utekelezaji wa mkataba kwa kuweka wajibu wa nchi wanachama kutekeleza mabadiliko ya Paris kama ifuatavyo:-

3 APRILI, 2018

(i) Kuongeza ushirikishwaji wa nchi zote duniani katika juhudzi za kuhakikisha joto haliongezeki zaidi ya *centigrade* mbili kabla ya mwisho wa karne hii ya 21;

(ii) Kuweka utaratibu wa kuzijengea uwezo nchi zinazoendelea katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi;

(iii) Nchi kuhimizwa kutunza misitu inayonyonya gesijoto; na

(iv) Kuzuia ongezeko la gesijoto na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mifumo ya ikolojia ya dunia ili kuhakikisha maendeleo endelevu duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna Kamati ilivyoshughulkia hoja hii; katika kushughulkia Azimio hili, Kamati ilikutana na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la kuridhia mabadiliko ya Mkataba wa Paris wa Mabadiliko ya Tabianchi siku ya Jumatano, tarehe 28 Machi, 2018. Kabla ya kupokea na kujadili taarifa ya Serikali kuhusu Azimio hili, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Uchambuzi wa Azimio kutoka kwa Mshauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria. Uchambuzi huo ulisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri kuifanya kazi hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa mabadiliko haya hayakinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria za nchi zinazohusiana na usimamizi wa uhifadhi wa mazingira. Faida zitakazopatikana kutokana na kuridhia makubaliano hayo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha ushirikiano mionganini mwa nchi wanachama katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Kuongeza fursa za upatikanaji wa miradi na teknolojia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na

(iii) Kuogeza mipango ya Taifa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijiridhisha kuhusu maudhui ya Makubaliano ya Paris kwa kuititia vifungu vya mkatuba huo. Baadhi ya vifungu muhimu katika Makubaliano ya Paris ni pamoja na Ibara ya Tatu ambayo inaweka wajibu wa kila nchi katika kutekeleza Makubaliano ya Paris ambapo kila nchi itatakiwa kuandaa na kuwasilisha taarifa kuhusu juhudzi zake katika kufikia malengo ya makubaliano. Katika makubaliano haya, nchi zilizoendelea zitapaswa kuchangia fedha katika kutekeleza programu na miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na miradi ya upunguzaji gesjoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Sita ya Makubaliano ya Paris inazitaka nchi wanachama kuwa na ushiriki wa hiari katika utekelezaji wa mikakati ya kupunguza gesjoto na kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kuchochea maendeleo endelevu na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tisa ya Makubaliano ya Paris inaelezea manufaa ya makubaliano haya kifedha. Makubaliano ya Paris yameweka utaratibu wa nchi zinazoendelea ambazo ni wanachama kupata fedha za kushughulikia changamoto za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kuititia ufadhili wa mifuko ya mabadiliko ya tabianchi na wadau wengine. Aidha, nchi zilizoendelea zitatakiwa kutoa taarifa kila baada ya miaka miwili kuhusu kiwango cha fedha walichotoa au wanachotarajia kutoa kwa msaada wa nchi ambazo ziko hatarini kuathirika na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 ya Makubaliano ya Paris inatambua uwezo mdogo wa nchi zinazoendelea, hivyo, imeweka utaratibu wa hiari katika utekelezaji pasipo kuingilia uhuru wa nchi wanachama. Faida za kuridhia Azimio hili ni nydingi kuliko gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati; naomba sasa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lengo la Makubaliano ya Paris ni kuzuia ongezeko la gesijoto na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi;

Kwa kuwa sisi sote ni mashuhuda wa athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na ukame, mafuriko, kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza, kumezwa kwa visiwa vidogo kwenye bahari na maziwa kutokana na kuongezeka kwa ujazo wa maji, kuyeyuka kwa barafu katika kilele cha Mlima Kilimanjaro na uharibifu wa miundombinu ya barabara na makazi kutokana na mafuriko;

Na kwa kuwa Makubalino ya Paris yanalenga kuandaa na kutekeleza mipango ya kuhimili mabadiliko ya tabia nchi na kuweka mifumo ya upatikanaji wa fedha na teknolojia safi kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania kwa ajili ya kukabiliana na changamoto tajwa na kuweka utaratibu wa kuzijengea uwezo nchi zinazoendelea katika kukabiliana na changamoto hizo;

Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuridhia Makubaliano ya Paris ili kuwezesha utekelezaji wake wenye lengo la kupambana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi kama tulivyoainisha hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Kamati kumshukuru sana Mheshimiwa Spika na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa uongozi wenu mahiri. Kwa niaba ya Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Suleiman Saddiq na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wote tunapenda kumhakikisha Mheshimiwa Spika na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kuwa tutafanya kazi kwa weledi na uadilifu mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa

3 APRILI, 2018

Mussa Zungu na Mheshimiwa Najma Giga kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuendelea kuliongoza Bunge letu. Naomba pia kuwapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mheshimiwa January Makamba, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Kangi Lugola, Makatibu Wakuu pamoja na wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Azimio hili mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapo chini na kwa ruhusa yako, naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge yaani *Hansard*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati. Pamoja na yeye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bwana Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Sehemu ya Fedha na Uchumi, Bwana Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Bwana Wilfred Magova na Bi. Zainabu Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi. Pauline Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio. (*Makofii*)

3 APRILI, 2018

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA  
NA MAZINGIRA KUHUSU MAKUBALIANO YA PARIS KUHUSU  
KUBORESHA UTEKELEZAJI WA MKATABA WA MABADILIKO YA  
TABIANCHI (*THE PARIS AGREEMENT UNDER THE UN  
FRAMEWORK CONVENTION ON CLIMATE CHANGE*)  
KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) na (4) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane Kanuni ya 7(1) (b), ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016, hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Makubaliano ya Paris yatokanayo na utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (*The Paris Agreement Under the UN Framework Convention on Climate Change*) ililetwa mbele ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ajili ya kulipitia, kulichambua na hatimaye kulishauri Bunge kuliridhia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Makubaliano ya Paris.

**Mheshimiwa Spika**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi Mwanachama wa Mkataba wa Paris wa Mabadiliko ya Tabia nchi wa mwaka 1992 na Itifaki yake ya Kyoto ya mwaka 1997(Kyoto Procal). Tanzania iliridhia Mkataba huu tarehe 17 Aprili, 1996 na Itifaki yake mwaka 2002.

**2.0 CHIMBUKO LA MKATABA WA MABADILIKO**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza Mkataba huu na Itifaki zake kumejiotokeza changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- i) Baadhi ya nchi wanachama kuhofia kupoteza nguvu za kiuchumi kwa sababu utekelezaji wa Mkataba huu

3 APRILI, 2018

utaathiri uzalishaji viwandani kwa kupunguza matumizi ya nishati chafu;

ii) Ushindani wa kiuchumi baina ya nchi zinazoendelea na zile zenye uchumi unaokua haraka unasababisha kuongezeka kwa viwanda vinavyochafua mazingira; na

iii) Kutoshirikisha nchi zote katika upunguzaji wa gesijoto na kuongezeka kwa gharama za kukabiliana na majanga ya mabadiliko ya tabianchi hasa kwa nchi zilizoendelea kukwepa gharama zinazosabishwa na athari za kuongezeka kwa gesijoto.

**Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto tajwa nchi wanachama wa Mkataba wa mabadiliko ya tabianchi walipitisha Makubaliano ya Paris kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba wa mabadiliko ya tabianchi wa mwaka 1992. Makubaliano haya ya yalifikiwa katika mkutano wa ishirini na moja (21) uliofanyika Paris-Ufaransa tarehe 30 Novemba hadi 22 Disemba, 2015 na kutiwa saini na nchi wanachama ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania terehe 22 Aprili, 2016 huko New York-Marekani.

**Mheshimiwa Spika**, dhununi la mabadiliko haya ni kuboresha utekelezaji wa Mkataba kwa kuweka wajibu kwa nchi wanachama kutekeleza Makubaliano ya Paris kama ifuatavyo:-

i) Kuongeza ushirikishwaji wa nchi zote duniani katika juhudzi za kuhakikisha joto haliongezeki zaidi ya nyuzi 20C kabla ya mwisho wa karne hii ya 21;

ii) Kuweka utaratibu wa kuzijengea uwezo nchi zinazoendelea katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi;

iii) Nchi kuhimizwa kutunza misitu inayonyonya gesijoto; na

3 APRILI, 2018

iv) Kuzuia ongezeko la gesijoto na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mifumo ya lkolojia ya Dunia ili kuhakikisha maendeleo endelevu duniani.

### 3.0 NAMNA KAMATI ILIVYOSHUGHULIKIA HOJA HII

**Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia Azimio hili, Kamati ilikutana na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la kuridhia Mabadiliko ya Mkataba wa Paris wa Mabadiliko ya Tabianchi siku ya Jumatano tarehe 28 Machi, 2018. Kabla ya kupokea na kujadili Taarifa ya Serikali kuhusu Azimio hili, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Uchambuzi wa Azimio kutoka kwa Mshauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria. Uchambuzi huo ulisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuwa mabadiliko haya hayakinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria za nchi zinazohusiana na usimamizi na uhifadhi wa mazingira.

**Aidha**, faida zitakazopatikana kutohana na kuridhia Makubaliano hayo ni pamoja na:-

i) Kuimarisha ushirikiano mionganini mwa nchi wanachama katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

ii) Kuongeza fursa za upatikanaji wa miradi na teknolojia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

iii) Kuongeza mipango ya Taifa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuhusu maudhui ya Makubaliano ya Paris kwa kuititia vifungu vya mkataba huo. Baadhi ya vifungu muhimu katika Makubaliano ya Paris ni pamoja na **Ibara ya 3** ambayo inaweka wajibu wa kila nchi katika kutekeleza makubaliano ya Paris ambapokila nchi itatakiwa kuaandaa na kuwasilisha

3 APRILI, 2018

taarifa kuhusu juhudini zake katika kufikia malengo ya makubaliano. Katika makubaliano haya nchi zilizoendelea zitapaswa kuchangia fedha katika kutekeleza programu na miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na miradi ya upunguzaji gesijoto.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6** ya Makubaliano ya Paris inazitaka nchi wanachama kuwa na ushiriki wa hiari katika utekelezaji wa mikakati ya kupunguza gesijoto na kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kuchochea maendeleo endelevu na uhifadhi wa mazingira.

**Ibara ya 9** ya Makubaliano ya Paris inaelezea manufaa ya Makubaliano haya kifedha. Makubaliano ya Paris yameweka utaratibu wa nchi zinazoendelea ambazo ni wanachama kupata fedha za kushughulikia changamoto za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kuititia ufadhili wa mifuko ya mabadiliko ya tabianchi na wadau wengine. Aidha, nchi zilizoendelea zitatakiwa kutoa taarifa kila baada ya miaka miwili kuhusu kiwango cha fedha walichotoa au wanachotarajia kutoa kama msaada wa nchi ambazo ziko hatarini kuhathirika na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13** ya Makubaliano ya Paris inatambua uwezo mdogo wa nchi zinazoendelea hivyo imeweka utaratibu wa hiari katika utekelezaji pasipo kuingilia uhuru wa nchi wanachama. Aidha, faida za kuridhia Azimio hili ni nyingi kuliko gharama.

#### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa**, lengo kuu la Makubaliano ya Paris ni kuzuia ongezeko la gesijoto na athari zitokanazo na mabadiiko ya tabianchi, na

**Kwa kuwa**, sisi sote ni mashuhuda wa athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali nchini

ikiwa ni pamoja na ukame, mafuriko, kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza, kumezwa kwa visiwa vidogo kwenye bahari na maziwa kutokana na kuongezeka kwa ujazo wa maji, kuyeyuka kwa barafu katika kilele cha Mlima Kilimanjaro na uharibufu wa miundombinu ya barabara na makazi kutokana na mafuriko, na

**Kwa kuwa,** Makubaliano ya Paris yanalenga kuandaa na kutekeleza mipango ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kuweka mifumo ya upatikanaji wa fedha na teknolojia safi kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania, kwa ajili ya kukabiliana na changamoto tajwa na kuweka utaratibu wa kuzijengea uwezo nchi zinazoendelea katika kukabiliana na changamoto hizo,

**Hivyo basi,** Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuridhia Makubaliano ya Paris ili kuwezesha utekelezaji wake wenye lengo la kupambana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kama tulivyo ziainisha hapo awali.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nikushukuru sana wewe na Naibu Spika kwa uongozi mahiri. Binafsi nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunitfea kuwa Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambapo nilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Mhe. Andrew Chenge, Mhe. Mussa Zungu na Mhe. Najma Giga kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuendelea kuliongoza Bunge letu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba pia kuwapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba (Mb), Naibu Waziri wake

Mhe. Kangi Lugola (Mb) Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano waloutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano waloutoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Azimio hili mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa rukhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard).

- i) Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb.....Mwenyekiti
- ii) Mhe. Innocent Lughah Bashungwa, Mb .....M/Mwenyekiti
- iii) Mhe. David Cecil Mwambe, Mb.....Mjumbe
- iv) Mhe. Balozi Dkt. Diodorus B. Kamala, Mb.....Mjumbe
- v) Mhe. Salim Hassan Turky, Mb.....Mjumbe
- vi) Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb.....Mjumbe
- vii) Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb.....Mjumbe
- viii) Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb.....Mjumbe
- ix) Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb .....Mjumbe
- x) Mhe. Munde Tabwe Abdalah, Mb.....Mjumbe
- xi) Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb.....Mjumbe
- xii) Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb.....Mjumbe
- xiii) Mhe. Mussa Rashid Ntimizi, Mb.....Mjumbe
- xiv) Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb.....Mjumbe
- xv) Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb.....Mjumbe
- xvi) Mhe. Kmamis Ali Vuai, Mb.....Mjumbe
- xvii) Mhe. Zainab Mdolwa Amiri, Mb.....Mjumbe
- xviii) Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb.....Mjumbe
- xix) Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.....Mjumbe
- xx) Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb.....Mjumbe
- xxi) Mhe. Mansoor Hirani Sharif, Mb.....Mjumbe
- xxii) Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb.....Mjumbe
- xxiii) Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb.....Mjumbe
- xxiv) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb.....Mjumbe
- xxv) Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb.....Mjumbe
- xxvi) Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.....Mjumbe

3 APRILI, 2018

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano ambao amekuwa akitoa kwa Kamati; pamoja na yeye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bw. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.

Innocent Lugha Bashungwa, (Mb)

**MAKAMU MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA  
MAZINGIRA**

3 Aprili, 2018

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tutamsikia Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - MSEMAJI MKUU WA KAMBI  
YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (*The Paris Agreement under the UN Framework on Climate Change*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa suala la mabadiliko ya tabianchi ni mtambuka kwa maana kwamba madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri maisha ya binadamu na viumbwe wengine ikiwa ni pamoja na maliasili na mazingiara yetu kwa ujumla.

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kuwa Mkataba huu wa Kimataifa ulitiwa saini Desemba, 2015 huko Paris katika Mkutano wa Kimataifa wa 21 wa mabadiliko ya tabianchi. Mpaka sasa nchi 195 zimesaini mkataba huu na kati ya hizo nchi 175 zimeridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilisaini mkataba huu tarehe 22 Aprili, 2016 huko New York, Marekani katika hafla iliyoandaliwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Bwana Ban Ki-moon na kuifanya Tanzania kuwa ni nchi ya tano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuridhia mkataba huu ikiungana na Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda. Kuletwa kwa Azimio hili ni ishara kuwa tunaungana na juhudzi za kimataifa katika kushughulikia changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi la kuhoji siku zote ni kwa nini Serikali inachelewa kuleta Bungeni Maazimio ya Kimataifa ambayo ni muhimu kwa ajili ya maisha yetu ya kila siku?

Pamoja na kuwa kwa wakati huu wa Azimio hili limekuja mapema kidogo tofauti na maazimio mengine, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Maazimio ya Kimataifa kama hili linalojadiliwa leo yanaletwa Bungeni mapema zaidi kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni kuhusu Makubaliano ya Paris; Makubaliano ya Paris yamekuja baada ya malalamiko ya muda mrefu ya nchi zinazoendelea kuhusu namna zinavyoathirika na mabadiliko ya tabianchi huku uzalishaji mkubwa wa gesijoto ukifanywa na nchi zinazoendelea na ambazo uchumi na ushawishi wao wa kimataifa ni mkubwa. Hata wakati wa mjadala wa makubaliano haya taarifa zinaonyesha kuwa mataifa yanayoendelea hayakuwa thabitii kusimamia matakwa yao kwa sababu ya kuogopa kunyimwa misaada na nchi zinazoendelea duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tisa ya mkataba huu inazungumzia na inatoa masharti ya namna nchi zilizoendelea zinavyoghamramia masuala ya kupunguza athari ya mabadiliko ya tabianchi au kuondoa kabisa athari hizo. Tatizo la Ibara hii ni kuwa inazitaja nchi zilizoendelea kwa ujumla wake na hata utaratibu wa kuchangia mpaka sasa haujawekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa Ibara ya Tisa imewekwa kama kisafisha macho tu, lakini haitoi jukumu la nchi ambazo zinatakiwa kuchangia nchi zinazoendelea kukabiliana na athari hizi huku ikizingatiwa kuwa nchi hizo zinakabiliwa na changamato za kibajeti kugharamia huduma za kawaida za nchi hizo na hivyo kuwa vigumu kwao kuwa na bajeti nyingine ya mabadiliko ya tabianchi. Pamoja kuridhia Azimio hili kuhusu mkataba huu, ni vyema Serikali ikasisitiza na kuendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kuwa makubaliano katika mkataba huu yanafanyiwa marekebisho ili kutoa jukumu la kisheria kwa nchi zilizoendela kutoa fedha kwa ajili ya masuala ya mabadiliko ya tabianchi kwa nchi zinazoendelea ambazo huathiriwa zaidi pamoja na kuwa wanazalisha gesijoto kidogo zaidi ikilinganishwa na nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujandaa kukabiliana na majanga; Ibara ya 8(4) ya mkataba inaanisha maeneo ushirikiano ambapo pamoja na mambo mengine inasisitiza kujandaa na majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi. Taarifa zinaonyesha kuwa kwa miaka 40 nchi yetu imekuwa ikabiliwa na ukame na mafuriko katika nyakati mbalimbali mambo ambayo yanahusishwa moja kwa moja na mabadiliko ya tabianchi. Siku za hivi karibuni Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro, Mwanza imeathirika sana na mabadiliko ya tabianchi jambo ambalo limesababisha wananchi wengi kukosa makazi. Nyakati zote za majanga Serikali imekuwa ikionekana dhaifu kutokana na kutokuwa na vifaa na nyenzo za kuzuia athari hizo pamoja na kushindwa kuwasaidia kwa wakati wahanga wa majanga hayo.

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, katika masharti ya mkataba huu inaonekana dhahiri kuwa hakuna jukumu la moja kwa moja la kisheria kwa nchi zilizoendelea la kuwalipa fidia wananchi wanaaoathirika na majanga kama haya. Ikumbukwe kuwa majanga ya mafuriko na ukame yanaathiri sekta za kilimo, mifugo pamoja na miundombinu ya umeme na hivyo kwa ujumla kuathiri ukuaaji wa uchumi wa nchi yetu. Pamoja na kutegemea fedha kutoka nje kwa maana ya michango ya nchi zilizoendelea kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ni vyema sisi wenyewe tukajipanga zaidi kukabiliana na matokeo hasi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri maisha yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 7(5) inaweka masharti ya ushirikishwaji wa jamii ikiwa ni pamoja na uwazi na masuala ya jinsia katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza umuhimu wa jambo hili kufanyika wakati wa utekelezaji wa sheria zetu tulizojiwekea kuhusu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa jamii zetu kitamaduni zimekuwa na shughuli mbalimbali kwa muda mrefu na kwa vizazi na vizazi ambazo kwa namna moja ama nyingine zimekuwa zikilinda mazingira. Mathalani huko Iringa na Njombe wananchi wamekuwa wakifanya shughuli zao za kilimo kwenye maeneo maarifu kama vinyungu, lakini Serikali imekuwa ikitumia Sheria ya Maji na Mazingira kuwaelekeza kuwa wanatakiwa kufanya hivyo kwa umbali wa mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji. Katika Mkoa wa Kilimanjaro wananchi wengi wanaishi milimani kwenye vyanzo vya maji na wamekuwa wakifanya shughuli za kilimo kwa miaka mingi huku wakitunza mazingira lakini baada ya utaratibu wa mita 60 Serikali inaingia kwenye mgogoro na wananchi ambao ni wadau wakubwa katika masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu umeweka utaratibu wa kushirikisha jamii na tamaaduni zao kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na juhudzi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ni vyema kama

nchi tukaona namna ya kushirikisha jamii zetu na tamaduni zetu kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na kuridhia Azimio hili, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali na wadau wengine wa mabadiliko ya tabianchi kusisitiza uwepo wa marekebisho au itifaki nyingine ambayo itatatau changamoto za masuala ya jinsia kuhusu mabadiliko ya tabianchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji na mabadiliko ya tabianchi. Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta mbalimbali za nchi. Vilevile ifahamike kuwa ni muhimu uwekezaji huo kuzingatia teknolojia ambayo ni rafiki kwa mazingira na ambayo inatoa gesijoto kidogo ili kuepuka madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 ya mkataba inazungumzia na kutoa masharti kuhusu ushirikiano wa kimataifa kuhusu masuala ya teknolojia rafiki kwa mazingira ambayo hutoa gesijoto kidogo. Pamoja na hekaya za Serikali kuhusu uchumi wa viwanda ambao haujafanyiwa utafiti wa soko la uzalishaji wa bidhaa hizo inaelekea Serikali inaitilia mkazo kidogo sana kwenye masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa hali ilivyo hasa kwenye miji mikubwa nchini athari za mabadiliko ya tabianchi ni ya dhahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Mkuranga wananchi wameanza kulalamika kutokana na kutanda kwa wingu zito la moshi unaozalishwa na viwanda. Ni vyema Serikali ikaona namna ya kutatua kero hiyo ambayo kwa namna moja ama nyingine inaweza kuathiri wananchi zaidi huko baadee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika Wilaya ya Nzega mwekezaji wa Mgodi wa Resolute baada ya kuvuna madini ameacha mashimo bila kurejesha mazingira katika hali yake ya awali na kupelekeea athari kubwa ikiwemo vifo vya wananchi. Ni vyema basi kuzingatia masuala ya mazingira katika uwekezaji kwa ujumla na matokeo chanya ya uwekezaji tunatakiwa kulinda mangira yetu kwa ajili ya vizazi vijavyo. (*Makofii*)

3 APRILI, 2018

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya jumla; kwa kuridhia mabadiliko yaliyopo katika mkataba huu, kama nchi tunalo jukumu la kuzingatia masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza, upatikanaji wa fedha za kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Tunatambua kwamba katika makubaliano haya ya kimataifa nchi zilizoendelea zina jukumu la kutoa fedha kwa nchi zinazoendelea ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Tunatambua kuwa fedha hizo zimekuwa hazitolewi kwa kiasi cha kuridhisha na kwa wakati kama zilivyo kubaliwa na zilivyo ahidiwa na nchi zilizoendelea. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha kutoka vyanzo vyta ndani ili kuweza kukubaliana na athahri za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali iweke mikakati madhubuti kuweza kupata fedha moja kwa moja (*direct funding*) kutoka mifuko mbalimbali ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi ikiwemo *Green Climate Fund, Adaptation Fund* na *Global Environment Facility*. Ileleweke kuwa fedha nydingi zimekuwa zikipotea kwa ajili ya kulipa mashirika ya kimataifa na wataalam ili kuweza kupata fedha hizo ambapo hupunguza kiasi kinachofika nchini kwa utekelezaji. Suala hili linaweza kuondolewa kwa kuboresha uwezo wa taasisi za Serikali kufikia vigezo tengwa na pia kujenga utashi na ushawishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa fedha zinazopatikana zinaelekezwa katika miradi ya vipaumbele na yenye manufaa kwa nchi na vilevile kuwepo usimamizi madhubuti na matumizi ya fedha hizo ili kuepuka ujisadi ambao umejitokeza katika baadhi ya miradi inayotekelzwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya mabadiliko ya tabianchi ili kuweza kuboresha matumizi bora na kuepuka ujisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, upunguzaji wa utoaji gesijoto na matumizi ya vyanzo vyta nishati; Kambi

Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa Tanzania inatoa kiasi kidogo cha gesijoto (*greenhouse gases*) ikiwa ni chini ya asilimia moja duniani. Kutokana na shughuli za kibinadamu pamoja na ongezeko la watu ambavyo vyote viwili vitaongeza matumizi ya nishati kwa kiasi kikubwa, kuna haja ya kupata uwiano mzuri wa kufikia malengo yote mawili, maendeleo ya shughuli za kiuchumi ikiwemo uwekezaji na kupunguza utoaji wa gesijoto na kuwa na maendeleo endelevu. Pia Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuhakikisha kuwa inafanya mchanganyiko mzuri wa matumizi ya vyanzo vyta nishati kwa kujumuisha nishati jadidifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu, kujumuisha masula ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi katika mipango na bajeti ya Serikali; Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kujumuisha masuala ya mkataba huo pamoja na masuala ya mabadiliko ya tabianchi kiujumla katika mipango ya bajeti. Hii itasaidia kufikia shabaha za nchi katika kutekeleza mkataba huo. Serikali kuititia Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Fedha iweke kasma maalum ya mabadiliko ya tabianchi (*budget expenditure code*) ili kurahisisha suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne, ushirikishwaji wa wadau; Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuhakikisha kuwa inashirikisha kikamilifu wadau wote ikiwemo vyama vyta siasa, asasi za kiraia, sekta binafsi na wadau wa maendeleo na jamii kwa ujumla kama tulivyoeleza ili kuweza kutekeleza vizuri masharti yaliyopo katika mkataba huu. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza dhana hii kujumuisha ngazi zote kuanzia katika uchaguzi wa vipaumbele, tathmini ya utekelezaji na matokeo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; athari za mabadiliko ya tabianchi ni dhahiri na tunahitaji kuwa na mipango ya ndani kukabiliana nazo na si kusubiri michango au fedha za nchi zilizoendelea ambazo kuzipata ni changamoto. Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono

3 APRILI, 2018

Azimio hili lakini inaitaka Serikali kuzingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS MAZINGIRA,  
KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MAKUBALIANO YA  
PARIS CHINI YA MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU  
MABADILIKO YA TABIANCHI (THE PARIS AGREEMENT UNDER  
THE UN FRAMEWORK CONVENTION ON CLIMATE CHANGE)  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za  
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)*

---

**1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (The Paris Agreement under the UN Framework on Climate Change).

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa suala la mabadiliko ya tabianchi ni suala mtambuka kwa maana kwamba; madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi yanaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine, ikiwa ni pamoja na maliasili na mazingira yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kuwa Mkataba huu wa kimataifa ulitiwa saini makubaliano Desemba 2015 huko Jijini Paris-Ufaransa katika Mkutano Kimataifa wa Ishirini na Moja (21) wa Mabadiliko ya Tabianchi. Mpaka sasa, nchi 195 zimesaini Mkataba huu na kati ya hizo, nchi 175 zimeridhia Mkataba huu.

3 APRILI, 2018

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ilisaini Mkataba huu tarehe 22 Aprili, 2016 huko Jijini New York-Marekani katika hafla iliyoandalisha na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa – Bw. Ban Ki Moon na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya 5 katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuridhia Mkataba huu ikiungana na Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda.

**Mheshimiwa Spika**, kuletwa kwa Azimio hili ni ishara kuwa tunaungana na juhudzi za kimataifa katika kushughulikia changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Suala la msingi la kuhoji siku zote ni kwa nini Serikali inachelewa kuleta Bungeni Maazimio ya Kimataifa ambayo ni muhimu kwa ajili ya maisha yetu ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa kwa wakati huu Azimio hili limekuja mapema kidogo tofauti na maazimio mengine Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa maazimio ya kimataifa kama hili linalojadiliwa leo yanaletwa Bungeni mapema zaidi kwa ajili kuridhiwa na Bunge.

2.      **MAONI KUHUSU MAKUBALIANO YA PARIS**  
2.1     **Nchi Zilizoendelea na Mabadiliko ya Tabianchi**

**Mheshimiwa Spika**, Makubaliano ya Paris yamekuja baada ya malalamiko ya muda mrefu ya nchi zinazoendelea kuhusu namna zinavyoathirika na mabadiliko ya tabianchi huku uzalishaji mkubwa wa gesijoto ukifanywa na nchi zilizoendelea na ambazo uchumi na ushawishi wao kimataifa ni mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, hata wakati wa mjadala wa makubaliano haya, taarifa zinaonesha kuwa Mataifa yanayoendelea hayakuwa thabiti kusimamia matakwa yao kwa sababu ya kuogopa kunyimwa misaada na nchi zilizoendelea duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 9 ya Mkataba huu inazungumzia na inatoa masharti ya namna nchi

zilizoendelea zikavyoghamaria masuala kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi au kuondoa kabisa athari hizo. Tatizo la ibara hii ni kuwa inazitaja nchi zilizoendelea kwa ujumla wake na hata utaratibu wa kuchangia haujawekwa.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa ibara ya 9 imewekwa kama kisafisha macho tu lakini haitoi jukumu la nchi ambazo zinatakiwa kuchangia nchi zinazoendelea kukabiliana na athari hizi huku ikizingatiwa kuwa nchi hizo zinakabiliwa na changamoto za kibajeti kugharamia huduma za kawaida za wananchi na hivyo kuwa vigumu kuwa na bajeti nydingine ya mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuridhia Azimio kuhusu Mkataba huu, ni vema Serikali ikasisitiza na kuendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kuwa Makubaliano katika Mkataba huu yanafanyiwa marekebisho ili kutoa jukumu la kisheria kwa nchi zilizoendelea kutoa fedha kwa ajili ya masuala ya mabadiliko ya tabianchi kwa nchi zinazoendelea ambazo huathiriwa zaidi pamoja na kuwa wanazalisha gesijoto kidogo ukilinganisha na nchi zilizoendelea.

## 2.2 Kuiandaa Kukabiliana na Majanga

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 8(4) ya Mkataba inaainisha maeneo ya ushirikiano ambapo pamoja na mambo mengine inasisitiza kuiandaa na majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa zinaonyesha kuwa kwa miaka 40 nchi yetu imekuwa ikitabiliwa na ukame na mafuriko katika nyakati mbalimbali mambo ambayo yanahusishwa moja kwa moja na mabadiliko ya tabianchi. Siku za hivi karibuni Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na Mwanza imeathirika sana na mabadiliko ya tabianchi jambo ambalo liimesababisha wananchi wengi kukosa makazi.

**Mheshimiwa Spika**, nyakati zote za majanga Serikali imekua ikionekana dhaifu kutokana na kutokuwa na vifaa na nyenzo za kuzuia athari hizo pamoja na kushindwa kuwasaidia kwa wakati wahanga wa majanga hayo. Katika

masharti ya mkataba huu inaonekana dhahiri kuwa hakuna jukumu la moja kwa moja la kisheria kwa nchi zilizoendelea za kuwalipa fidia wananchi wanaoathirika na majanga haya.

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa majanga ya mafuriko na ukame yanaathiri sekta za kilimo, mifugo pamoja miundombinu ya umeme na hivyo kwa ujumla kuathiri ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kutegemea fedha kutoka nje kwa maana ya michango ya nchi zilizoendelea kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ni vema sisi wenye we tukajipanga zaidi kukabiliana na matokeo hasi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri maisha yetu ya kila siku.

### 2.3 Ushirikishwaji wa Kijamii

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 7(5) inaweka masharti ya ushirikishwaji wa jamii ikiwa ni pamoja na uwazi na masuala ya jinsia katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza umuhimu wa jambo hili kufanyika wakati wa utekelezaji wa Sheria zetu tulizojiwekea kuhusu mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa jamii zetu kitamaduni zimekuwa na shughuli mbalimbali kwa muda mrefu na kwa vizazi na vizazi ambazo kwa namna moja ama nyingine zimekuwa zikilinda mazingira. Mathalani huko Iringa na Njombe wananchi wamekuwa wakifanya shughuli zao za kilimo kwenye maeneo maarufu kama "vinyungu" lakini Serikali imekuwa ikitumia Sheria ya Maji na ya Mazingira kuwaelekeza kuwa wanatakiwa kufanya hivyo kwa umbali wa mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkoa wa Kilimanjaro wananchi wengi wanaishi milimani kwenye vyanzo vya maji na wamekua wakifanya shughuli za kilimo kwa miaka mingi huku wakitunza mazingira lakini baada ya utaratibu wa mita

60 Serikali inaingia kwenye mgogoro na wananchi ambao ni wadau wakubwa katika masuala ya mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba huu umeweka utaratibu wa kushirikisha jamii na tamaduni zao kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na juhudzi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni vema kama nchi tukaona namna ya kushirikisha jamii na tamaduni zetu kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

#### **2.4 Kuzingatia Masuala ya Jinsia**

**Mheshimiwa Spika**, ieleweke kuwa, athari za mabadiliko ya tabiachi zinaathiri makundi mbalimbali ya kijamii katika nchi yetu. Ni wazi kuwa wanawake na watoto ni kati ya makundi ambayo yanaathirika zaidi na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, Makubaliano haya hayajatoa kwa upana masuala ya jinsia hasa namna wanawake watakavyopata fedha kwa ajili kufanya miradi ya mabadiliko ya tabianchi, kuwapatia na kuwaelemisha kutumia nishati jadidifu pamoja na kuwajengea uwezo kuelewa na kukabiliana na majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuridhia azimio hili, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali na wadau wengine wa mabadiliko ya tabia kusositiza uwepo wa marekebisho au itifaki nyingine ambayo itatatua changamoto za masuala ya jinsia kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

#### **2.5 Uwekezaji na Mabadiliko ya Tabianchi**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi uwekezaji wa sekti binafsi katika sekti mbalimbali nchini. Lakini ni vema ikafahamika kuwa ni muhimu uwekezaji huo kuzingatia teknolojia ambayo ni rafiki kwa mazingira na ambayo inatoa gesijoto kidogo ili kuepuka madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 10 ya Mkataba inazungumzia na kutoa masharti kuhusu ushirikiano wa kimataifa kuhusu masuala ya teknolojia rafiki kwa mazingira ambayo hutoa gesijoto kidogo. Pamoja na hekaya za Serikali kuhusu uchumi wa Viwanda ambao haujafanyiwa utafiti wa soko la uzalishaji wa bidhaa hizo inaelekea Serikali inatilia mkazo kidogo sana kwenye masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa hali ilivyo, hasa kwa miji mikubwa nchini, athari za mabadiliko ya tabianchi ni dhahiri.

**Mheshimiwa Spika**, katika Wilaya ya Mkuranga wananchi wameanza kulalamika kutokana na kutanda kwa wingu zito la moshi unaozalishwa na viwanda. Ni vema Serikali ikaona namna ya kutatua kero hiyo ambayo kwa namna moja ama nyingine inaweza kuathiri wananchi zaidi huko baadae.

**Mheshimiwa Spika**, hata katika Wilaya ya Nzega, mwekezaji wa Mgodi wa Resolute baada ya kuvuna madini ameacha mashimo bila kurejesha mazingira katika hali yake ya awali na kupelekea athari kubwa ikiwemo vifo vyta wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, ni vema kuzingatia masuala ya mazingira katika uwekezaji kwa kuwa pamoja na matokeo chanya ya uwekezaji tunatakiwa kulinda mazingira yetu kwa ajili ya vizazi vijavyo.

## 2.6 MAPENDEKEZO YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuridhia Makubaliano yaliyopo katika Mkataba huu kama nchi tunalo jukumu la kuzingatia masuala yafuatayo:

### (i) **Upatikanaji wa Fedha za Uhimili na Ukabili wa mabadiliko ya tabianchi**

**Mheshimiwa Spika**, tunatambua kwamba; katika makubaliano haya kimataifa, nchi zilizoendelea zina jukumu la kutoa fedha kwa nchi zinazoendelea ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Tunatambua kuwa fedha hizo zimekuwa hazitolewi kwa kiasi cha kuridhisha na kwa wakati

3 APRILI, 2018

kama zilivyokubaliwa na zilivyoahidiwa na nchi hizo zilizoendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha kutoka vyanzo vya ndani ili kuweza kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabanchi.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Serikali iweke mikakati madhubuti kuweza kupata fedha moja kwa moja (Direct Funding) kutoka mifuko mbalimbali ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi ikiwemo Green Climate Fund (GCF), Adaptation Fund (AF) na Global Environment Facility (GEF).

**Mheshimiwa Spika**, ieleweke kuwa fedha nyingi zimekuwa zikipotea kwa ajili ya kulipa mashirika ya kimataifa na wataalam ili kuweza kupata fedha hizo ambapo hupunguza kiasi kinachofika nchini kwa utekelezaji. Suala hili linaweza kuondolewa kwa kuboresha uwezo wa taasisi za Serikali kufikia vigezo tengwa na pia kujenga utashi wa ushawishi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa fedha zinapopatikana zinaelekezwa katika miradi ya vipaumbele na yenye manufaa kwa nchi na vilevile kuwepo usimamizi madhubuti wa matumizi ya fedha hizo ili kuepuka ujisadi ambao umejitokeza katika baadhi ya miradi inayotekelzwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kanzisha mfuko maalum kwa ajili ya mabadiliko ya tabianchi ili fedha ili kuboresha uwazi, matumizi bora na kuepuka ujisadi.

**(ii) Upunguzaji wa Utoaji wa Gesijoto na Matumizi ya Vyanzo vya Nishati**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa Tanzania inatoa kiasi kidogo cha gesijoto (Greenhouse Gases) ikiwa ni chini ya 1% kidunia. Kutokana na shughuli za kibinadamu pamoja na ongezeko la watu ambavyo vyote viwili vitaongeza matumizi ya nishati kwa kiasi kikubwa, kuna haja kupata uwiano mzuri wa kufikia

malengo yote mawili – maendeleo ya shughuli za kiuchumi ikiwemo uwekezaji na kupunguza utoaji wa gesijoto (kuwa na maendeleo endelevu); Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inafanya mchanganyiko mzuri wa matumizi ya vyanzo vya nishati kwa kujumuisha nishati jadidifu.

**(iii) Kujumuisha Masuala ya Mkataba na Mabadiliko ya Tabianchi katika Mipango na Bajeti za Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kujumuisha masuala ya Mkataba huu pamoja na masuala ya mabadiliko ya tabianchi kiujuimla katika mipango na bajeti. Hii itasaidia kufikia shabaha za nchi katika kutekeleza Mkataba huo. Serikali, kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Fedha, iweke kasma maalum ya mabadiliko ya tabianchi (budget/expenditure code) ili kurahisisha suala hilo.

**(iv) Ushirikishwaji wa Wadau**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inashirikisha kikamilifu wadau wote – ikiwemo vyama vya siasa, asasi za kiraia, sekta binafsi na wadau wa maendeleo na jamii kwa ujumla kama tulivyoeleza ili kuweza kutekeleza vizuri masharti yaliyopo katika Mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza dhana hii kujumuisha ngazi zote kuanzia katika uchaguzi wa vipaumbele, namna ya utekelezaji, utekelezaji na tathmini ya utekelezaji na matokeo yake.

**3. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, athari za mabadiliko ya tabianchi ni dhahiri na tunahitaji kuwa na mipango ya ndani kukabiliana nazo na si kusubiri michango au fedha za nchi zilizoendelea ambazo kuzipata ni changamoto. Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono Azimio hili lakini inaitaka Serikali kuzingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa.

3 APRILI, 2018

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha.

.....  
Ally Saleh Ally (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI.  
KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS- MUUNGANO NA  
MAZINGIRA**

3 April, 2018

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha hapa ya wachangiaji, tutaanza na Mheshimiwa George Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Salim, Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Azimio hili ambalo ni muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, niipongeze Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa taarifa yao nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu miaka ya 1960 haikuwa hivi, ilikuwa nchi nzuri sana, ilikuwa na misitu mikubwa na mito ambayo inatiririsha maji mwaka mzima. Kwa sababu ya shughuli za kibinadamu watu wamefyeka miti, wamechoma moto hovyo na mifugo isiyozingatia maeneo ya malisho sasa hivi misitu mingi sana katika maeneo yetu imekwisha. Misitu ndiyo inayoleta mvua na hali ya hewa nzuri na mito ndiyo inayoleta maji.

Maji ni uhai, maji ni maendeleo na maji ni uchumi wa nchi yetu. Lakini vyote hivi uharibifu huu wa ufyekaji, uchomaji moto hovyo ndiyo umesababisha majangwa, umesababisha ukame katika nchi hii kama Kamati ilivyoelezea ukame, milipuko ya magonjwa, viwanda, kemikali hizi, maji machafu yanamwagwa hovyo, madawa, makemikali yanasababisha watu wanapata magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sasa hivi takataka zinachomwa hovyo hata mijini utakuta mtu anachoma takataka sasa zile takataka zinatoa moshi, ule moshi unaharibu hali ya hewa badala ya watu kuvuta *oxygen* wanavuta *carbonmonoxide*, kwa hiyo ile ni *pollution of air by combustion* ambayo inaleta matatizo makubwa sana sana kwa Wananchi wetu wanapata matatizo ya magonjwa ya kifua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hali ya hewa inabadilika kunakuwa na joto kwa sababu ya mabadiliko hayo mpaka wakati fulani unakuta hata bahari maji nayo yanaongezeka. Kwa hiyo, wito wangu kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi wazingatie kutunza mazingira, bila kutunza mazingira nchi hii ndugu zangu tutakwenda wapi? Maji yatakwisha na bila maji dunia hii tutaishi wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuiweka Wilaya Mpwapwa, naomba nisome kidogo; "Mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya vijiji, Mfumo wa ikolojia na lengo la mradi huu ni kuongezea vijiji uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi" na Mpwapwa imo. Mpwapwa ilikuwa na misitu mikubwa sana, kulikuwa na Mto Shaban Robert wote mnaufahamu mmesoma kwenye vitabu, Shaban Robert. Ulikuwa unatiririsha maji mwaka mazima, sasa hivi uko wapi? Hakuna, umekauka kwa sababu watu wamechoma, watu wamefyeka hovyo mpaka sasa hakuna na kuna baadhi ya vijiji kuna ukame umeanza, barabara zinaharibika kwa sababu watu wamechoma, watu wamefyeka hovyo kwa hiyo, maji yanakuja kwa kasi yanaharibu barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana kabisa na Mheshimiwa Waziri kwamba azimio hili naliomba Bunge wote tukubaliane liweze kupita bila kipingwa na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yussuf Salim atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Richard Mbogo ajiandae.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika azimio hili lililopo mbele yetu.

Kwanza nisikitike tu kwamba Azimio lenyewe ni kubwa sana na kwa liliwyopangwa na litakavyojadiliwa sioni kama tumelipa thamani hiyo au uzito huo ambao inalo. Ni kitu kikubwa sana na ndiyo kinagusa maisha yetu sasa kujadiliwa hapa kwa siku moja sidhani kama tunalipa uzito huo, naomba tulipe uzito sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili nasema linagusa maisha yetu kwa sababu gani? Wamezungumza hapa katika *paragraph* ya nne kwamba kuna kupotea, sasa nitazungumza hii habari ya kupotea kwa visiwa na maeneo ya namna hiyo, *sea erosion*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna upoteaji mkubwa sana, lakini siyo kwamba vile visiwa vinaisha tu au ardhi inamegwaa na bahari kwa sababu ya nguvu ya maji, hatuishii hapo tu lakini kuna na viumbe vinapotea ambavyo vimo katika vile visiwa au katika bahari na vikiendelea kupotea viumbe na mimea ndiyo na sisi maisha yetu yanapotea vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mifano michache tu, kuna miti ambayo inapotea kwa kasi kubwa sana, *xylocarpus moluccensis* na *xylocarpus granatum* hii ni mitonga, mtonga mweusi na mtonga mwekundu inapotea sasa ikipotea hiyo ina maana kizazi chetu watakuja kuona au watakuja kusikia ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna *heritiera littoralis* (msikundasi) nayo inapotea. Kizazi chetu kinachokuja hii miti hawataikuta, watakapokuja hawakuti hii miti ni hisotoria itakuwa nini? Itakuwa tumewajengea faida gani? Lakini siyo hivyo tu ni mazalia ya viumbe vingine hii kama kaa, chanje kama hii miti haipo katika bahari ina maana na hivyo viumbe vingine navyo vinapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika visiwa vilevile kuna ndege ambaa ni *endemic*, ni ndege muhimu hapa duniani wanapotea vilevile. Kwa mfano *white eyes* (chigi manjano) sisi kule Zanzibar tunaita tayari wamepotea hawapo, sawa. Kuna ndege hawa *Javaspironous* tayari wanapotea hawapo na yote ni kwa sababu ya kwamba mabadiliko haya ya tabianchi yanapotea. Kwahiyo kupotea na kuondoka kwa visiwa siyo kwasababu tu kwmaba tuna ardhi inaondoka, lakini tunapoteza na hizo mnaita wenyewe sasa *bioanua* sijui na nini, vitu vyote vinapotea tutakuwa hatuna na kizazi chetu kitakujakurithi nchi ambayo mimea na ndege hawapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee mbele kuna tatizo linasema kwamba mvua hizi tunapata tunaita mabadiliko ya tabianchi, lakini hatuwezi kuwa na mabadiliko ya tabianchi mazuri tunayoyategemea kama sisi wenyewe hatujabadilika. Mwenyezi Mungu ametuleta duniani kuitawala dunia na vilivyomo ndani yake, je, sisi wenyewe tunalijua hili? Tumebadilika? Kama hatujabadilika na tunachokitawala katika dunia hii kitaendelea kuharibika, hakitakuwa katika namna tunayoitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tulikuwa tunapata mvua nne kwa mwaka, leo tunapata mvua mbili kwa taabu na zikija hizo mvua basi ni laana maana yake ni mafuriko, uharibifu. Likitoka jua ni hivyo hivyo, kwanini? kwamba sisi wenyewe hatujabadilika kwa hiyo na sisi wenyewe lazima tubadilike. Oman ilikuwa jangwa, walikuwa miaka miwili hawaoni mvua, mvua ikinyesha ni ajabu leo wanapata mvua nne, kwanini? Wao wenyewe wamebadilika. Kwa hiyo na sisi lazima tubadilike na tuelewe kwamba tumeletwa

ulimwenguni kwamba tuvitawalie hivi, Je tumebadilika nafsi zetu? Tunalijua hilo? Kwa hiyo na sisi wenyewe lazima tubadilika na ndiyo maana sasa mvua hizi zinaleta mafuriko, zinaleta athari kubwa, kilimo kinaharibika, matokeo yake sasa ni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hapo tu wadudu hawa kuna wadudu sasa hivi matunda haya yote kuna vidudu dudu hivi mapapai yanaharibika, maembe, ndizi, wale wadudu weupe sijui mnawaitaje sijui sigatoka, sijui wenyewe wataalam mnawaitaje. Wataalam wa kilimo kwa miaka nenda miaka rudi hakuna mabadiliko yoyote. Yote haya yanababishwa na kubadilika kwa haya mabadiliko ya tabianchi ambayo tunayababisha sisi wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, tunasema kwamba theluji inayeyuka katika Mlima Kilimanjaro, wenyewe Wachaga wa Kilimanjaro wanaita Kibo. Sasa kwa maana ile Kibo ikipotea maana yake na Mlima Kilimanjaro unapoteza thamani yake tutakuwa tunajivunia nini kama Watanzania? Kwa hiyo, vyote hivi ni vitu ambavyo tunatakiwa tuviangalie sana. Lakini jangwa linaongezeka kwasababu sisi wenyewe ambao tumeambiwa tuitawale dunia ndiyo wakataji wakubwa wa miti, ndiyo wachomaji mkaa, ndiyo wachomaji wa moto kwenye misitu, kwa hiyo, ni sisi wenyewe na ndiyo maana nikasema tunalichukulia uzito kiasi gani? Sisi kama wananchi, kama binadamu ambao tmeletwa tuvitawale hivi tunalichukulia hili suala la mabadiliko ya tabianchi kwa thamani kiasi gani, kwa nguvu kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni nini athari yake? Wanaoathirika sana ni wakulima na wavuvi. Tabianchi ikibadilika, wakulima hawa watalima hawavuni kwa sababu hizo nilizotitaja ama kwa mafuriko ama za jua ama za wadudu waharibifu hawatavuna na matokeo yake sasa tutakuwa tunawasema watalaam wa kilimo, sijui madawa, sijui hatuna watu ugani lakini ni tabianchi tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tabia hizi zikibadilika, mazingira yakibadilika, hali ya hewa ikibadilika na maradhi

yatakuja. Zanzibar nime-*check* mara hii pale mwezi Januari na Februari ongezeko la wagonjwa wa *pressure hospitali* pale ni kubwa sana, kwa sababu gani? Ya joto tu limeongezeka. Kwa hiyo, hizo ni athari za moja kwa moja tunaziona lakini wavuvi pia samaki watakosekana, wakikosekana samaki inamaana hao nao wanaathirika. Kwa hiyo, ikifa hii *ecosystem* yote ina maana na kizaizi chetu kinachokuja hakitaona mimea na ndege na wanyama ambaو walikuwepo wa asili hapa kwa hiyo, lazima tuwe *serious* na hili ili tuone kwamba kizazi chetu kinakuja kufaidika kwa kiasi gani, nini tufanye?

Mheshimiwa Naibu Spika, waathirika wa masuala haya duniani asilimia 20 ni wale watu maskini kabisa na ndiyo hao wanaoathirika kwa sababu wao ndiyo wanaoishi huko kwenye miti, kwenye misitu na huko vijijini kwa hiyo, hao ndiyo watakaoathirika. Sasa hili suala linalozungumzwa la *global warming* basi ioneerane sasa kwamba inafanyakazi vizuri na iwfakie wale walengwa. Nitatoa mfano, kwa mfano, kuna hizi kaya maskini ambazo zinasaidiwa sijui shilingi 20,000 kwa mwezi hivyo inamsaidia nini mtu wa kaya maskini? Yeye ni masikini unampa shilingi 20,000 kwa mwezi inamsaidia nini? Pesa ambayo hata mtoto wangu na mtoto wako Mheshimiwa Naibu Spika haimtoshi kwa mwezi kwenda shule tu.

Sasa unamsaidia mtu wa Kaya maskini sasa nadhani hizi pesa Mheshimiwa Waziri hebu zipangiwe sasa utaratibu ili kama tuna tatizo sehemu fulani twende tuka-*solve* hilo tatizo na hizi pesa tusiwe tunazigawanya kisiasa siasa tu, kupendezeshana pendezeshana tu hali ni mbaya ni lazima tuwe *commited* katika kuyatafutia suluhisho masuala haya vinginevyo itakuwa tunapoteza muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani natoa mfano tu hapa wa *TASAF* kwamba hizi shilingi 20,000 hizi hazisaidii kuondoa yale matatizo na badala yake zinaleta mizozo tu zaidi, mnawapa mnaowajua, mnawapa watu mnachangua na nini kwa hiyo, hebu hii pesa ndogo ambayo

tutaipata katika kufanya haya basi tuipeleke katika eneo ambalo lina tatizo tuondoe tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala haya ya *social protection* (kinga za kijamii) je, tuna *alternative* gani? Maana yake tusiwe tunasema tu wkamba kuna hili, Je, *alternative* yetu ni ipi? Juzi nilikuwa namuangalia Dkt. Kilahama amepunguza yaani wamefanya utafiti, wamepata miti kutoka miaka 14 kuvuna mkaratusi sasa ni miaka nane unavuna katika ubora. Kwa hiyo, *solution* ziwe hizi na tuzieleze sasa kwa jamii moja kwa moja kwamba *solution* ni hii. Kwa hiyo, tufanye vitu vya namna hii na tuwatumie wasomi na watalaaam wetu katika tafiti zao tufanye katika kukabiliana na hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lazima tujitathmini kama Watanzania. Kama haya tunayaona leo na haya dunia inayasema leo tunachukua hatua gani? Tuna gesi lakini bado asilimia 80 ya Watanzania wanatumia mkaa na kuni kama nishati. Kwa hiyo, tuendeleze elimu na tuwasaidie, tuboreshe kurahisisha matumizi ya gesi ili tupunguze sasa hizi athari zinazotkana vinginevyo itakuja kuwa kama hadithi ya biashara ya utumwa. Wazungu ndiyo walioanzisha biashara ya utumwa, wakafaidika, walipopata teknolojia wakawatupia watu wengine wao wakasema ni biashara haramu. Kwa hiyo, na sisi tusipoliangalia hili tutakujakuishia katika historia za namna hiyo.

Kwa hiyo, naomba katika matumizi sasa gesi tunayo tuhamasishe sana ili tuepuke ukataji wa miti na utumiaji wa mkaa na kuni kama nishati na badala yake tuweze kuyatunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yussuf Salim. Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala, tutamalizia na Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia mada hii muhimu ilio mbele yetu. Naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja ilio mbele yetu na naunga mkono hoja hii kwa kutumia hoja ndogo saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza kwanini naunga mkono hoja hii, naunga mkono hoja hii kwa sababu itatuwezesha Tanzania kunufaika na shilingi trillioni 195 ambazo tutaweza kuzipata kwa sababu tu ya kuridhia mkataba huu. Kwa nini nasema tutanufaika na sehemu ya fedha hizi? Fedha hizi trillioni 195 zimetengwa kupitia makubaliano ya Nchi za *ACP* pamoja na Jumuiya ya Ulaya ni bilioni 70 sasa ukiziweka kwa fedha za Kitanzania zinakuja kwenye trillioni 195 na fedha hizi zinaelekezwa kwa nchi 78 Kimsingi kwa sababu nchi wanachama wa *ACP* ni 79, lakini Cuba yeye ni mwanachama mtazamaji, kwa hiyo, yeye hatanufaika hata na shilingi moja.

Kwa hiyo, ukigawa fedha hizi kwa nchi zote za *ACP* ni fedha nyingi sana na fedha hizi zinalenga kuelekezwa kwenye *Global Climate Change Alliance* ambayo inalenga katika kutekeleza huo mkataba wa Paris. Lakini pia ni fedha ambazo zitatusaidia sana katika kupambana na mazingira ukizingatia ukweli kwamba rasilimali siku zote huwa hazitoshelezi, kwa hiyo, kila fursa inayojitokeza ya kukuwezesha kupata rasilimali lazima tuichangamkie kwa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa sababu najua kwamba tutaweza kunufaika na fedha hizi lakini nina uhakika kabisa kwamba Wizara imejipanga, wameanzisha mfuko wa kutafuta fedha za kupambaa na mazingira na najua mipango ambayo tayari wameshaiweka ya kuhakikisha wanapata fedha na ndijo maana nalishawishi hata Bunge hili katika bajeti ijayo basi tutenge fedha za kuweka kwenye huo mfuko wa mazingira ili waweze kuandaa miradi mizuri ya kuweza kunufaika na fedha hizi na fedha nynginezo. Kwa hiyo, hiyo ni hoja ya kwanza kwa nini naunga mkono hoja hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hoja ya pili, ukiangalia mazungumzo yaliyokuwepo kuhusiana na masuala ya mazingira nakumbuka pale Brussels tulikuwa na mazungumzo ya muda mrefu kuhusu mkataba huu maana mkataba huu ulizungumzwa maeneo mbalimbali duniani. Ulizungumzwa New York, ulizungumzwa Brussels, ulizungumzwa Beijing hata Tanzania mlizungumza wakati huo sikuwepo nilikuwa Brussels lakini tulipokuwa Brussels tulizungumza pia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja kubwa ambalo lilichukua muda mrefu kuzungumza na kukubaliana ni kukubaliana kwamba ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi, kila nchi itabidi ichangie kulingana inavyoharibu mazingira lakini pia kwa kuzingatia uwezo wake wa kiuchumi. Hoja hii nchi zilizoendelea hazikuitaka sana lakini kwa mara ya kwanza katika dunia hii, nchi za ACPzikaungana na nchi za Ulaya ili kuwa na msimamo wa pamoja wa kwamba katika uharibifu wa mazingira basi kama wewe unaharibu zaidi utatakiwa uchangie zaidi katika kupambana na tabianchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hoja iliyotuchukua muda mrefu lakini nashukuru hatimaye hoja hiyo ilipita na ilipoenda *UN* mataifa yote yakakubaliana na ndio maana tunaita kifungu namba mbili katika mkataba huu kinachosema mataifa yote duniani yatawajibika kupambana na mazingira kulingana na jinsi anavyochangia, ukichangia kuchafua zaidi basi uchangie zaidi katika kupambana na hayo mazingira kwa hiyo, ndio maana nasema naunga mkono hoja hii kwa sababu ni hoja muhimu inatoa fursa hata kwa mataifa ambayo yanachafua zaidi yaweze kuchangia zaidi katika kupambana na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni kwanini naunga mkono haja hii ukiangalia kifungu namba tano kinasema nchi zinazoendelea zitaendelea kusaidiwa kukubaliana na mabadiliko ya tabianchi. Sasa ukisema nchi zinazoendelea na nchi nyingine zenye uchumi kama wa sisi ni kwamba sisi tunachangia kidogo katikakuharibu

mazingira, lakini kifungu hiki kinatuhakikishia kwamba tutaendelea kusaidiwa katika kupambana na mazingira.

Lakini sababu nyingine kwa nini naunga mkono hoja hii ukiangalia sehemu ya pili, kifungu cha 4(2) kinasema nchi zinazoendelea ziendelee kukabiliana na hatua za kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mabadiliko ambayo hakuna mkataba ambao utasaini tu usiokupa wajibu, ni kwamba makubaliano haya tuna wajibu wa kufanya ni upi. Wajibu wa kufanya ni kuendelea kuwa na mikakati na kuonyesha dhamira ya kuendelea kupambana na mazingira ndiyo maana tunapopitisha tunatoa ridhaa maana yake tunakubali kama Bunge kwamba tutaendelea kusaidia Wizara yetu ya Mazingira na Masuala ya Muungano kuiwezesha kuendelea kupambana na mazingira hiyo ndio maana yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukiangalia mwenendo wa bajeti Wizara imekuwa ikpatiwa kila mwaka unaona kwamba ilikuwa si fedha zinazotosheleza mahitaji yao yote basi kwa kupitisha kifungu hiki ninakuwa nina uhakika kwamba sasa tunaenda kutenga fedha za kutosha kwa Wizara ya muungano na masuala ya mazingira ili kuweza kusaidia masuala mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ilio mbele yetu kwa sababu hata mataifa makubwa kama Marekani na Japan sitawataja baadhi ya viongozi kwa sababu kidiplomasia si vizuri kumtaja mtu, wapo waliosema hawatakubaliana na masuala ya *Paris Agreement*, lakini naomba kulithibitishia Bunge hili kwamba mataifa yote makubwa mnayoyajua yaliyokuwa yanaonesha hayatakubaliana na kupambana na mazingira tayari yameweka sahihi na tayari yameridhia, sasa wale waliokuwa na wasiwasi waliojaribu kuonesha kwamba hawatakubali, wameshakubali sioni sababu kwa nini sisi tusiridhie kwa sababu sisi ni wanuifaika wakubwa wa makubaliano hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuridhia maana yake tutaweza kunufaika na *Global Environmental Facility, Adaptation Fund*, pamoja na *Green Climate Fund* na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho hoja ya saba kwa nini hoja iliyo mbele yetu ni muhimu tukiridhia maana yake tunaiambia dunia kwamba tutaendelea kupambana na mazingira, miradi mizuri kama ya Kihansi tutaendelea nayo kuna mradi mzuri sana unaendelea kutekelezwa chini ya ofisi ya Makamu wa Rais mradi kama Ruaha Mkuu, kutunza Ruaha Mkuu kwa sababu tunazungumzia *Green Stiegler's Gorge* huwezi ukazungumzia *Stiegler's Gorge* wakati unaendelea kuharibu mazingira, lakini tunaposema tunasaini, tunaiambia dunia kwamba tutatunza hata mazingira, lakini tutaendelea kutoa elimu, tutaendelea kutunza vyanzo vyta maji, pale *Ocean Road* kuna mradi mkubwa wa kutunza mazingira na zaidi ya nchi 10 kutoka dunia nzima zinakuja pale kuangalia Tanzania tunafanyaje kutunza mazingira kwa hiyo, ni mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hizo saba naunga mkono hoja iliyo mbele yetu kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi moja kwa moja niseme tu kwanza naunga mkono hoja ya kupitisha hili azimio kwa ajili ya makubaliano ya Paris kuhusu kuboresha utekelezaji wa mkataba wa mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kuchangia kwanza tukubaliane na hili Azimio kwa sababu tuna faida nydingi ambazo Mheshimiwa Waziri ameweza kuzieleza kama nchi ambavyo tunaweza kufaidika; la kwanza ni mkakati wa kutekelezwa utunzaji wa mazingira, upatikanaji wa fedha, masuala ya kuweza

kupanda miti ambayo itaweza kunyonya gesijoto, lakini kikubwa ni kwamba uhai wa mwanadamu upo kwenye mazingira, duniani nchi zote tunafanya shughuli za kimaendeleo lakini tunaangalia na uhai wa kwetu sisi wanadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la joto duniani lina athari nyingi sana kama ambavyo tumeweza kuelezwu pamoja ikiwa ni uchafuzi wa mazingira, kuleta ukame, magonjwa, uharibifu wa miundombinu na mambo mengine mengi sasa kwa misingi hiyo tunavyokubali azimio hili na kila nchi kuweza kutaekeleza ili Azimio katika kusimamia kutunza mazingira tutaenda kuonyesha kwamba uhai wetu sisi wanadamu utakuwa na uhakika wa kuwepo na kuishi.

Sasa kutokana na vifungu mbalimbali vyatubali ambavyo vimeweza kuelezwu ningependa kama nchi kwa sababu haya ni mabadiliko yamepitishwa mwaka 2016 basi tuombe kwenye mabadiliko ambayo yatakayofuata mbeleni katika haya maazimio tusisitizwe sana kwenye nchi ambazo zinachangia katika uharibifu na kuleta joto duniani ziweke vipengele ambavyo vitahakkisha kwamba wanatekeleza utoaji wa fedha kwa ajili ya nchi zinazoendelea katika kutunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu spika, hilo litakuwa ni jambo la umuhimu sana katika kuzibana hizi nchi na pia katika mawasilisho imeonekana kuna baadhi ya nchi ambazo zinakuwa haziko tayari zikiangalia kwamba zenyewe zinaathirika zaidi katika shughuli zao za kiuchumi kutokana na kubanwa kwenye shughuli zao.

Kwa hiyo, tuombe katika maazimio mbeleni huko marekebisho ambayo yatafanyika tuone namna ya kuzibana hizi nchi na hasa hizi nchi ambazo tena zilizoendelea zinazoshindana zaidi na zinakuwa zinapingga maazimio kama haya basi tuone namna ya kuzibana ili ziweze kutekeleza kwa namna ambayo na sisi ambao ndio nchi maskini tunaoendelea na ndio ambao wengi tunaotunza mazingira na dunia angalau inakuwa ya ina uhakika kwamba

tutaendelea kuishi duniani kwa sababu ya nchi hizi ambazo tunazoendelea ambazo tunatunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Tanzania asilimia 30 ya nchi yetu iko kwenye uhifadhi kwa hiyo, tuna uhakika wa kuendelea kutunza na dunia ikapata nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuangalia upande wa kimataifa naomba nije kwa upande wa kama nchi Tanzania, tunajua tunazo sheria, tuna sera, na tuna uongozi, lakini ni kwa namna gani tunasimamia hizi sera upande wa mazingira na tunasimamia sheria zetu ili ziweze kutunza mazingira tumeona changamoto sehemu mbalimbali za nchi yetu kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa mazingira na hasa kufanya kazi za maendeleo kutoka kwenye kingo za mito kama sheria inavyosema mita 60 na mita 500 kutoka kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu spika, lakini kuna wamiliki wa mabonde, tunayo TAMISEMI na tunayo Wizara husika ila usimamizi katika maeneo mbalimbali huku hafifu mno matokeo yake shughuli za kibinadamu, za mifugo, za kulima wamekuwa wanaingia mpaka maeneo ya vyanzo vya maji na kingo za mito kwa hiyo inapelekea kuharibu mazingira, na kwa misingi hiyo changamoto mojawapo ninayoiona ni uweshehaji wa Halmashauri zetu kuititia hii Wizara jinsi gani wanazishikisha katika kusimamia na kikubwa pia tunashindwa kuwatumia namna fulani sijapenda kuielewa Wakuu wetu wa Wilaya ambaa ni Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama katika Wilaya kwanza hawana *OC* za kutosha kuweza kuzunguka na kusimamia vizuri watendaji walio chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe Serikali tuangalie namna gani tunaongezea *OC* Wakuu wetu wa Wilaya waweze kusimamia Halmashauri zetu katika kulinda mazingira na kijumla maana imekuwa ni changamoto na mpaka maeneo mengine Wakuu wetu wa Wilaya hawana vyombo vya usafiri vya kutosha au vingine vimechakaa na havifai katika utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la kiuongozi kiujumla jinsi gani tunashirikisha kuanzia Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Kitongoji katika kulinda mazingira elimu je, wanayo na inatumika ipasavyo kwa hiyo tuombe tena Wizara tuone namna gani tunawashirikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la nishati katika matumizi ya kawaida ya nyumbani mambo ya kupikia mkaa na kuni ndio vinatumika kwa asilimia 98 na je, mkakati wa Serikali katika kulinda mazingira nishati mbadala kwenye matumizi ya nyumbani mkakati uko namna gani, matumizi ya mkaa kwa mfano Jiji la Dar es Salaam ndio linaloongoza katika nchi hii je nishati mbadala iko vipi, tuna taasisi za Serikali sasa hivi wananchi wengi na wataalam wengi wanatengeneza *biogas* kwa kupitia taka na vyanzo vingine na wanatumia kwenye matumizi ya nyumbani kwa ajili ya kupikia, sasa mkakati wa Wizara hii husika kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais hili fungu linalopatikana toka kwenye nchi wahisani wanaotoa kwa ajili ya kutunza mazingira watenge kwa ajili ya kuelemisha na kufundisha na watu kuwawezesha kutumia *biogas* kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa mfano unaweza ukaanza na taasisi kama Magereza, taasisi hizi kama vyuo vikuu, mashule watengeneze *biogas* kwa ajili ya kupikia. Hizi shule za bweni maana yake wanapikia wanafunzi chakula je, wanatumia nishati gani? Pia tukienda kwenye shughuli za kilimo kwa mfano mazao ya biashara kama tumbaku sasa hivi wakulima wanakausha tumbaku, wanakata miti sawa Serikali imeleta mabanio ambayo kidogo yanatumia kuni zile ndogo ndogo chache, lakini wengine hawatekelezi je tuna nishati mbadala tuache kukata miti?

Kwa hiyo, niombe sana Serikali kupitia hii Wizara waje watueleze *biogas* na nishati mbadala tuachane na mkaa na kuni katika kupikia ambayo ndio inayokata miti sana katika nchi yetu namna gani tunaenda kuwawezesha kwa kupitia haya mafungu yanayotoka kwenye nchi zilizoendelea zinazotoa kwa ajili ya kusaidia kupunguza athari za ongezeko la joto humu duniani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia niombe sasa kwa upande wa hizi halmashauri mlizilazimishsa kwamba Serikali ilisema kila Halmashauri ipande miti 1,500,000 na waliweka kwenye bajeti sasa utekelezaji mpaka sasa hivi kila halmashauri wamepanda miti mingapi hiyo utakuta ni hafifu na watu hata wakipewa ile miti, je, wanaisimamia wanahakikisha kwamba na inakua kwa hiyo, usimamizi katika upande wa mazingira tuone namna gani tunaongeza juhudji ili tuhakikishe kwamba utekelezaji wake wa haya maagizo tunayotoa yanasisimamiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni Wizara ya maliasili na utalii ina maeneo mengi yaliweza kuathirika kutokana na watu kuvamia kwa shughuli za kilimo mbalimbali lakini je, tunahusisha vipi kuingia ubia na halmashauri zetu kupanda miti rafiki kama ilivyo katika maeneo mengine kwa mfano kama mazao ya korosho ili tuweze kuboresha hayo maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na la mwisho ni elimu tumesema kwamba tupande miti ambayo itaenda kunyonya gesi je, hii miti tunayowaambia wataalamu wetu huko na wananchi wetu tunawaelimisha kwamba miti hii mnayopanda ndio ambayo itaenda kunyonya gesi elimu hiyo inatolewa na kwa kiasi gani inatolewa na fedha za kusaidia kutoa elimu Halmashauri zetu tunazozipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Kangi Lugola kwa dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu spika, nishukuru kwa kunipa fursa na mimi kuweza kuchangia hoja hii ya Azimio letu la makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya mabadiliko ya tabianchi. Mheshimiwa Waziri wangu atawatambua wale wote ambao

wamechangia kwenye Azimio letu, mimi nigusie baadhi ya maeneo ambayo wachangiaji wameyasema.

Kwanza kabisa chimbuko la azimio hili ni mukutano ambao ulifanyika kule Stockholm na ulikuwa unahu su binadamu na mazingira. Kwa hiyo, utaona ni kwa kiasi gani jinsi umuhimu ulivyo kati ya binadamu na mazingira jinsi wanavyotegemeana. Sheria yetu namba 20 ya mwaka 2004 ya Usimamizi wa Mazingira imesheheni mambo ambayo Watanzania wakiyafuata bila shuruti tutakwenda kutunza, kuhifadhi na kulinda mazingira ya nchi yetu na tutakuwa ni nchi ya mfano katika ukanda mzima wa Afrika na dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo katika sheria yetu mazingira yametajwa kwamba ni urithi katika msingi wa ile sheria kwamba mazingira ni urithi wa kizazi hiki ambacho tunaishi sasa na vizazi vinavyokuja kwa hiyo, wananchi wakielewa umuhimu huo watakuwa katika fursa nzuri ya kujali katika kutunza vyanzo vya maji katika nchi yetu, watajali katika kutunza miti, watajali kila wakati kupanda na kutunza miti na hivyo urithi huu ndio hoja ambayo Mheshimiwa Saleh alikuwa anazungumzia masuala ya urithi, namna ambavyo baadhi ya ndege wanatoweka, baadhi ya miti inatoweka, theruji kwenye Mlima Kilimanjaro inapungua kwa hiyo tutakapokuwa katika fursa hii ya kujitambua kwamba mazingira tunatakiwa uwe ni urithi kwa sasa na baadaye Watanzani tutakuwa katika mazingira mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia suala la kufanyika tafiti hasa kuwatumia wataalamu tafiti hii ya mimea, tafiti ya miti sheria yetu ya mazingira inaaniszha mfuko wa Taifa wa dhamana ya mazingira na mojawapo ya matumizi katika mfuko ule ni katika masuala ya tafiti, ni katika masuala pia ya kuwafadhili Watanzania waweze kusoma katika maeneo haya ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yetu Ofisi ya Makamu wa Rais kwamba bajeti hii inayokuja tuombe Waheshimiwa Wabunge wapitishe tuweze kuwa na fedha za kutosha katika mfuko wa Taifa wa dhamana ya mazingira ili kupitia mfuko huo tuweze kuhakikisha kwamba tunakuwa na wataalam wanaofanya hizi tafiti ikiwa ni pamoja na kuwasaidia wananchi katika kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria yetu ya mazingira kifungu cha sita kimetoa wajibu kwa Watanzania wote kuhakikisha kwamba wanatunza na kuhifadhi mazingira, kwa hiyo sio suala tu la Ofisi ya Makamu wa Rais au *NEMC* kwamba sisi ndio tunawajibika kuhakikisha kwamba wananchi wanatunza mazingira ni wananchi wote.

Niwaombe Waheshimiwa Wabunge nyinyi ndio mko majimboni kule ambako ndiko kuna halmashauri zetu kuanzia Halmashauri za Wilaya, za Miji za Manispaa na Majiji na amezungumzia Mheshimiwa Richard Mbogo masuala ya uelewa kwenye Vitongoji, kwenye Vijiji Waheshimiwa ninyi ndio Madiwani kwenye Halmashauri zenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba kwa kuwa sheria hii kuanzia kifungu cha 36 mpaka 41 kinazungumzia kuwepo kwa Kamati za Mazingira kwenye ngazi za Vitongoji, Vijiji, Mitaa, Kata mpaka Wilaya na kuwepo kwa Maafisa Mazingira hakikisheni kwamba Kamati hizo zipo na zinafanya kazi pale ndipo tutakuwa katika nafasi nzuri ya kulinda na kuhifadhi mazingira kwa sababu mazingira yako kule chini kabisa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala lililozungumzwa sana la hasa kuanzia Kambi ya Upinzani kwamba kuwabana zile nchi ambazo zinachafua mazingira ili waweze kuleta fedha.

Katika Azimio hili kwenye mkataba imewekwa bayana kabisa namna ambavyo hizi nchi zinawajibika kusaidia fedha na tumetaja Mifuko mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa ambako sisi hupata fedha. Tumewaonesha miradi mbalimbali, mingine ambayo Mheshimiwa Lubeleje amesema itaenda kwenye Wilaya yake na baadhi ya Wilaya za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba sisi tutakapotenga fedha za ndani na tukaendelea kupata fedha hizi kutoka kwa wafadhili, ni imani yetu kwamba tutakwenda kuhifadhi na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na wasiwasi Mheshimiwa Mbogo. Anasema kweli, kwenye llani yetu ukurasa wa 213 tumezungumzia kwamba kila Halmashauri hapa nchini lazima kila mwaka wawe na miradi ya kupanda miti isiyopungua 1,500,000 na kwamba, ni kweli hiyo miti ipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba mimi na Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukizunguka nchi nzima ikiwa ni pamoja na kutumia Sikukuu za Mazingira Duniani, tumekuwa tukizunguka na kuhimiza Halmashauri waweze kupanda hiyo miti na kutuonesha kwa macho. Tunajipanga kama sehemu ya mkakati wa Kitaifa ili kuanzia mwakani, kama ilivyokuwa kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Magufuli, akiwa Waziri wa Uvubi, alikuwa na uwezo wa kujua idadi ya samaki kwenye bahari na kwenye maziwa na mito; nasi tutakuwa na sensa ya miti ili tujue kwamba hii miti tunayoambiwa kwenye taarifa mbalimbali wamepanda, je, hii kweli hii miti ipo, ili tuwe na uhakika kwamba mazoezi haya yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mita 60 na wamezungumzia kwenye Kambi ya Upinzani vinyungu kule Iringa na Njombe; wamezungumzia kule milimani kule Kilimanjaro. Niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri alishatoa mwongozo kwamba Halmashauri zote nchini walete orodha ya vyanzo vyote vya maji, pamoja na milima na vilima ili wachanganue kwamba vyanzo hivyo vya maji vina

changamoto gani ili sisi Ofisi ya Makamu wa Rais tuweze kutengeneza mkakati wetu wa Kitaifa ambao unaendelea kwenye *task force* ili tuweze kuwabana hao ambao wanaharibu na kuchafua vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba nchi hii ambayo tumekuwa tukisema Mataifa yanayochafua na kuharibu mazingira, hasa kwenye hewa ya ukaa ambayo inakuja mpaka huku na kuleta athari za mabadiliko ya tabianchi kwamba tuzibane zilete fedha; sisi kwa kutumia Sheria ya Mazingira tunawabana wananchi watumie fedha katika kuhifadhi na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawabana wawekezaji na hasa wenyewe viwanda kuhakikisha kwamba katika uwekezaji wao, nao wasiangalie tu sehemu ya faida, waangalie pia kuweka mifumo rafiki ambayo itahakikisha kwamba wanalinda na kuhifadhi mazingira ili siku ya siku Tanzania ya viwanda ambayo Mheshimiwa Rais ni *champion* kuhakikisha kwamba Tanzania ya Viwanda inaenda sambamba na kuzingatia sheria za kutunza na kuhifadhi mazingira. Kwa hiyo, tutaendelea sisi Ofisi ya Makamu wa Rais kuwa wakali sana kusimamia sheria hii ili Watanzania wote wahakikishe kwamba wanatunza na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala aliloligusia Mheshimiwa Lubeleje. Mheshimiwa Lubeleje amegusia suala la Mpwapwa. Mheshimiwa Waziri wangu alishaniagiza niende Mpwapwa ambako wananchi wanaendelea kukata miti ovyo kwenye vilima, wanaharibu vyanzo vya maji na kuchoma moto ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule moja ya sekondari ambayo inasemekana kuna mwananchi mmoja alienda akakata miti ya shule ambayo wao walikuwa wameipanda kwa ajili ya kuhifadhi mazingira. Kwa hiyo, nitoe wito kwa nchi nzima, siyo Mpwapwa tu kwa Mheshimiwa

Lubeleje, kwamba suala la kisingizio cha kwamba tunatumia kuni, tunatumia mkaa, vijjini kule wananchi wengi hawatumii mkaa, mkaa mwingi unaenda mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Serikali imeshajipanga kuhakikisha kwamba kupitia Wizara ya Nishati wanaanza kusambaza gesi katika Mji wa Dar es Salaam ambapo tunaamini sasa tunaenda kuwa na nishati mbadala kwa njia ya gesi ili tuanze kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi nyingi za Serikali yakiwemo Magereza, Hospitali na shule, tumeshawapa mwongozo na maelekezo kwamba waache sasa kutumia kuni na mkaa, waende kwenye nishati mbadala. Wazo zuri alilolitoa hapa Mheshimiwa Mbogo, kuwa shulen i kwenye *bio-gas*, kuna baadhi ya shule ambazo tayari tumeanza kuzitembelea kwamba wana-recycle, wana *bio-gas* ili sasa kupitia Bunge lako tutakapopata uwezeshaji wa kibajeti, tuanze kupita kwenye shule na taasisi nyingine ambazo nimezitaja kama majeshi na shule ili waanze kuwa na nishati hii ya *bio-gas* ili tupunguze ukataji wa miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mtoha hoja, Mheshimiwa January Makamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Mazingira na Muungano).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA NA MUUNGANO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru tena, lakini pia naishukuru Kamati kwa maoni mazuri waliyoyatoa na ushauri tutauzingatia wote. Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Ally Saleh Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye masuala ya Mazingira na Muungano. Bahati nzuri yeye ni mwanamazingira mzuri, ametoa mawazo mazuri na tutayazingatia hasa la kushirikisha wadau zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ia suala la baadhi ya vipengele ambavyo vimezungumzwa kwa ujumla na hakuna ufanuzi kuhusu utekelezaji wake. Nataka nimweleze tu kwamba majadiliano bado yanaendelea kuhusu namna ya utekelezaji wa makubaliano haya. Kwa hiyo, mambo mengine aliyoyazungumza yatapatiwa majawabu na ufumbuzi mara pale mazungumzo kuhusu utekelezaji wa mkataba huu yatakapokwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kujibu karibu mambo yote yaliyozungumzwa na kwa kwa ufasaha kabisa na kwa kweli zaidi ya hapa nampongeza, mwanzo nilisahau kumshukuru kwa mchango wake na kazi nzuri anayoifanya katika ofisi yetu ili kusaidiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Lubeleje amezungumza kwa hisia sana kuhusu masuala haya na namshukuru. Wakati mwingine utu uzima unasaidia kuonesha tofauti. Asilimia 50 ya Watanzania ni watu wa umri wa chini ya miaka 18. Asilimia 44 ya Watanzania ni watoto chini ya miaka 14. Kwa hiyo, unapokuwa na Taifa la watu wengi ni wenyе umri mdogo, wanakuwa hawajapata kuona nchi ilikuwaje miaka iliyopita na ilivyo sasa. Kwa hiyo, wanaona huu uharibifu uliopo na hali iliyopo sasa ndivyo nchi ilivyo, kwa hiyo, wanakosa uchungu na hamasa ya hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mzee Lubeleje, amekula chumvi nyingi na anaposema hasa kwamba miaka ya 1960 nchi hii haikuwa hivi, ni kweli, ana ushuhuda kwa sababu ameona ilivyokuwa huko. Kwa kweli tungependa yeye na wazee kama yeye wapate nafasi hizi za kutuelimisha sisi vijana, tuone kwamba uoto wa asili na *landscape* ya nchi yetu, kwa kweli inaharibika kwa haraka sana katika miongo hii kadhaa aliyoshi, ambayo vijana wengi wa sasa wataishi, hali itakuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa ushuhuda wake. Kama nilivyomwelekeza Naibu Waziri, atakwenda Jimboni kwake. Kwa kweli hali ni mbaya,

ndiyo maana tumepeleka huu mradi mmoja Jimboni kwake kwa ajili ya kusaidia watu wa Mpwapwa. Nafahamu kuna habari ya makorongo mengi yanayopitisha maji na kuharibu mazingira na Naibu Waziri atakuja kuyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Salum, amezungumza kwa hisia sana na kwa kweli ametufundisha na kutueleza jinsi gani baianuai inavyopotea. Kwenye kisiwa kama cha Zanzibar ambapo eneo ni dogo na utajiri wa Zanzibar; utajiri wa Tanzania kwa kweli haupo chini ya ardhi peke yake kwa maana ya madini. Utajiri ni kwenye maarifa ya Watanzania lakini pia ni kwenye uoto na mimea na wanyama ambayyo Mungu ametujaalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya nchi hapa duniani zina aina chache sana za mimea, aina chache sana ya wanyama, ndiyo maana wanakuja huku na dunia inavyoenda kuna baadhi ya nchi hata sauti ya ndege watoto wanaozaliwa miaka inayokuja watakuwa hawaijui mpaka waje kwetu. Sasa na sisi tukipoteza ndege wale, ina maana vizazi vijavyo tutakuwa tunahadithiana kwamba, bwana kuna ndege fulani aliishi miaka hiyo alikuwa na rangi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utajiri mkubwa kabisa wa nchi yetu ni baianuai (*bio-diversity*); wingi wa mimea na wanyama. Sasa huu mkataba tunaouzungumza leo, makubaliano haya yapo chini ya makubaliano ya *UNFCC United Nations Convention of Climate Change* na siku ile yale makubaliano yalivyowekwa sahihi kule Brazil kulikuwa na mkataba mwingine unaitwa Mkataba wa Uhifadhi wa Baianuai (*Convention on Biological Diversity*) ambao sisi ni wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule mkataba unatoa fursa nydingi za kuhifadhi baianuai. Pia unatoa nafasi ya nchi yetu kutajirika na kunufaika na baianuai yetu tuliyonayo. Baianuai siyo kwa maana tu ya kuja kuitazama, lakini kuitumia kwenye tiba, utafiti na kadhalika. Mnafahamu madawa yote yanatokana na miti; na mnapoharibu miti na mimea

mnapunguza uwezo wa kujitibia siku zijazo. Kwa hiyo, uharibifu wa mazingira ndugu zangu unahusu pia hata tiba yetu kwa miaka inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashukuru kwamba hilo tumelizungumza na sisi kama Serikali, tunaendelea na utekelezaji wa mikataba yote hii miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Mbunge amezungumza kwamba tubadilike. Leo tunazungumza mabadiliko ya tabianchi lakini inawezekana cha kwanza kinapaswa kuwepo ni mabadiliko ya tabiamtu ili tuweze kudhibiti mabadiliko ya tabianchi. Kwa sababu kama mabadiliko ya tabiamtu hayatokei, itakuwa ni vigumu sana kudhibiti mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumezungumzwa pia kuhusu kuni na mkaa na Mheshimiwa Mbogo vile vile amezungumza kuhusu kuni na mkaa. Nataka nizungumze kwamba sisi tunaangalia matumizi ya nishati hizi za tungomotaka wanaita (*biomass*) katika suala zima la *deforestation* na *landscape degradation*, kwamba huu uoto unaouona, ardhi, mimea; hii *landscape* ya nchi yetu inayopendeza, kasi yake ya kuharibika ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo, ufugaji, utalii maji, zote zina uhusiano na hifadhi ya mazingira. Kwa hiyo, tunapopata uharibifu wa *landscape*, huu uoto, hizi sekta nyingine zote haziwezi kufanikiwa. Kwa hiyo, uchumi wa nchi yetu na ukuaji wa uchumi na umaskini na ustawi wa watu, unafungama moja kwa moja na hifadhi ya mazingira. Huwezi kutofautisha!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunasema hapa, tunataka kuhamasisha Wabunge wote wawe wanamazingira. Kama unataka kuzungumza maji Jimboni kwako, huwezi kuyapata bila hifadhi ya vyanzo vyaa maji, bila hifadhi ya miti na kadhalika. Kwa hiyo, nafurahi kwamba waliochangia karibu wote wamesaidia kutoa elimu na wamesaidia kuonesha hisia katika mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye matumizi ya kuni na mkaa, sisi kama Serikali tunashirikiana na tutashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha kwamba tunatengezea mpango mkubwa wa Kitaifa wa matumizi ya nishati. Tayari maelekezo yametolewa kwenye Wizara ya Nishati na Madini kutunga sera mpya ya nishati ya tungomotaka (*biomass policy*) ili tuwe na mwongozo wa namna gani tunapata nishati ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi kinachotokea ni kwamba miti iko vijjini lakini ukataji wake unanufaisha watu wa mijini. Watu wa mijini hawana miti, lakini watu wa vijjini kuni zile wanakata matawi tu. Ili mtu wa mijini apate mkaa, ni lazima akate mti wenyewe, gogo lile. Sisi kwenye shule, Magereza na Mahospitali, hatutumii kuni za matawi tu, ni lazima tukate mti wenyewe. Ukienda unakuta lundo la magogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais tumetumia kifungu cha 13 cha Sheria yetu ya Mazingira ambacho kinasema kwamba Waziri mwenye dhamana ya mazingira ana uwezo wa kuelekeza mamlaka zozote za kisekta, binafsi na taasisi kufanya mambo ambayo yatahifadhi mazingira. Kwa hiyo, tumetoa maelekezo kwa shule, Magereza, hospitali na tumewapa mwaka mmoja kwamba waondokane na matumizi ya kuni na mkaa na tumeanza hapo *UDOM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *UDOM*pale pana wanafunzi takriban 30,000, wanapikiwa chakula mara tatu kwa siku. Sasa hebu fikiria kulisha watu 30,000 mara tatu kwa siku, kiwango cha kuni kinachotumika ni kikubwa sana. Ukienda pale utataka kutoa machozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale tumewaambia ndiyo watakuwa wa kwanza na bahati nzuri tumekubaliana kwamba watu wanaowapa zabuni pale, wote sasa ili upate zabuni ya kupika chakula, hauwezi kupata kama unatumia mkaa au kuni. Kwa hiyo, tutaona mabadiliko

yaliyotokea pale *UDOM* yatatusaidia kutoa mfano kwenye taasisi hizi kubwa zenyе watu wengi kuhusu kuondokana na hili suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni jambo ni kubwa, sisi kama Serikali tunalichukulia kwa uzito wake. Matumizi ya nishati nchini yanafungamana na umaskini kwamba masikini zaidi ndio wanagharamia nishati zaidi. Pia tuisahau kwamba wewe unatoka Pemba; ukitazama mkaa unaopelekwa Pemba kutoka bara, haulingani na idadi ya watu walioko Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule kwenye hizi bandari za kwetu; Mbweni, Bagamoyo utaona magunia ya mkaa yanaenda Pemba. Unajua yanaenda wapi? Hayaendi Pemba, yakifika Pemba yanaenda shimonii, Mombasa. Yakifika Mombasa yanapakiwa vizuri yanaenda Somalia au Uarabuni kuchoma kondoo vizuri. Maana wale wanataka kuchoma kondoo na mkaa mzuri; na yakienda Somalia yanasaidia ku-*finance Al-shabaab*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkaa wetu tunaweza tukauona hapa ni jambo la kawaida lakini una muunganiko na *value chain* kubwa sana ambapo wote kama Serikali na Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo ndiyo inahusika moja kwa moja na haya mambo, inabidi tukae tupange vizuri. Kwa sababu siyo tu kwamba mkaa unaokatwa nchini unatumika nchini, unaenda nje ya Tanzania vile vile. Kwa hiyo, tunakata miti yetu sisi kwa manufaa ya watu wengine huko nje ya Tanzania. Kwa hiyo ni suala la kulizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia matumizi bora ya ardhi. Moja ya changamoto kubwa inayosababisha sisi tushindwe kuhimili mabadiliko ya tabianchi ni kwamba tuna kilimo hiki cha kuhamahama. Mtu anavamia msitu, analima mtama misimu miwili, ardhi ikiharibika anakata tena kipande kingine cha msitu. Kwa hiyo, baada ya miaka michache unakuta msitu wote umefyekwa. Au wale wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi kama nchi, wajibu wetu ni kuweka taratibu za kutumia vizuri ardhi. Kielelezo na shabaha ya maendeleo ni kutumia ardhi kidogo kuvuna zaidi. Nitatoa mfano, nchi ya Uholanzi, eneo lake ni dogo kuliko Mkoa wa Katavi, yaani Mkoa wa Katavi ni mkubwa kuliko Uholanzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uholanzi ni nchi ya pili duniani kwa kuuza bidhaa za kilimo pamoja na kuwa na eneo dogo. Ukiiondoa Marekani, inakuja Uholanzi. Uholanzi wanaauza dola bilioni 90 za mazao ya kilimo kwenye eneo kama la Mkoa wa Katavi. Kwa hiyo, ndiyo kielelezo cha maendeleo. Nasi tunaweza kufika huko. Wanafanya hivyo bila kutumia *GMO* wala nini, ni kilimo tu endelevu na wanahifadhi mazingira na ni kuzuri. Kwa hiyo, naamini maendeleo yetu yatafikiwa tutakapokuwa tumefanya mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbogo nashukuru sana kwa mchango, nimekupata. Tutashirikiana na Serikali za Mitaa na tumezungumza na wenzetu wa Wizara ya Fedha, Naibu Waziri yupo ananisikia, tumependekeza kwamba kila Wizara na kila Halmashauri iwe na *budget code* yaani zile...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba urudi ukae kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28 fasili ya (2), nakusudia kuongeza nusu saa ili tuweze kumaliza shughuli tulizonazo mbele yetu. Vile vile fasili hii inanitaka niwahoji ili tuweze kukubaliana. Kwa hiyo, nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, tunaendelea ili tuweze kumaliza shughuli zetu za leo.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa pendekezo kwamba, saa yetu ile pale mbele itengenezwe. Kumbe inakuwa sahihi mara mbili kwa siku. Naona imesimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiliwa nasema kwamba, kuhusu mapendekezo ya Mheshimiwa Mbogo kuhusu ushirikishwaji wa Halmashauri na viongozi kwenye maeneo yetu ya vijiji, Wilaya na Halmashauri tutayachukua, tumeyazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mipango yetu katika Ofisi yetu ya Makamu wa Rais ni kufanya kazi kwa karibu zaidi na Serikali za Mitaa. Katibu Mkuu anayo maelekezo yetu kuandaa mikutano baina ya ofisi yetu na Serikali za Mitaa kwenye *level/ya Mawaziri, Makatibu Wakuu,* lakini pia kujaribu kutumia fursa za vikao mbalimbali vilivyopo ikiwemo vikao *nya RCC ili kuweza kwenda kutoa elimu kwao,* lakini kuweka makubaliano ya ushirikiano ikiwemo ushirikiano katika kuhakikisha kwamba Sheria ya Mazingira inazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata baadhi ya masuala ikiwemo ya usimamizi wa sheria, ikiwemo ya kufanya hizi habari za tathmini ya athari kwa mazingira, baadhi ya mambo tunafikiria kuyakasimu kwenye Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, mpango huo upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali kabla sijakaa, itapendeza kama tutakubaliana ndani ya Serikali kuwa na *budget code,* ili kila Halmashauri katika bajeti yake iwe na sehemu inasoma namba zile, “Hifadhi ya Mazingira,” ili fedha ziweze kupangwa kwa ajili ya hawa Wakuu wa Wilaya, kama ulivyosema, wapate *OC* ya kuzunguka na kusaidia kwenye hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupanda miti, Naibu Waziri amelizungumza kwamba tutalipa msukumo mpya na tutafanya sensa ya miti. Pia, niseme tu kwamba, kama tulivyozungumza kwenye Azimio kwamba pale Morogoro tumeanzisha kituo kinaitwa *National Carbon Monitoring Centre* ambapo kuna teknolojia ya kujuu kasi ya uharibifu wa mazingira maeneo ambayo miti inahitaji kurejeshwa. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Maliasili ni mhusika pia kuhusu masuala ya misitu, kwa hiyo, tutashirikiana naye kuhakikisha kwamba tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi kuhusu misitu, siyo kupanda miti mipyä, ni kutokata iliyopo. Katika miti yote iliyopo Tanzania, 95% ni ile iliyokuwepo, 5% tu ndiyo iliyopandwa. Kwa hiyo, ili ufanikiwe zaidi kwenye hili jambo, usikate miti, bali uhifadhi ile ambayo haijakatwa na hiyo itatusaidia tutakapowezesha watu kutotegemea miti zaidi katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Kamala kwa hoja nzuri alizoziwasilisha za sababu ya kuunga mkono. Tunakushukuru na tunakubali kwamba sisi kuridhia haya makubaliano kutatusaidia kuweza kupata fursa. Zaidi tunafurahi kwamba yeche kama Mbunge, anaona haja ya Serikali kuwa na rasilimali nyingi zaidi na Bunge mna wajibu pia wa kupanga fedha kwa ajili ya hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa fedha kwa ajili ya hifadhi ya mazingira haziko kwenye bajeti peke yake, ziko namna nyingi ikiwemo Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Mazingira ambapo kwenye sheria ile unategemea moja ya vyanzo vilivyoandikwa vya Mfuko, nacho ni *subvention appropriation* kutoka kwenye Bunge, ukiondoa kwenye bajeti. Kwa hiyo, Bunge lina uwezo wa kuamua lenyewe kwamba licha tu ya bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, pia tunaweza kabisa kupangia Mfuko wa Mazingira kiasi fulani cha fedha na Mfuko huu utakapopata fedha hizo, basi utatuwezesha kufanya kazi zetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nadhani nimeweza kuzungumza yote yaliyozungumzwa, lakini niseme tu kwamba, ushauri uliotolewa tutauzingatia. Tunaomba sasa utusaidie namna ya kwenda kwamba, tunatoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge. Sasa tutaendelea na utaratibu wetu, nitawahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja illamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (The Paris Agreement Under the UN Framework Convention on Climate Change) lilipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, Bunge siku ya leo limepitisha Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Paris Chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (*The Paris Agreement Under the UN Framework Convention on Climate Change*).

Kwa hiyo, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kuweza kufanya kazi Makubaliano haya na mpaka Bunge kuweza kupitisha Azimio. Tuwatakie kila la heri katika utekelezaji wa mambo ambayo ni mazuri sana mliyotueleza kuhusu Azimio hili na umuhimu wake. Nasi tunaamini kwamba Serikali mtalitendea haki ikiwa ni pamoja na kutekeleza yale yote ambayo yamewekwa kwenye Azimio hili ambalo limepitishwa na Bunge leo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa; na kwa kuwa, hili jambo huwa linajitokeza kila wakati, nalazimika kutoa maelezo kidogo kuhusu namna Bunge linavyofanya kazi. Kwa sababu tunaelekea kwenye Bunge la Bajeti, ili Wabunge twende wote kwa uelewa mmoja ni vizuri haya maelezo ambayo yako kwenye kanuni zetu, wote tukayaelewa.

Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 118 inaeleza kwamba kutakuwa na Kamati za Kudumu za Bunge kama zilivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizi. Ukienda kwenye Nyongeza ya Nane inazitaja Kamati zote za Kudumu za Bunge tulizonazo. Pia inataja majukumu ya kila Kamati na Wizara ambazo Kamati zinasimamia.

Sasa Kamati hizi zimeundwa na Waheshimiwa Wabunge, ndio wanaokaa kule. Wanapokuwa wanafanya kazi, wao wana muda mrefu zaidi wa kushughulika na mambo ambayo yanapelekwa kwao na Wizara husika. Kwa hiyo, yanapoletwa hapa ndani ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wameshafanya kazi kwenye Kamati zao. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Kamati inapoleta maoni hapa, ama mapendekezo, ni kwa ajili ya kututaarifu sisi ambao sio sehemu ya Kamati ile tuweze sasa kuwaelewa wao wamewalewaje hao watu wa Serikali? Kama wamekataa, watatueleza kwamba jambo hilo sisi kama Kamati tunalikataa. Ama kama wamekubali, Kamati itatueleza sisi Bunge zima kama wamekubali na sababu zao. Ndiyo maana ni lazima Serikali ikishasema jambo lake, Kamati inakuja kusema kwa niaba ya Bunge. Hapa tunaletewa kwa ajili ya kufanya maamuzi. Ndiyo kanuni zetu zinavyosema. Kazi zetu kubwa zinafanyika kwenye ngazi ya Kamati. (*Makofi*)

Kwa hiyo, isitokee mazingira yale ambayo Waheshimiwa Wabunge tunaona kwamba, tunapokaa hapa ndani mambo yanayoletwa na Serikali baadaye Kamati inaleta mapendekezo yake na baadaye Kambi Rasmi ya Upinzani inapewa fursa ya kuzungumza, ni kwa sababu wamepata muda wa kutosha wa kuyapitia mambo haya.

Ninyi ni mashahidi, pale ambapo Kamati inakuwa haijakamilisha kazi zake, maana yake ni Bunge halijakamilisha kazi, kwa hiyo, Mheshimiwa Spika hapangi shughuli hiyo kuingia humu ndani kama Kamati haijamaliza kazi yake. Kwa hiyo, inapokuja hapa ndani, hakuna muda ambao Mheshimiwa Spika analazimika kwamba jambo hili ni lazima lifanywe kwa muda fulani ili Waheshimiwa Wabunge 393 tulioko humu ndani wote tupate nafasi ya kuzungumza.

Kwa hiyo, utendaji wetu wa kazi uko kikanuni; na kwa hiyo, mambo yote yanayofanywa na Kamati yanafanywa kwa niaba ya Bunge na kwa hiyo, ufanuzi wote unaotolewa na Kamati hapa mbele ni kwa niaba ya Bunge. Hapa ndani ni kwa ajili kufanya maamuzi yale ambayo wenzetu wameshayajadili kwenye ngazi ya Kamati. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ukisoma hii Nyongeza ya Nane, hasa fasili ya (7) katika hiyo nyongeza, inasema hivi; "Majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta yatakuwa yafuatayo:-

"(a) Kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia."

Maana yake bajeti inaenda kwenye Kamati. Inapoletwa hapa, Kamati inapata nafasi ya kutueleza, wamesikia nini kule? Ndio utendaji tuliokubaliana nao. Siyo kwamba inapokuja hapa Bungeni ndiyo tunaanza kushughulikia moja, kwa sababu Wizara inakuwa ilishapeleka kwenye Kamati. Pia, hata kwenye hili, kwa mfano tunalishughulikia leo, (b) inasema, "Kushughulikia Miswada ya Sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia."

Kamati yetu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ndiyo inayosimamia Wizara hii ya Mazingira na Muungano. Kwa hiyo, inavyoleta maoni hapa ndani ni kwamba Bunge limeshafanya kazi kule kwenye ngazi ya Kamati. Kwa hiyo, inatuletea hapa ili sisi tujue na tufanye maamuzi juu ya yale ambayo Kamati inapendekeza. Yako

mambo mengi, Waheshimiwa Wabunge, niwashauri tuzipitie hizi kanuni vizuri ili sisi wenyewe tuwe tunaridhika na kazi tunayoifanya, lakini pia, tujue mipaka yetu na majukumu yetu yanaenda mpaka wapi?

Waheshimiwa Wabunge, pia mnaruhusiwa kikanuni, kwenda kwenye Kamati yoyote unayoona wewe inajadili jambo ambalo unataka kulifahamu zaidi ama ungependa kushiriki zaidi. Hakuna kanuni inayokukataza, isipokuwa hutaruhusiwa kupiga kura.

Kwa hiyo, tunapoenda kwenye bajeti za hizi Wizara, usije ukaona mtu kwamba, Wizara fulani bajeti yake hapa imepangiwa siku moja ukaona ni muda mfupi; hakuna muda mfupi kwa sababu, Kamati ulioichagua wewe ndiyo ambayo imefanya kazi hiyo.

Ninavyosema umeichagua wewe, ni kwa sababu sisi wote tumekasimu mamlaka hayo kwa Mheshimiwa Spika, aliyempangia Kamati hiyo, anajua atafanya kazi nzuri kwenye lile eneo. Kwa hiyo, tunavyoletewa hapa ndani, tukipangiwa siku moja, tukipangiwa siku mbili ni kwamba kwa tathmini imeonekana Kamati hiyo imefanya hiyo kazi na siku moja hiyo inawatosha kutueleza yale ambayo wameyapitia. (*Makofii*)

Kwa hiyo, kwa sababu, huwa linajitokeza tokeza, naamini kwamba hata Waheshimiwa Wabunge ambao hawako pamoja nasi hapa, watapata haya maelezo ili mtu anaposimama aendelee na mchango wake kuliko kulalamikia muda maana Kamati, Wabunge wale wanakuwa wamefanya kazi kama Mbunge mwингine aliye kwenye Kamati nyingine. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, tarehe 4 Aprili, 2018, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.15 Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,  
Tarehe 4 Aprili, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*